

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA NNE**

**Kikao cha Kumi - Tarehe 16 Februari, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kikao cha Kumi cha Mkutano wa Kumi na Nne kinaanza. Lakini kabla hatujaanza, nina maelezo ya ufafanuzi kuhusu *Order Paper* ya leo, natafuta Kanuni namba 82 ambayo inatuelekeza kama ifuatavyo:-

Inasema hivi: "Masharti ya Kanuni zote zinazohusu Makadirio ya Mwaka ya Matumizi ya Serikali, yaani Bajeti ile ya mwaka, yatumika pia kwa Matumizi ya Nyongeza (*supplementary*)."

Sasa leo ni kikao cha *supplementary*. Miongoni mwa Kanuni hizo, inahusu Kanuni za muda wa maswali, wakati wa Mkutano wa Bajeti huwa maswali yanaisha baada ya saa moja. Sasa leo ni Kikao cha Bajeti Ndogo maswali yatakwishaa saa nne, yaani baada ya saa moja. Lengo ni kutoa muda zaidi kwa ajili ya kujadili Bajeti yenyewe, ndiyo ilikuwa lengo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo sasa tunaanza.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 120

**Ziara za Viongozi Wakuu Mkoani/Wilayani**

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa Viongozi wetu wa Kitaifa yaani Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, wamejitahidi kufanya ziara mbalimbali Mikoani na Wilayani; na kwa kuwa katika ziara zao ipo Mikoa na Wilaya zilizotembelewa mara nyingi na nyingine zinatembelewa kwa nadra sana na yapo maeneo ambayo viongozi hao hawajawahi kufika tangu tupate uhuru kwa mfano katika Wilaya ya Songea kuna Kata ya Matumbi na Vijiji vya Ifinga, maeneo hayo hayajawahi kutembelewa na Viongozi wa Kitaifa, ingawa Wamisionari wa Kijerumani walijenga Kanisa, Shule ya Msingi na Zahanati mnamo mwaka 1928, vile vile kwenye Wilaya hiyo hiyo kuna Kata za Kila - Gano, Mhukuru na Magagura ambako nako viongozi wetu hawajawahi kufika tangu tupate Uhuru:

Je, Serikali inaweza kuandaa *Matrix* ikionyesha ziara za viongozi wetu wa Awamu ya Tatu kwenye Mikoa na Wilaya walizowahi kutembelea?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, Viongozi wetu wa Kitaifa wa Awamu hii ya Tatu, yaani Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, wamejitahidi sana kufanya ziara mbalimbali Mikoani na Wilayani, katika kuhimiza shughuli za maendeleo na kuzungumza na wananchi.

Mheshimiwa Spika, viongozi wetu wamefanya jumla ya ziara 477 Mikoani na Wilayani. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametembelea Mikoa yote 21 ya Tanzania Bara na ziara 162 katika Wilayani zote, ikiwemo Wilaya ya Songea. Mheshimiwa Makamu wa Rais, ametembelea Mikoa yote na amefanya ziara 130 Wilayani ikiwemo Wilaya ya Songea. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametembelea Mikoa yote, ziara 185 Wilayani na Songea ikiwemo. Serikali inaweza kuandaa *Matrix* inayoonyesha ziara za viongozi wa Awamu ya Tatu kwenye Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, viongozi wetu wataendelea kufanya ziara Mikoani kila inapowezekana, kwa mujibu wa ratiba zinazopendekezwa na Mikoa yenyewe. Aidha, kutokutembelewa maeneo hasa vijijini ni kutokana na ratiba zinavyopangwa na Wilaya na ni jukumu la Wilaya kupendekeza ratiba zenyewe.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na namshukuru Waziri kwa majibu mazuri ya swali langu. Nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

- (i) Mara nyingi viongozi wakija wanatembelea Makao Makuu ya Wilaya, mara chache wanakwenda vijijini. Je, hilo ni makusudi au ni mawasiliano mabaya kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Mkoa?
- (ii) Kwa kuwa mara nyingi pia baada ya kupanga ratiba wakubwa wana-*cancel* ile safari, huwa hawaji. Sasa nilidhani kuwa ingekuwa bora kama wangeweza kufidia gharama zile maana inakuwa kila siku mbuzi wamechinjwa, kuku. Sasa wangeweza kufidia hiyo kusudi wakati wanakuja waweze kutumia fedha kwa ajili ya maandalizi ya pili? (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):**  
Mheshimiwa Spika, kwanza anasema mara nyingi viongozi hawa wanatembelea Makao Makuu ya Wilaya na siyo vijijini. Sina uhakika sana lakini kwa vyovyote vile viongozi wakifika, kwanza wanafika kama siyo Makao Makuu ya Mkoa, lakini lazima wafike Makao Makuu ya Wilaya, kwa uzoefu wanapewa taarifa ya Wilaya kwa ujumla kwa sababu kwa namna nyingine yoyote hawawezi kutembelea vijiji vyote katika Wilaya. Halafu baada ya hapo ndiyo wanapelekwa katika maeneo ambayo Wilaya yenyewe imeamua, kwa sababu kabla viongozi hawajaenda kuna mawasiliano hufanywa kati ya Viongozi wa Wilaya na Mkoa kupendekeza ratiba.

Kwa hiyo, kiongozi anapotoka Dar es Salaam au popote pale anakwenda Wilayani akijua hasa kwa uhakika anakwenda vijiji gani. Ratiba haianzii Wilayani inaanza kabla ya kufika Wilayani. Kwa hiyo, narudia tena, wanaopendekeza ratiba na matukio ambayo viongozi wanatakiwa kwenda kuyaona huko katika Wilaya na Mikoa ni Viongozi wa Wilaya na Mikoa. Mara nyingine hata Waheshimiwa Wabunge huwa wanashirikishwa, sehemu nyingine. Ndiyo nimetumia mara nyingine siyo mara zote. Kwa wale wenye bahati ya kushirikishwa huwa wanapendekeza na maeneo ambayo viongozi hawa wanatakiwa kufika na viongozi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, hushiriki katika ziara hizo.

La pili, kurudisha gharama kama mbuzi wamechinjwa na ratiba imekuwa *cancelled*. Yapo mazingira mengi ambayo yanasababisha ratiba kufutwa, wakati mwingine inasababishwa na Wilaya zenyewe. Kwa mfano, muda huu wa masika ratiba imepangwa, ghafla imetokea mvua kubwa kule bondeni,

mzee ninyi wenyewe mnasema kuna utelezi mzee usije safari inafutwa. Wakati mwingine kwa mazingira ya kawaida tu hawa ni Viongozi wa Kitaifa, linatokea jambo muhimu ambalo kiongozi huyu lazima awepe, inafutwa. Kwa hiyo, ufutwaji wa ratiba hizi huwa haufanywi makusudi na Wilaya, Mkoa au Kitaifa. Kwa hiyo, ningomba utaratibu uliopo uendelee.

Na. 121

### **Mradi wa *SELF* - Pemba**

#### **MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kupambana na umaskini ni la Taifa zima; na kwa kuwa katika Kisiwa cha Pemba vipo vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali vikiwemo vile vya wanawake na vijana kwa lengo la kujikwamua kimaisha kutokana na umaskini; na kwa kuwa vikundi hivyo havina nyenzo za kutosha na soko kwa ajili ya bidhaa wanazozalisha:-

Je, ni lini Mradi wa *SELF* utafika Pemba ili kusaidia wanaushirika hao katika miradi yao ya kiuchumi?

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mradi wa *SELF* ambao upo chini ya usimamizi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, ulianzishwa kama mojawapo ya jitihada za Serikali kupambana na umaskini Tanzania Bara na Zanzibar. Upande wa Tanzania Bara, Mradi wa *SELF* hufanya kazi katika Mikoa ya Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Lindi na Mtwara na huko Zanzibar *SELF* hufanyia shughuli zake Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *SELF* unajishughulisha na kutoa mikopo kwa Asasi za kifedha ili hatimaye Asasi hizo ziweze kutoa mikopo midogo midogo kwa wananchi wenye kipato kidogo hususan waliopo vijijini. Asasi hizo ni kama vile Mashirika yasiyo ya Kiserikali (*NGOs*), Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) na Jumuiya za Kijamii (*CBOs*).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania Zanzibar, *SELF* imewezesha kufanyika shughuli zifuatazo:-

- (i) Mpaka sasa katika shughuli za kutoa mikopo Mradi wa *SELF* umetoa mikopo yenye thamani ya jumla ya shilingi 95 milioni iliyotolewa kwa Asasi mbili yaani *PRIDE Tanzania* na *Changamoto Life Preservation Fund*. Kulingana na maombi ya Asasi hizo, mikopo hii ililenga soko la Unguja pekee.
- (ii) Uhamasishaji na Masoko. Mradi umefanya zoezi la uhamasishaji Unguja na Pemba kwa kuzitembelea Asasi za kifedha zilizopo na kusambaza machapisho ya mradi kama vile vipeperushi, mabango, kalenda na jarida la mradi. *SELF* vile vile imeanzisha kipindi cha Redio kijulikanacho kama “Kopa Ujiendeleze” kinachorushwa hewani kila siku ya Jumapili kupitia Redio Tanzania Dar es Salaam na Redio Sauti ya Tanzania Zanzibar kwa lengo la kuutangaza zaidi mradi.
- (iii) Uwezeshaji na mafunzo. Jumla ya Asasi za kifedha zipatazo tatu zimekwishapatiwa mafunzo kwa lengo la kuzijengea uwezo wa watendaji.
- (iv) Upatikanaji wa Mikopo Pemba. Asasi moja kati ya mbili zilizopatiwa fedha kwa ajili ya kutoa mikopo katika Kisiwa cha Unguja, imeonesha nia ya kutoa mikopo katika Kisiwa cha Pemba. Ushauri umetolewa kwa Asasi husika kukamilisha taratibu zinazopaswa

kufuatwa ikiwemo kuwasilisha maombi rasmi ya mkopo. Mara tu ombi hili litakapowasilishwa *SELF*, litashughulikiwa kwa haraka ili wananchi wa Pemba waweze kupata huduma ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mradi wa *SELF* haujijusishi na utoaji mikopo kwa mtu mmoja mmoja, bali kama nilivyoelezea hapo juu, hutoa mikopo kwa Asasi za fedha. Hivyo basi, ili wananchi walioanzisha vikundi vya uzalishaji mali waweze kupata mikopo ni vyema wakashauriwa kujiunga pamoja na kuviandikisha vikundi vyao kuwa asasi za kifedha kama vile *SACCOS* au kuomba mikopo kutoka kwenye asasi za kifedha zilizopo.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa *NGO* ya *Wise* ina programu nzuri ya kutoa mafunzo ya biashara kwa wafanyabiashara wanawake wa Kitanzania na kwa kuwa mafunzo hayo yalifanyika Unguja na Pemba lakini tatizo lililobakia ni mtaji:-

- (i) Je, Serikali itayashauri lini Mabenki yatoe mikopo kwa wingi na isiyo ya riba kubwa kwa wafanyabiashara wadogo wadogo ili kuondoa tatizo hili? (*Makofi*)
- (ii) Kwa kuwa mbali na matatizo ya mtaji kwa wafanyabiashara hawa wadogo wadogo wa Pemba au Tanzania, lakini tatizo zaidi ni lile la soko kama alivyozungumza mwenyewe kwa bidhaa wanazozalisha, jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada za wanaushirika hawa wanawake na vijana, je, Serikali inatoa ahadi gani ya kuwaundia chombo maalum cha kununua bidhaa za wana ushirika hao? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, kwanza, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba, Asasi yoyote ambayo inaanzishwa na wananchi kama alivyosema yeye *NGO*, inaweza kabisa ikifuata taratibu zilizopo kupewa fedha ambazo zitakopeshwa hawa akina mama anaowasema pamoja na vijana. Kwa hiyo, ni vizuri baada ya kupata majibu, awashauri wahusika wawasiliane na ofisi zetu ikiwepo Ofisi ya Makamu wa Rais, pamoja na Mradi huu wa *SELF* ili tuweze kuwaelekeza namna ya kuanzisha Asasi hizo.

Pili, kuhusiana na suala la ukosefu wa soko la bidhaa na kwamba kiundiwe chombo, ningependa kumjibu kwamba, kutokana na uchumi unaoendeshwa kwa soko huria, kinachotakiwa ni kwamba, tuwasaidie wahusika wanaoendesha hiyo miradi na kutengeneza hizo bidhaa wawe wanazitengeneza katika hali ambayo inaweza ikavutia vizuri zaidi kwa wateja kwa maana ya ubora wa bidhaa na vile vile unadhifu wa shughuli zao. Lakini ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kuvishauri vikundi kuboresha bidhaa na vile vile kuwashauri suala zima la masoko.

Na. 122

#### **Jitihada za Kuondoa Umaskini Zanzibar**

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa ya kuondoa umaskini nchini, hasa katika maeneo yaliyoathirika na kwa kuwa Zanzibar yako maeneo yaliyoathirika na yanaendelea kuathirika kwa umaskini:-

- (a) Je, Serikali inatambua kwamba Zanzibar, yako maeneo yanayoathirika kwa umaskini?
- (b) Je, Serikali imetoa misaada kiasi gani kwa waathirika wa umaskini Kisiwani Pemba kwa kipindi cha 2002/2003?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua kuwa huko Zanzibar yako maeneo yanayoathirika kwa umaskini. Kwa kuzingatia hilo, utekelezaji wa Mradi wa *SELF*, ambao uko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, unashirikisha Mikoa yote ya Zanzibar katika kutoa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo, tofauti na Tanzania Bara ambapo mradi huo upo katika mikoa sita tu kati ya 21. Katika kipindi cha 2002/2003, jumla ya shilingi 94,000,000/= zilikopeshwa na watu 1,460 walifaidika na mkopo huo. Waliofaidika ni wanawake 907 na wanaume 553.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha 2002/2003, Kisiwa cha Pemba kilipewa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*). Hilo limefanyika kwa kushirikiana na wananchi wenyewe kama inavyotakiwa katika utaratibu wa kisasa wa kutekeleza mikakati ya kupunguza umaskini. Miradi ya usambazaji wa maji safi, ujenzi wa vituo vya afya, ujenzi wa barabara na ujenzi wa madarasa, ilitokelezwa katika maeneo yafuatayo:-

Matale, Kichokochwe, Ikulini, Weshi, Shidi, Mgagadu, Daya, Mgeloma, Kiuyu Minungwini, Chumbageni, Shunge juu, Pondeani, Shumba vya Mboni, Finya, Kilindi, Mtuhaliwa, Kiuyu Mbuyuni, Kinowe na Limbali. Jumla ya shilingi 472,058,600 zilitolewa kusaidia utekelezaji wa miradi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kumuarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, Zanzibar inao mpango wa kupunguza umaskini uliozinduliwa mwaka 2002 na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, ambao umebainisha maeneo ya kutiliwa mkazo. Mpango huo unatekelezwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ni bora viongozi kwa upande wa Visiwani wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, waunge mkono utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusesitiza tena juu ya umuhimu wa viongozi kuhamasisha wananchi ili washiriki katika jitihada za kujitelea maendeleo yao kuliko daima kutegemea Serikali. Jitihada za Serikali sharti ziungwe mkono na zile za wananchi wenyewe. (*Makofi*)

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa njia moja ya kuondoa umaskini ni kuwapa uhuru wananchi waweze kujiuzia mazao yao wanapopataka. Sasa je, Serikali haioni kwamba, inapingana na sera zake kutowapa nafasi Wanzanzibari kuuza karafuu zao wanakotaka? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA - MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninampongeza kwa kuonyesha moyo wa wazi kabisa kwamba anapenda kuondoa umaskini na anaunga mkono shughuli za Serikali. Kuhusu swali lake la kusema kuwe na uhuru wa kuuza bidhaa huko Zanzibar, katika mgawanyo wa kazi hilo suala linashughulikiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa hiyo, ningependa aelekeze huko ili kupata muafaka wa majibu na pia kama anaweza kumtumia Mwakilishi wake, maana naye pamoja na kuwa ni Mbunge, anaye Mwakilishi kwenye Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja. Kwa kuwa biashara za nje ni mambo ya Muungano, Waziri haoni kuwa hakufahamu Sheria na Katiba ya Nchi, suala la kuuza karafuu nje ni suala la Muungano, kwa sababu biashara za nje ni mambo ya Muungano? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, kitendo cha kuniambia mimi sijui sheria ni sawa na kunitukana kabisa. Mimi nikiwa Mbunge ambaye nilipoingia Bunge nilikwishakuwa tayari mwanasheria niliyebobea. Kwa

hiyo, basi kwa heshima na taadhima, bado nasema kwamba, suala la biashara hususan aliyosema ya karafuu na naipongeza Serikali ya Zanzibar, kwa kupambana na magendo ya karafuu. Kwa hiyo, litarekebisha huko nyumbani. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 123

### Utungaji wa Sheria

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika utaratibu wa kutunga sheria vyombo viwili vya dola yaani Bunge na Serikali hufanya kazi hizo kwa ukaribu sana:-

- (a) Je, katika suala hilo, Mahakama inashirikishwaje?
- (b) Je, kwa kutoshirikisha Mahakama, Serikali haioni kwamba kunalidhalilisha Bunge hasa pale Mahakama inapozitupilia au kuziweka pembeni sheria zilizopitishwa na Bunge kwa sababu Bunge limekiuka vifungu fulani vya Katiba au kwa sababu nyingine yoyote ile?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulijibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaainisha mgawanyo wa madaraka baina ya nguzo tatu za uendeshaji wa nchi ambazo ni Serikali, Bunge na Mahakama. Kama ilivyoainishwa katika Katiba, kazi ya kutunga sheria ni ya Bunge. Mahakama haishirikishwi na wala haitakiwi kushirikishwa katika kazi hiyo ili kulinda mgawanyo huo.
- (b) Kazi ya Mahakama ni kutoa haki kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni mbalimbali za nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, hutafsiri sheria mbalimbali. Pale sheria inapokiuka Katiba, ni kazi ya Mahakama kutamka kuwa sheria hiyo ni batili kwa kiwango kinachopingana na Katiba.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Bunge halidhalilishwi na wala halitakiwi kujiona linadhalilishwa kwa Mahakama kutekeleza jukumu lake hilo ambalo lipo kwa mujibu wa Katiba.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya kisheria ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Bunge ni chombo cha kutunga sheria lakini huwa linashirikiana na baadhi ya *NGOs* na watu mbalimbali, hii ni pamoja na wanasheria; na kwa kuwa Mahakama pia inahusiana na wanasheria:-

- (i) Je, Waziri haoni sasa ni wakati muafaka kushauriana na Mahakama?
- (ii) Kwa kuwa imeshajitokeza mfano wa suala la kutoa *deposit* ya shilingi milioni 5 wakati wa kufungua kesi na Bunge likadhalilika, haoni sasa ni wakati muafaka hata ikiwezekana Katiba hiyo, itazame vizuri ili Mahakama, Bunge na Serikali, wawe pamoja katika suala zima la kutunga sheria na kuwatendea haki wananchi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme swali lenyewe lilikuwa la kisheria, anayeulizwa ni Waziri wa Sheria, kwa hiyo jibu lazima liwe la kisheria. *(Kicheko/Makofi)*

Suala la kwamba *NGOs* na jumuiya mbalimbali kushirikishwa katika utungaji wa sheria hiyo ni kupata maoni toka *NGOs* mbalimbali na kwa wananchi ili kuweza kuboresha Miswada ile kabla haijapitishwa kuwa sheria. Sasa Mahakama ni nguzo hawa wengine siyo nguzo. Nguzo ziko tatu na Bunge lenye jukumu la kutunga sheria. Hivyo hivyo kwa ajili ya kuhifadhi huo mgawanyo (*Separation of Powers*), suala la hii la shilingi milioni tano inawezekana kabisa kwamba Bunge likakosea na kunakuwepo chombo kingine ambacho kitarekebisha makosa yale. Serikali inaweza ikakosea katika kuleta Muswada, Bunge linaweza likakosea, Mahakama iko pale kufanya tafsiri. Kwa hiyo, ni lazima kwa kweli tuheshimu huo mgawanyo. Hata nyumbani tuna *separation of powers*, si ndiyo? Mama ana kazi, mzee ana kazi, watoto wana kazi na hilo ni katika muundo wa Serikali. (*Kicheko/Makofi*)

Na. 124

### **Adhabu Kali**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi tunasikia kwenye vyombo vya habari kauli ya Hakimu akisema anatoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwa wengine wanaopanga kutenda kosa kama la mtu huyo aliyetiwa hatiani na kwa kuwa adhabu kwa makosa mbalimbali zimeainishwa katika taratibu za Mahakama:-

- (a) Je, kauli kama hiyo ina maana kwamba Hakimu anao uhuru wa kupanga adhabu nzito/kali ambayo yeye anafikiri itakuwa *deterrent*?
- (b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ni busara faini za pesa kufanyiwa mapitio (*review*) ya mara kwa mara ili kuondokana na baadhi ya hukumu kuwa ni kichekesho kwa jinsi kiwango cha pesa za adhabu zinavyokuwa kidogo mno ikilinganishwa na uzito wa kosa lenyewe?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mahakama kama chombo cha dola, kinafanya kazi kwa mujibu wa sheria mbalimbali ambazo zimepitishwa na Bunge lako Tukufu. Makosa mbalimbali ya jinai yamewekewa adhabu zake kisheria na sheria hizo hazitoi mamlaka kwa Hakimu kutoa adhabu nje ya viwango vile vilivyowekwa kisheria. Ndani ya viwango vilivyowekwa, Hakimu anao uwezo wa kutoa adhabu kulingana na uzito wa kosa ili mradi havuki kiwango cha juu kilichowekwa. Hivyo, Hakimu anapotamka kwamba anatoa adhabu kali ni katika kuzingatia uzito wa kosa, lakini katika mipaka ya viwango vya adhabu vilivyowekwa.

(b) Ni utaratibu wa Serikali kupitia upya viwango mbalimbali vya ada pamoja na adhabu ya faini pale inapoonekana viwango hivi ni vidogo na kupitwa na wakati. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, wajibu wa kufanya mapitio na kutoa mapendekezo ya mabadiliko ya adhabu ya faini ni wa Asasi mbalimbali za Serikali.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri. Nina swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Daktari anapompa kitanda mgonjwa wake huwa anapita kila wakati kukagua hali yake mpaka hapo atakaporidhika anampa ruhusa kwenda nyumbani; na kwa kuwa mfano huo unaelekeana sana na kazi ya Hakimu; je, Waziri haoni kwamba ingekuwa vizuri kuwe na mipango kwa Mahakimu kwenda kuwaona wateja wao badala ya kuwasweka ndani na kuwasahau kabisa? Kama anakubaliana na mapungufu hayo, isingekuwa wakati muafaka Magereza ikawa chini ya Idara ya Mahakama moja kwa moja? (*Kicheko/Makofi*)

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa upande wa Madaktari kuwatembelea wagonjwa wao, basi utaratibu huo pia upo kwa upande wa Mahakimu

kuwatembelea mahabusu pamoja na wafungwa. Lakini kwa upande wa Madaktari inabidi wafanye zoezi hilo kila siku na kila wakati. Wagonjwa wakiwa taabani inabidi wapimwe kila wakati na wauguzi, lakini kwa upande wa wafungwa na mahabusu, inakuwa sio lazima kwa kweli kuwatembelea kila wakati.

Kwa hiyo, Mahakimu wote katika ngazi zote tangu Majaji mpaka Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, ikiwa ni pamoja na sisi Wabunge, tuna majukumu ya kuwatembelea wafungwa na mahabusu kujua hali zao zikoje.

Kuhusu suala la Mahakama kushughulikia ama kusimamia Magereza, hiyo ni kazi ya Serikali. Sana sana ambalo unaweza kufanya na nchi nyingine zinafanya ni kwamba, Magereza yanakuwa yako chini ya Wizara ya Sheria. Lakini kusema kwamba Magereza yawe chini ya Idara ya Mahakama, sio utaratibu wa mgawanyo wa madaraka.

125

### **Uwianishaji wa Vyanzo vya Mapato**

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali zetu za Mitaa zimetakiwa kuwianisha vyanzo vyake vya Mapato na zimefanya hivyo. Je, ni lini basi Serikali Kuu nayo itarekebisha vyanzo vyake vya mapato kwa kuziachia Halmashauri baadhi ya vyanzo au asilimia fulani ya mapato yake yanayohusiana na Halmashauri kama vile mrahaba wa madini na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa mara kadhaa imerekebisha vyanzo vyake vya mapato kwa kuziachia Halmashauri baadhi ya vyanzo. Aidha, kwa baadhi ya vyanzo, kiasi fulani cha mapato yanayokusanywa kinaachiwa Halmashauri. Kwa mfano, katika Sheria ya Fedha Na.11 ya mwaka 1999, marekebisho mengi yalifanywa ili kujibu hoja hii. Marekebisho hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

- (a) Vyanzo vya mapato na ada vilivyohamishiwa kwenye Halmashauri ni pamoja na:-
- Mapato yote yanayotokana na usajili wa teksi na mabasi ya mijini;
  - Mapato yote yanayotokana na ada za ukaguzi wa vyama na matumizi ya machinjio; na
  - Mapato yote yanayotokana na ada za leseni za biashara ambazo Halmashauri ndio Mamlaka ya kutoa leseni. Leseni hizo ni pamoja na udalali, uwakala wa usafiri, uuzaji na ununuzi wa magari, uwakala wa Bima, migahawa na hoteli za kawaida, nyumba za kulala wageni na kadhalika.
- (b) Kodi na ada ambazo sehemu ya mapato yake hugawiwa kwa Halmashauri ni:-
- Asilimia 20 ya mapato yanayotokana na kodi ya ardhi inayokusanywa na Serikali Kuu, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 (*The Land Act, 1999*);
  - Asilimia 20 ya mapato yanayotokana na ada za uwindaji ambazo zinakusanywa kwa mujibu wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 1974 (*The Wildlife Conservation Act, 1974*); na



- Asilimia kumi ya mapato yanayotokana na usajili wa hospitali binafsi ambayo yanakusanywa na Serikali Kuu chini ya Sheria ya *The Private Hospitals (Regulations) Act, 1977*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kahumbi ameridhika, tunaendelea. Swali linalofuata Mheshimiwa Hamad Rashid.

Na.126

### **Uanachama wa Tanzania Kwenye Asasi za Fedha Duniani**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa Asasi nyingi za kifedha duniani:-

- (a) Je, ni Asasi ngapi ambazo Tanzania ina hisa?
- (b) Je, ni Asasi ngapi ambazo Tanzania ni mwanachama?
- (c) Je, Serikali inafaidika vipi na *PTA Bank, Africa Export Bank*?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina hisa na pia ni mwanachama katika sehemu saba za kifedha duniani, nazo ni kama ifuatavyo:-

- (i) *African Export - Import Bank* yaani, *AFREXIM Bank*;
- (ii) *East African Development Bank (EADB)*;
- (iii) *PTA Bank*;
- (iv) *African Development Bank (ADB)*;
- (v) Benki ya Dunia (*World Bank Group*);
- (vi) *International Monetary Fund (IMF)*; na
- (vii) *African Trade Insurance Agency (ATI)*.

- (c) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania kama mwanachama wa *PTA Bank* na *AFREXIM Bank*, kwa ujumla inafaidika kwa njia mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Benki hizi zina malengo ya kuimarisha nguvu za kiuchumi miongoni mwa nchi wanachama. Kwa mfano, *AFREXIM Bank* inasaidia katika kutoa mikopo ya aina mbalimbali kwa wafanyabiashara wanaoingiza au kupeleka bidhaa nje miongoni mwa nchi wanachama wa *AFREXIM*. Kwa upande wa Tanzania hadi mwaka 2003 *AFREXIM Bank* ilitoa jumla ya mikopo yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 65.0 kwa Kampuni ya *VODACOM Tanzania Limited*. Tanzania kupitia Benki Kuu ya Tanzania, ina hisa zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1.2 katika Benki hii na hadi sasa tumepata gawio la faida la Dola za Kimarekani 153,484.55; na

(ii) *PTA Bank* ilianzishwa kuhamasisha biashara na kuwakopesha wafanyabiashara miongoni mwa nchi wanachama. Katika Benki hii Tanzania ina hisa 2,606 zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 26.07 ambazo ni sawa na asilimia 9.64 ya hisa zote za *PTA Bank*. Hivyo, Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo zimefaidika sana na mikopo kutoka *PTA Bank*. Katika kipindi kati ya mwaka 1999 na 2003 Benki hii ilitoa mikopo yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 50.3 kwa Makampuni na wafanyabiashara wa Tanzania. Aidha, Januari, 2004 *PTA Bank* zimeandikisha dhamana (*Corporate Bonds*) zenye thamani ya shilingi bilioni 15.0 katika Soko la Hisa la Dar es Salaam na fedha zote zitakopeshwa kwa Makampuni ya kitanania.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Asasi hizi zinalenga kutoa mikopo ya miradi na ya biashara katika nchi zilizo na uanachama kwa kulenga Sekta Binafsi na Mashirika ya Umma.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa ruksa yako naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa tatizo moja kubwa la Tanzania na Watanzania kwa jumla ni kupata taarifa kamilifu juu ya vyombo vya fedha ambavyo vinatoa mikopo au vinatoa *services* kwa Watanzania na ni wachache tu wanaojua huduma hizo. Je, Serikali itakuwa tayari kuwafanyia Semina Wabunge juu ya Asasi zote za fedha na taratibu zinazotumika za kupata mikopo hiyo?

Pili, kwa kuwa bado viwango vya riba katika Benki zetu za hapa nchini ni kubwa, je, Serikali itakuwa tayari kuelekeza Benki hizo sasa kuangalia uwezekano wa kutoa riba ndogo hasa kwa wakulima Vijijini na kupunguza masharti ambayo wakulima wataweza kulipa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali kutoa Semina ili kutoa taarifa juu ya Mabenki haya. Mabenki yenyewe yameshafanya hivyo, kwa mfano mwaka juzi *AFREXIM Bank*, ambayo Makao Makuu yake yako Cairo, ilikuja kutoa semina maalum kwa kupitia *CCLA* na *Bank of Tanzania*, kuhakikisha kwamba, wafanyabiashara wengi wanajua fursa hii. Lakini hata hivyo, Serikali itachukua dhamana hiyo ya kufanya Semina kuwaelekeza Wabunge juu ya Asasi za Fedha. (*Makofi*)

Kuhusu riba na masharti, Serikali kwa kutumia Taasisi mbalimbali za Fedha kama hivi leo asubuhi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, alizungumzia juu ya *SELF* ambazo zinatoa riba ndogo na *TASAF* ni mojawapo ya mikakati ambayo inahakikisha wale wafanyabiashara wadogo wadogo na wa vijijini hawatozwi riba kubwa katika mikopo wanayochukua. Lakini vile vile kwa sheria ambayo inaletwa Bungeni ya *Land Act*, itasaidia vile vile kurejesha chini riba ya mkopaji katika maeneo mbalimbali.

Lakini vile vile Waheshimiwa Wabunge mfahamu kwamba, riba vile vile inategemea na aina ya mkopo uliokopa. Inaweza kuwa *average* iko katika 14, lakini unaweza kupata riba ya *ten percent* kulingana na hali ya biashara yenyewe uliyoifanya na namna ya pato litakavyokuja, Benki inaangalia hayo yote.

Kwa hiyo, sio riba yote inakuwa Benki ni *14 to 15 percent*, hapana. Inategemea na aina ya biashara yenyewe na wewe mfanyabiashara utakavyozitumia zile fedha ili uweze kuitumia ile riba kwa yale uliyoyakusudia kwa mkopo ule uliochukua.

Na.127

### **Ujenzi wa Barabara ya Lami Toka Mwanza hadi Mtwara**

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO (k.n.y. MHE. DR. WILLIM F. SHIJA)** aliuliza:-

Kwa kuwa mpango wa kujenga barabara ya lami toka Mwanza hadi Mtwara hauwezi kukamilika bila ya kujenga barabara ya lami toka Bukoba - Biharamulo - Geita - Sengerema na Usagara (Misungwi):-

(a) Je, Serikali imefikia wapi katika mpango huo?

(b) Je, Serikali inasema nini juu ya taarifa kwamba wanaomiliki migodi ya dhahabu ya Kahama na Geita wameomba kusaidia ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. William F. Shija, Mbunge wa Sengerema, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara inayunganisha Mikoa ya Kagera, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara, umeainishwa katika

mpango mzima wa ujenzi wa barabara kuu kwa kiwango cha lami hapa nchini zenye urefu wa kilometa 10,300. Mpango huu pia umeainishwa katika mikakati tuliyojiwekea ya kuboresha usafiri, uchumi na hatimaye kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2025.

Aidha, utekelezaji wa mpango huu umegawanywa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha za Wafadhili pamoja na za ndani. Ujenzi wa barabara inayounganisha Mikoa ya Kagera na Mtwara kupitia Mwanza na Dar es Salaam, unafadhiliwa na Benki ya Dunia (*IDA*), Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta kwa Wingi Duniani (*OPEC*), *DANIDA*, Kuwait, pamoja na Serikali ya Tanzania (*GOT*).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya Bukoba - Biharamulo - Geita - Sengerema - Usagara, utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mutukula - Bukoba - Muhutwe (kilometa 112): Ujenzi unaendelea na utakamilikia Februari, 2004. (*Makofi*)
- (ii) Muhutwe - Kagoma (kilometa 24): Ujenzi umekamilika Oktoba, 2003. (*Makofi*)
- (iii) Kagoma - Lusahunga (kilometa 154): Maandalizi ya kuitisha zabuni za ujenzi wa barabara yanaendelea. Tunatarajia ujenzi kuanza katikati ya mwaka 2004 na kukamilika mwaka 2007. (*Makofi*)
- (iv) Kyamiorwa/Biharamulo - Usagara (kilometa 388): Mkataba wa Usanifu wa Awali ulisainiwa tarehe 25 Juni, 2003 kwa lengo la kuanza ujenzi Juni, 2004.

(b) Mheshimiwa Spika, kumekuwapo na mawasiliano kati ya Makampuni yanayomiliki migodi ya dhahabu ya Kahama na Geita kwa lengo la Makampuni hayo kusaidia katika kuboresha barabara ya Usagara hadi Geita mara Serikali itakapokuwa tayari katika maandalizi. Kama nilivyokwishaeleza katika jibu la sehemu (a), Serikali imeanza kuifanyia upembuzi yakinifu sehemu hii ya barabara ambao utafuatiwa na usanifu pamoja na ujenzi. Ni dhahiri kuwa uwezo wa Serikali utahitaji msaada kama huo wakati ujenzi kwa kiwango cha lami utakapokaribia. Hadi sasa Wizara ya Ujenzi haina taarifa yoyote iliyoletwa na wenye migodi ya Kahama na Geita kutaka kuchangia ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, tutashukuru kama Mbunge atasaidia kuwashawishi wawekezaji hawa katika hili. (*Makofi*)

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika barabara hii ya Bukoba - Biharamulo - Geita, Sengerema hadi Usagara kuna kivuko muhimu cha Visisi - Kigongo ambacho feri yake sasa hivi ni mbovu, imechakaa na imechoka, je, Serikali itakuwa tayari sasa katika ujenzi wa barabara hii kutenga hela kwa ajili ya kununua kivuko kipya na cha kisasa katika Kivuko cha Usinsi - Kigongo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na ujenzi wa barabara hii, Wizara ya Ujenzi sasa hivi ina mikakati maalum juu ya vivuko nchini, vivuko karibu vya nchi nzima tumeagiza vifanyiwe utafiti, iletwe taarifa kamili ili tuviwekee mikakati wa kununua vipya pale panapostahili kununuliwa vipya ama tutengeneze pale panapostahili ukarabati au tuombe madaraja pale panapostahili madaraja mbadala ya vivuko. (*Makofi*)

**MHE. FAUSTINE KABUZI RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya kutoka Usagara hadi Geita - Biharamulo imekuwa ikiharibiwa sana na magari ya migodi ya Geita na Kahama na pesa nyingi za Mkoa wa Mwanza hutumika kwa ajili ya kutengeneza barabara hiyo; Serikali inaona aibu gani kuwashinikiza hawa wachimba mgodi ambao wanachukua fedha nyingi kuanza kukarabati barabara za Geita angalau zifanane na Wilaya nyingine? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali haioni aibu na wala haitaona aibu kusindikiza yeyote anayeharibu barabara nchini. Lakini uko pale pale kwamba unaporuhusu utekelezaji wa miradi mikubwa, basi ujue mitambo na malori makubwa yanatumia nchi hiyo. Tunazungumza na wenzetu

wanaochimba migodi hii tuone ni jinsi gani ya kutengeneza barabara zinazoweza kukidhi matumizi yao kwa kule wanakoitumia. Sasa hivi tumewaita waje tuzungumze nao ili wasaidie barabara hii maalum, wazitengeneze wenyewe kwa kutumia mitambo yao tu ili tusiwe na uharibifu wa kutumia pesa zetu kila wakati. (*Makofi*)

Na.128

### **Sehemu ya Barabara Inayoanzia *Number One***

**MHE. WILLIAM J. KUSILA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara inayoanzia sehemu inayoitwa *Number One* katika barabara Kuu ya Dodoma hadi Iringa kupitia Vijiji vya Bihawana, Mbabala, Nkhome, Mpalanga, Chidilo, Zejele, Nondwa, Sanza hadi Manyoni iko chini ya Mamlaka tatu za Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma na *TANROADS* Mkoa wa Singida; na kwa kuwa Kamati ya Ushauri ya Mkoa ilishapendekeza kuwa, sehemu ya barabara hiyo iliyo katika Mkoa wa Dodoma kati ya *Number One* na Nondwa ipandishwe hadhi ili iwe chini ya Mkoa:-

- (a) Je, Serikali inayo taarifa juu ya uamuzi huo na kama inayo taarifa imeamua nini kuhusu pendekezo hilo la Mkoa wa Dodoma?
- (b) Kwa kuwa sehemu ya barabara hiyo kati ya *Number One* na Sanza ni mbaya sana, je, Serikali itapokea ombi langu la kutoa fungu maalum la fedha kwa ajili ya matengenezo ya dharura katika sehemu hiyo?
- (c) Kwa kuwa baadhi ya Vijiji nilivyovitaja kuna tatizo kubwa la wizi wa mifugo kwa wafugaji wa maeneo hayo na kwa kuwa taarifa za wizi na matatizo mengine zinachelewa kufikishwa Polisi, Mjini Dodoma na Polisi pia huchelewa kufika kwenye eneo la tukio kutokana na ubovu wa barabara hiyo, je, isingekuwa wakati muafaka sasa Serikali ikakubaliana nami katika vipengele (a) na (b) vya swali hili ili kuwaondolea kero wananchi wa maeneo hayo ikiwa ni moja ya Sera za CCM?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Jonathan Kusila, Mbunge wa Bahi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Wakala wa Barabara (*TANROADS*), Mkoa wa Dodoma, imepokea mapendekezo ya Bodi ya Barabara ya Mkoa yaliyohusu maombi ya kupandishwa daraja barabara zinazohudumiwa na Halmashauri za Wilaya zenye jumla ya urefu wa kilometa 834 ili kuwa barabara za Mkoa. Mojawapo ya barabara hizo ni hii anayoiulizia Mheshimiwa Mbunge, ambayo inaanzia Mkonze (*Number One*) - Bihawana - Mbabala - Nkhome - Mapalanga - Chidilo - Zejele hadi Nondwa, yenye urefu wa kilometa 55.

Napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara yangu karibu itakamilisha mapitio ya Sheria ya Barabara (*Highway Ordinance*), ambayo ndani yake barabara zote nchini zitawekwa kwenye makundi au madaraja yanayostahili kulingana na vigezo vilivyokubalika. Katika zoezi hilo, baadhi ya barabara za Wilaya zinazokidhi vigezo vya kupandishwa daraja zitapandishwa na baadhi ya barabara za Mikoa zitashushwa hadhi na kuwa za Wilaya na baadhi ya barabara za Wilaya zitashushwa hadhi kuwa za Vijiji.

Kwa wakati huu, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, kupitia Bodi ya Barabara ya Mkoa, awaarifu wadau wote kuwa na subira juu ya suala hili.

- (b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sehemu ya barabara kati ya *Number One* na Sanza kwa sasa inasimamiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma Vijijini, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge, kulipeleka ombi la kutengewa fedha za matengenezo ya dharura kwa Wizara husika yaani TAMISEMI. Ikumbukwe pia kwa sasa Halmashauri zote za Wilaya nchini, zinapata migao yao ya fedha toka Mfuko wa Barabara. Hivyo, Mheshimiwa Mbunge, anayo nafasi ya kuishawishi Halmashauri ya Wilaya yake kuipa kipaumbele matengenezo ya barabara hii kulingana na umuhimu wake.
- (c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana kimsingi na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuwa, endapo barabara hii itafanyiwa matengenezo yatakayoivezesha kupitika katika majira yote ya mwaka, kero nyingi zinazosababishwa na ubovu wa barabara katika maeneo hayo zitaondoka. Hata hivyo, kikwazo kikubwa katika kutimiza azma hiyo kwa barabara hii na nyingine nyingi hapa nchini kwetu ni ufinyu wa Bajeti ya Serikali.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake. Tatizo nililolizungumzia ni kwamba, barabara hii ni moja inaunganisha Miji ya Dodoma na Manyoni, lakini iko katika hadhi mbili. Kwa upande wa Mkoa wa Singida iko chini ya *TANROADS*, kwa upande wa Mkoa wa Dodoma iko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma na Halmashauri ya Manispaa. Sasa hii ni *abnormally*. Sasa pamoja na maelezo mazuri ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni kuna haja ya kurekebisha *abnormally* hii ili barabara hii ambayo ni moja iwe na hadhi moja ya kutoka Dodoma hadi Manyoni? Kwa vile iko chini ya Mkoa wa upande ule, basi iwe chini ya Mkoa vile vile kwa upande wa Mkoa wa Dodoma. Vinginevyo inafanya barabara hii inakuwa katika vipande viwili. Upande mmoja ni nzuri na upande mwingine haipitiki kabisa. Haoni kuna haja ya kurekebisha *abnormally* hiyo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, dosari iliyopo katika barabara hii kati ya Dodoma na Singida tunaifahamu, lakini kwa kuwa tumeikuta hapo hatuwezi kufanya maamuzi kwa barabara hii tu. Zipo nyingi za namna hiyo. Ndio maana nimesema wakati tutakapoleta Sheria ya Kusahihisha Barabara na ya Kupandisha Daraja Barabara Tofauti, dosari kama hizi zitasahihishwa. (*Makofi*)

Na.129

### **Sheria Kuzuia Vitendo vya Ukahaba**

**MHE. ALHAJI AHAMADI HASSAN MPEME** aliuliza:-

Kwa kuwa Ukimwi ni tishio la maisha ya binadamu; na kwa kuwa hali ya maambukizi inazidi kuongezeka kila siku:-

- (a) Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Kupinga Vitendo vya Ukahaba na mambo yote yanayofanana na hayo ili kupunguza tatizo hilo ambalo kwa namna moja linachangia maambukizi makubwa ya Ukimwi ndani ya jamii?
- (b) Je, Kitendo cha vijana wa kike kuonekana hadharani kwenye *TV* wakiwa kwenye michezo au sherehe huku wakinengua wakiwa nusu uchi hakiwezi kuchangia kueneza Ukimwi na kama hivyo ndivyo, je, Serikali inachukua hatua gani kwa vitendo kama hivyo ambavyo licha ya kuwa vinaweza kuamsha tamaa ya matendo ya ngono na hatimaye maambukizi ya Ukimwi, lakini pia vinaidhalilisha jamii ya Kitanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Hassan Mpeme, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, ni kweli vitendo vya ukahaba vinaweza kuongeza kasi ya maambukizi ya Ukimwi. Hatua madhubuti zimekuwa zikichukuliwa na Serikali ili kupunguza maambuziki ya Ukimwi. Kwa mfano, kutunga na kupitisha Sera ya Kudhibiti Ukimwi ya mwaka 2002, Kuzindua Mkakati wa Kimataifa wa Kudhibiti Ukimwi, kuboresha Mitaala ya Shule kwa kuingiza masuala ya kuzuia maambuziki ya Ukimwi, Kuundwa kwa Tume ya Kudhibiti Ukimwi, 2001 na kuanzishwa kwa Programu ya Kudhibiti Ukimwi chini ya Wizara ya Afya.

Vile vile Serikali imezindua Mkakati wa Jamii wa Kujikinga na Maambukizi ya Ukimwi, ambao unasisitiza afya ya uzazi kwa wanawake na Vituo vya Afya kwa watoto. Aidha, Sheria ya Uzururaji pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (*Penal Code Cap. 16*), pamoja na mambo mengine, zinashughulikia watu wanaozurura na kukataza uendeshaji wa maisha kwa kutegemea kufanya shughuli za ukahaba ili kujipatia fedha.

Serikali inaamini kwamba, hatua hizo zinatoshesheleza. Hata kama itaonekana kuna haja ya kuwa na Muswada, bado jamii ina wajibu wa kukabiliana na vitendo vya ukahaba na vinginevyo vinavyofanana na hivyo ambavyo vinaidhalilisha jamii, kwani inawezekana kuwa Sheria nzuri, lakini kama jamii haiko tayari kubadilisha tabia na mienendo tatizo halitakwisha.

- (b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kitendo cha vijana wa kike na hata wa kiume kuonekana hadharani kwenye televisheni, michezo au kwenye sherehe wananengua wakiwa nusu uchi, kinaweza kuwa ni mojawapo ya kichocheo cha kueneza Ukimwi kwani vinaweza kuamsha hisia ya kufanya mapenzi kiholela. Serikali kupitia Sheria ya Utangazaji ya mwaka 1993, inatamka wazi kuwa, Vyombo vya Habari vinaweza kufungiwa endapo vitaonesha picha zinazodhalilisha maadili ya kitanzania. (*Makofi*)

Hata hivyo, kuwepo kwa sheria hakutaweza kuondoa kabisa tatizo la udhalilishaji endapo hapatakuwepo na mabadiliko katika fikra na mtizamo wa jamii kuhusiana na masuala ya mapenzi. Aidha, asilimia kubwa ya vitendo vinavyoamsha hisia za mapenzi hutokana na mambo mengine zaidi ya unenguaji unaoonekana katika televisheni na michezo. Ukimwi ni suala linalohitaji ushirikiano wa jamii nzima kwa kuelewa athari zake na kuacha vitendo vyote vinavyoweza kueneza maambukizi ya ugonjwa huo. Serikali inaamini kwamba, jambo muhimu zaidi ni kubadilika kwa jamii nzima kifikra na kimatendo. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuliza swali moja tu la nyongeza.

**SPIKA:** Hebu sogeza *microphone* karibu na pale unapozungumzia.

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Kwa kuwa tatizo kubwa la akina mama wengi kuendelea na mambo ya ukahaba ni maisha duni na kwa kuwa fungu linalotengwa kwa ajili ya kuondoa umaskini kwa wanawake kwa ajili ya kuwapa mikopo halitoshi. Je, sasa Serikali haioni kama ni vizuri kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuwawezesha wanawake hao kupata mikopo ili waondokane na umaskini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kutoa au kusema kwamba, umaskini hauwezi kuondolewa na mikopo tu, kuna njia nyingi. Kwa hiyo, isiwe kisingizio, hilo la kwanza. La pili, ni kweli Serikali tumeanzisha mikopo kwa ajili ya wanawake. Mfuko huo unaitwa *WDF*. Fedha kweli hazitoshi, lakini pia kuna agizo kwamba, kila Halmashauri itenge asilimia 10 ya mapato kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na Vijana.

Mheshimiwa Spika, tatizo ni marejesho. Hadi leo kati ya Halmashauri zilizopo hapa nchini ni Halmashauri 51 tu zimefanya marejesho ya kutosha. Kwa hiyo, naomba marejesho yawepo kwa sababu Mfuko huu ni wa mzunguko. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa hiki ni kikao cha Bajeti Ndogo, muda wa maswali wa saa moja umekwisha. Kwa hiyo, maswali yamemalizika, tunaendelea na mambo mengine.

Kwanza ni matangazo ya vikao vya Kamati vilivyopangwa kwa siku ya leo. Kamati nne zimepangiwa vikao na Wenyeviti wake. Ya kwanza, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Makamu Mwenyekiti wake, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo, wakutane leo Jumatatu, tarehe 16 Februari, 2004 saa 9.00 mchana kwenye Chumba Na. 219. Kamati ya pili, ni Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Malecela, ameomba Wajumbe wakutane leo tarehe 16 Februari, 2004 saa 5.00 asubuhi katika Chumba Na. 227 ghorofa ya pili. Kamati ya tatu, ni Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mgana Msindai, anaomba kikao kifanyike leo tarehe 16 Februari, 2004 saa 7.00 mchana Chumba Na. 133 ghorofa ya kwanza. Kamati ya nne, ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sophia Simba, anaomba Kamati hiyo ikutane saa 5.00 asubuhi Chumba Na. 428 ghorofa ya nne.

Tangazo la vikao vya Kamati limekwisha. Sasa kuhusu shughuli zilizoko kwenye *Order Paper* ya leo, waliokwisha kujiandikisha hadi sasa wanaomba kuchangia Bajeti ya Nyongeza wamefikia 27. Nadhani wanatosha kwa uwiano wa muda uliopo na wachangiaji, nadhani sasa orodha hiyo inafungwa.

Lakini tuna utaratibu wa kuchangia kwa maandishi. Kwa hiyo, bado kuna nafasi kwa yeyote anayeweza kuchangia. Waliojiandikisha kuchangia Hotuba ya Rais hadi sasa ni 17. Nadhani inatuwezesha sasa kuweza kupanga muda ili hoja hizi ziweze kujadiliwa vizuri. Lakini bado kuna nafasi ya kuchangia kwa maandishi kama nilivyosema.

Mwisho wa matangazo tunaendelea na *Order Paper*.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### **Muswada wa Sheria ya Nyongeza ya Matumizi ya Fedha wa Mwaka wa Fedha 2003/2004 (*The Supplementary Appropriation for Financial Year 2003/2004 Bill, 2004*)**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Muswada wa Sheria ya Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya shilingi milioni 87,250 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya ziada ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kwa niaba ya Serikali kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri thabiti.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada ulioko mbele yetu ni kuomba makadirio ya nyongeza ya matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 ili kuiwezesha Serikali kugharamia mahitaji ya dharura yaliyo nje ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, lakini ambayo ni lazima Serikali iyatafutie fedha kwa manufaa ya Taifa na ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Januari 2004, niliwasilisha mbele ya Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2003/2004 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2003 na mwelekeo wake hadi Juni, 2004. Katika taarifa hiyo, nilieleza kuwa, mwenendo wa uchumi mpana yaani (*Macro-economic Performance*) katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo ya mwaka huu wa fedha umekuwa wa kuridhisha, licha ya matatizo yaliyojitokeza kutokana na ukame na kupanda kwa bei ya mafuta.

Mwenendo wa Bajeti kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2003 ulikuwa wa kuridhisha pia. Mapato ya ndani katika kipindi hicho yalikuwa shilingi 713,511 milioni, sawa na asilimia mbili zaidi ya lengo la shilingi 699,354 milioni. Awali tulikuwa na wasiwasi kwamba, mapato ya ndani yangepungua na mwenendo wa Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka ungekuwa chini ya lengo kutokana na hali ya ukame. Hata hivyo, tumepata matokeo mazuri kutokana na baadhi ya hatua za mapato zilizotangazwa kwenye

Bajeti ya mwaka huu wa fedha 2003/2004 na hivyo kuboresha hali ya ukusanyaji mapato. Mafanikio haya yametusaia sana katika kufidia upungufu ambao ungejitokeza kutokana na hali hiyo ya ukame.

Mheshimiwa Spika, pamejitokeza hali ambayo haikutarajiwa wakati wa kuandaa Bajeti ya sasa ambayo imesababisha matumizi yasiyotegemewa na hivyo kuilazimu Serikali kuyaomba kibali kipya kwa vyanzo na matumizi yenyewe. Kwa ujumla zinahitajika shilingi 176,784 milioni za nyongeza hadi Juni, 2004 ili kugharamia shughuli mbalimbali za Serikali kama ifuatavyo:-

- (a) Shilingi 87,250 milioni kuziba mapengo katika Wizara tatu za Kilimo na Chakula, Nishati na Madini na Mawasiliano na Uchukuzi. Hizi imebidi zitokane na vyanzo vipya.
- (b) Shilingi 89,534 milioni kwa mahitaji mengine kadhaa ya Serikali kama nitakavyofafanua baadaye. Hizi zimetokana na uhamisho (*reallocation*) wa ndani kwa ndani kutokana na akiba (*savings*) ya Serikali. Uhamisho huo ni pamoja na shilingi 36,030 milioni kutoka kila Wizara kwa njia ya kukata matumizi kutokana na Kasma za ununuzi wa magari, safari na mikutano ya aina mbalimbali. Kiasi hiki cha fedha kutokana na uhamisho, zitapatikana kwa njia ya Waziri wa Fedha kutumia madaraka aliyonayo kisheria, lakini zitatolewa taarifa Bungeni kama ilivyo desturi, baada ya zoezi la uhamisho huo kukamilika.

Mheshimiwa Spika, uhamisho huo wa shilingi 89,534 milioni ni kama ifuatavyo:-

- (a) Gharama za ongezeko la wanafunzi na walimu wapya wa Sekondari shilingi 2,424 milioni. Mwaka 2003, jumla ya watahiniwa 490,018 walifanya Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba na kati yao, walifaulu 196,296 sawa na asilimia 40 ya watahiniwa kulinganisha na asilimia 27 mwaka 2002. (*Makofi*)

Hili ni ongezeko la wanafunzi waliofaulu 63,000 sawa na asilimia 47.4. Haya ni matokeo ya utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Elimu ya Msingi. (*Makofi*)

Uwezo wa Sekondari za Serikali wa kusajili Kidato cha Kwanza ni wanafunzi 52,853. Hii ina maana kwamba, watoto 143,443 waliofaulu mtihani mwaka 2003 wangeachwa bila kuingia Kidato cha Kwanza mwaka 2004. Ili kuepukana na kero hii, Wizara ya Elimu na Utamaduni, imeshateua wanafunzi 75,872 sawa na asilimia 38.7 ya waliofaulu kuingia Kidato cha Kwanza na inatarajiwa kwamba, nafasi nyingine 18,130 zaidi zitaongezwa katika uteuzi wa pili ili kufikia jumla ya wanafunzi 94,002 sawa na asilimia 47.9 ya watoto waliofaulu darasa la saba. (*Makofi*)

Kwa taarifa Waheshimiwa Wabunge, wapo wanafunzi wengine 52,971 waliofaulu ambao inatarajiwa kwamba, watajiunga na Shule zisizo za Serikali na hivyo kufanya jumla ya watakoingia Kidato cha Kwanza mwaka huu kuwa 146,973 yaani asilimia 75 ya watahiniwa waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2003. (*Makofi*)

Matokeo haya ni kielelezo cha mafanikio ya Sera na Mkakati wa Serikali kuhusu Elimu ya Msingi, hivyo ni lazima kuchukua hatua za kuyakabili kikamilifu. Aidha, ili kuhimili pia ongezeko hilo la wanafunzi waliofaulu, itabidi Serikali iajiri walimu wapya 1,715 na kuwafunza haraka iwezekanavyo kati ya sasa na Juni. Zoezi hili linahitaji fedha kiasi cha shilingi 2,424 milioni za dharura.

(b) Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Serikali (shilingi 12.099 bilioni). Wakati mishahara ya wafanyakazi Serikalini iliporekebishwa na UTUMISHI kutokana na bajeti ya sasa, marekebisho kwa upande wa Pensheni hayakufanyika. Hivyo, fedha zinazohitajika kwa ajili hii ni shilingi 12,990 milioni ili wastaafu wasipate madhara ya kutokuwa wametengewa fedha zao kwa msimu huu.

(c) Malipo kwa Wadai wa Mashirika yanayobinafsishwa kupitia Mfuko wa (*PPF*), jumla (shilingi bilioni 5.0 bilioni), kutokana na mashirika takriban 151 yaliyobinafsishwa kutolipa michango ya wafanyakazi wao yalipokuwa hai katika Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma (*PPF*) na kwa kuwa



wafanyakazi hao hawawezi kulipwa mafao yao na *PPF* bila michango yao kuwasilishwa, Serikali inalazimika kuchukua mzigo huo ili kuwanusuru wafanyakazi husika.

Majadiliano kati ya *PPF* na Serikali yanaendelea lakini kwa sasa kiasi cha shilingi 2,800 milioni kimetolewa ambapo shilingi nyingine 2,200 milioni zitatolewa kwa *PPF* mwezi huu wa Februari, 2004 ili lianze kuwalipa wafanyakazi hao. Kiasi cha madeni ya pensheni ya Mashirika hayo kwa *PPF* kilichothibitishwa ni shilingi 18,419,000,000/= ambazo zitatengwa katika bajeti ijayo.

(d) Fidia kwa Serikali za Mitaa. Bajeti ya mwaka 2003/2004 ilikuwa imetenga shilingi 4,000 milioni kwa ajili ya kufidia mapato ya Halmashauri za Wilaya na Miji yaliyotokana na kufutwa kwa kodi ya maendeleo na nyinginezo zilizokuwa kero kwa wananchi. Uchambuzi uliofanywa na TAMISEMI na Hazina baada ya Bajeti, umebaini kwamba, kiasi cha fidia hiyo kinachohitajika mwaka huu wa fedha ni shilingi 22,990 milioni. Hivyo, nyongeza inayoombwa katika eneo hili ni shilingi 18,009 milioni. Hadi sasa kiasi cha shilingi 12,000 milioni kimeshatolewa kwenda Serikali za Mitaa na shilingi bilioni 11 zilizobaki zitatolewa mwezi Machi, 2004. Kiasi kitakachotolewa mwaka hadi mwaka kitaainishwa kwenye bajeti ya ruzuku kwa Halmashauri na kitatofautiana kwa mujibu wa vigezo vipya vya kitaalamu vitakavyotumika kwa kila Halmashauri.

(e) Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Sh. 14.27 bilioni. Katika Bajeti ya mwaka huu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imetengewa shilingi 1,100,000,000/= kwa ajili ya Daftari la Wapiga Kura na shilingi 3.0 bilioni zimetengwa kwa ajili ya Vitambulisho vya Taifa (*National Identity Card*). Sasa imebainika kwamba, zoezi la kutayarisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linahitaji si chini ya shilingi 29,922 milioni (bilioni 29.9). Kiasi kitakachohitajika mwaka huu wa fedha ni shilingi bilioni 18.37 bilioni na kilichobaki kitahitajika mwaka ujao wa fedha. Kwa kuwa ziko shilingi bilioni 4.1 kwenye Bajeti ya 2003/2004, matumizi ya ziada yanayoombwa kwa mwaka huu ni shilingi 14,270 milioni.

(f) Ukaguzi wa dhahabu, shilingi 9.6 bilioni. Kufuatia hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu uchimbaji na usafirishaji wa dhahabu, Serikali iliamua kuajiri Kampuni ya Kitaalam, kufanya ukaguzi wa dhahabu kwa lengo la kubaini gharama za uzalishaji, mapato ya mauzo nje, aina na kiasi cha dhahabu na madini yanayofungamana na dhahabu hiyo yaani shaba na fedha. Zoezi hilo, lilianza Julai, 2003 na linaendelea. Gharama ya kukagua dhahabu hii ni dola za Kimarekani 800,000 kwa mwezi kwa kutumia asilimia 1.9 ya thamani ya dhahabu safi inayosafirishwa nje ukiondoa gharama za kusafisha na kusafirisha. Hivyo, kwa kipindi cha miezi 12 kuanzia Julai, 2003 hii ni sawa na shilingi bilioni 9.6.

(g) Kuimarisha uwezo wa *TRC*, kusafirisha chakula cha njaa, shilingi 2.3 bilioni. Hivi sasa kuna mlundikano Bandarini Dar es Salaam wa chakula kilichoingizwa nchini kutoka nje kwa sababu ya uwezo mdogo wa Shirika la Reli (*TRC*). Ili kulikabili tatizo hili, Serikali inahitaji kutoa msaada kwa Shirika hilo wa shilingi 2.3 bilioni za dharura.

(h) Nyongeza ya Chakula cha Njaa. Kutokana na hali ya ukame inayoendelea hapa nchini, fedha za nyongeza kiasi cha shilingi bilioni 10.0 zitahitajika kwa ajili ya chakula cha njaa. Nitaelezea hali hii baadaye.

(i) Ruzuku ya kufidia gharama za umeme kwa Shirika la *TANESCO* shilingi bilioni 4.05 na mahitaji mapya ya dharura shilingi bilioni 10.0. Kiasi cha shilingi bilioni 4.05 kinahitajika kama nyongeza ya shilingi 37,250 milioni zilizotolewa tayari ili kukidhi mahitaji ya msaada kwa *TANESCO* ya shilingi 41,300 milioni. Aidha, kiasi cha shilingi nyingine bilioni 10.0 kinahitajika kama nyongeza kwa fungu la dharura.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, kwa utaratibu wa kisheria, matumizi ya ziada ya shilingi 87,250 milioni ndiyo yanayoombewa kibali cha Bunge. Matumizi hayo yatagharamiwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo:-

(a) Ongezeko la ukusanyaji mapato ya ndani, (*over performance*), jumla ya shilingi 7,580 milioni.

- (b) Ongezeko la misaada ya Bajeti, Jumla ya shilingi 39,670 milioni.
- (c) Kupunguza akiba ya Serikali ndani ya Benki Kuu, jumla ya shilingi 40,000 milioni. Jumla kuu ni shilingi 87,250 milioni.

Mheshimiwa Spika, Serikali pamoja na mahitaji haya ya ziada, inaendelea kutekeleza sera zake za uchumi mpana kama ilivyopangwa. Hata hivyo, kutokana na ukame ambao umeathiri uwezo wa Shirika la Umeme wa kuzalisha umeme, na kulazimika kununua umeme wa *IPTL* pamoja na kutumia mitambo yake ya Ubungo inayotumia mafuta ya *Jet-A-1* na kwa kuwa ukame huo umeathiri uzalishaji wa chakula na mazao mengine ya kilimo, Serikali inalazimika kuwasilisha Muswada huu wa Makadirio ya Nyongeza za Matumizi ili kuhakikisha kwamba, uchumi hauyumbi na Wananchi wanapata chakula.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe maelezo juu ya maeneo yanayohitaji nyongeza ya fedha kwa njia ya *Supplementary Appropriation*, ambayo ni pamoja na chakula cha njaa, shilingi 10,000 milioni, ruzuku kwa *TANESCO* shilingi 37,250 milioni na ununuzi wa ndege ya Serikali shilingi 40,000 milioni, kama ifuatavyo:-

(a) Fungu la 43 - Wizara ya Kilimo na Chakula: Serikali imelazimika kutumia fedha nyingi za ziada kununua na kusambaza chakula katika maeneo yaliyokumbwa na njaa kupitia Mfuko wa Akiba ya Chakula wa Taifa kutokana na hali ya njaa kuwa kali kuliko ilivyotazamiwa. Hadi mwisho wa Desemba, 2003, kiasi kiasi cha shilingi bilioni 8.0 zilikuwa zimetolewa kwa ajili hiyo. Ingawa fedha zilizotengwa kwenye Bajeti ya 2003/2004 zilikuwa shilingi bilioni 2.2 tu. Mwezi huu zimetolewa tena shilingi 1.0 bilioni ili kutoa chakula kutoka Akiba ya Chakula (*SGR*) na kukipeleka kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa. Kwa hiyo, hadi sasa tumetumia shilingi bilioni 6.8 zaidi ya Bajeti iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya chakula cha njaa. Inakadiriwa kwamba, dharura ya chakula kwa ujumla kabla ya mavuno yajayo, itahitaji shilingi bilioni 10.0 zaidi ya kiasi kilichotengwa katika Bajeti ya mwaka 2003/2004 na kile ambacho kimetokana na uhamisho wa ndani. Matumizi hayo, ndiyo sasa ninayoombea kibali cha Bunge hili.

(b) Fungu la 58 - Wizara ya Nishati na Madini: Kupungua kwa maji katika mabwawa yanayozalisha umeme kumelazimisha *TANESCO* kupunguza uzalishaji wa umeme kwa kutumia maji. Kama *TANESCO* ingeanza mgao wa umeme, uchumi ungeathirika sana na kungekuwa na upungufu mkubwa wa mapato ya Serikali. Serikali ililazimika kuongeza ruzuku kwa *TANESCO* ili kuiwezesha kununua umeme huo aghali wa mtambo wa *IPTL* na kuendesha mitambo yake ya Ubungo inayotumia mafuta ya *Jet-A-1* kuzalishia umeme. Hadi mwisho wa Desemba, 2003 shilingi 16.3 bilioni za ziada zilikwishatumika kwa ajili hii na shilingi 12 bilioni nyingine zilizotolewa Januari, 2004 na kufanya jumla ya shilingi 28.3 bilioni. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi 15.0 bilioni ambazo *TANESCO* ilikuwa inaidai Serikali ya Muungano na sasa Serikali haina deni la umeme tena kwa *TANESCO*. (*Makofi*)

Hata hivyo, kwa kuwa mabwawa ya maji yanayozalisha umeme hayajajaa vya kutosha, *TANESCO* inaendelea kununua umeme wa *IPTL* na kwa kuwa hakuna uhakika wa lini tatizo la uhaba wa maji ya kuzalishia umeme litakwisha, Serikali inaomba idhini ya Bunge hili Tukufu ya kutenga kiasi cha shilingi 37,250 milioni kwa ajili ya kuisaidia *TANESCO*.

(c) Fungu cha 61 - Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi: Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba, Bunge la Bajeti la mwaka 2002/2003 lilipitisha kusudio la kununua ndege mpya ya Serikali. Baada ya hapo Serikali ilifanya mazungumzo na Kampuni ya *Gulfstream Aerospace Corporation* ya Marekani, ambayo ndiyo ilishinda mchujo wa Zabuni. Ndege inayonunuliwa ni kwa bei ya dola za Marekani 46.2 milioni pamoja na programu ya matengenezo, mafunzo, huduma za matibabu ya dharura na sifa nyingine nyingi. Malipo ya awali ya dola za Marekani milioni 9.0 yamelipwa kutokana na fedha zilizokuwa zimetengwa katika bajeti na ndege inatarajiwa kuwasili kati ya Juni na Septemba, 2004. (*Makofi*)

Kiasi kinachoombewa matumizi ya ziada ni sawa na dola za Marekani 37.2 milioni ambayo ni sawa na shilingi 40.0 bilioni.

Mheshimiwa Spika, matumizi ninayaomba fedha za nyongeza yanahusu uhai wa Taifa na maslahi ya wananchi. Pia ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala, maamuzi ya nyuma ya Bunge lako Tukufu na ahadi za Rais na Serikali kwa ujumla kwa wananchi. Bila chakula wananchi watafikiria nini Serikali yao? Bila kusomesha wanafunzi walioshinda mitihani ya darasa la saba watoto wetu watapataje matumaini bora ya baadaye, wataionaje Serikali yao na Bunge la wazazi wao? Bila umeme, kukua kwa uchumi wetu, ongezeko la mapato yetu, ongezeko la wawekezaji na kadhalika lingewezekekanaje? *(Makofi)*

Mambo haya ndiyo yaliyoifanya Serikali isisite kufanya maamuzi haraka, ndiyo yanayotofautisha kati ya Serikali lelegege na Serikali madhubuti inayosimamiwa na kushauriwa na Bunge madhubuti. *(Makofi)*

Naomba Waheshimiwa Wabunge, waiunge mkono Serikali kwa hayo iliyokwishatenda na itakayotenda hadi Juni, 2004 kwa gharama nilizoelezea.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Makadirio haya ya Nyongeza, Mheshimiwa Njelu Kasaka.

**MHE. NJELU E.M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 70(ii) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2003, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati yangu kuhusu Muswada wa Sheria wa Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 yaani *Supplementary Estimates No. 1* ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Kamati, kwa kuhudhuria na kushiriki katika kujadili Muswada uliotajwa hapo juu na kwamba naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo: Kwanza ni Mheshimiwa Njelu E.M. Kasaka, ambaye ni Mwenyekiti, Mheshimiwa Lephy B. Gembe, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Simon M. Mbilinyi, Mheshimiwa Edson M. Halinga, Mheshimiwa Stanley H. Kolimba, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Hasnain M. Murji, Mheshimiwa Dr. Talala Bana Mbise, Mheshimiwa John L. Mwakipesile, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Raphael N. Mlolwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Wote nawashukuru sana kwa michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kuwasilisha mbele ya Kamati, hotuba yake fupi yenye maudhui na makusudio ya Muswada yaliyolenga katika kupata kibali cha Kamati cha kuiruhusu Serikali kufanya makadirio ya matumizi ya ziada kwa mwaka 2003/2004 akisaidiwa na Katibu Mkuu Mwandamizi wa Wizara hiyo, Ndugu Grey Mgonja. Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutoa ufafanuzi katika maeneo mbalimbali ya Muswada ulioisaidia Kamati kufikia uamuzi muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaliomba Bunge liidhinishe Bajeti ya Nyongeza ya Sh. 87.25 bilioni ili kukabiliana na njaa nchini na kutoa ruzuku kwa *TANESCO* na kununua ndege ya Serikali. Matumizi mengine yaliyojitokeza nje ya Bajeti ni pamoja na kugharamia Mfuko wa Pensheni, fidia kwa Serikali za Mitaa, Mfuko wa *PPF* na kuandaa Daftari la Wapiga Kura.

Kamati ilielezwa kuwa ukiondoa gharama za njaa, *TANESCO* na kununua ndege ya Serikali, matumizi mengine yamegharamiwa kwa kuhamisha fedha kutoka mafungu mengine ndani ya Bajeti iliyoidhinishwa mwaka 2003/2004. Kamati inaunga mkono Bajeti ya Nyongeza kwa kuzingatia hali mbaya ya chakula nchini hivi sasa na uwezekano wa kukosa umeme iwapo fedha hizi hazitaidhinishwa. Aidha, Kamati imeunga mkono kwa kuridhika kuwa fedha za nyongeza zitapatikana bila kutoza kodi au ushuru wowote. Kwa hatua hiyo ya kutowabebesha wananchi mzigo wa moja kwa moja, Kamati inaipongeza Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono Bajeti ya Nyongeza, Kamati ina maoni kwamba, matatizo ya njaa na kupungua kwa uzalishaji wa umeme kwa Tanzania ni masuala ambayo kwa kweli kwa kiwango fulani yanatabirika na pia yanaweza kuzuilika iwapo mipango thabiti na ya makusudi inaweza kutekelezwa. Ni jambo lililowazi kuwa kilimo cha Tanzania ni cha kubahatisha, hakitumii mbolea ya kutosha na ni cha kujikimu. Utaalam na maarifa katika kilimo ni kidogo sana kutokana na kuzorota kwa utafiti na huduma za ugani. Uzalishaji wa ziada hutokea bila kutarajia na inapotokea hivyo masoko ya uhakika hukosekana na hivyo kuwavunja moyo wakulima. Kutokana na kilimo kutosimamiwa vizuri hata Mikoa yenye mvua nyingi kama Kigoma na Mikoa yenye maji mengi kama Morogoro na Kigoma yenyewe haijaweza kutoa ufumbuzi wa tatizo la njaa nchini.

Mheshimiwa Spika, ingawa ni kweli sehemu nyingi za Tanzania zilikumbwa na ukame, matatizo tuliyonayo sasa kwa kiwango fulani yamechangiwa na *management* mbaya na usimamizi mbovu wa kilimo chetu hapa nchini. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa kilimo kinakuwa kweli ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania na njia kuu ya kuwapatia Watanzania chakula. Tunaipongeza Serikali kwa kuanza kukarabati vituo vya utafiti wa kilimo na kuvipatia mahitaji mbalimbali muhimu. Hata hivyo, Kamati inashauri hatua hizo sasa zifuatiwe na ongezeko la huduma za ugani, ongezeko la matumizi ya Mbolea na ongezeko la uzalishaji wa mazao kwa hekta moja. Kilimo chetu lazima kibadilike kuhimili mabadiliko ya hali ya hewa, mara nyingi sisi tunazalisha kiasi cha kula miezi mitatu na hali ya hewa ikibadilika kwa miezi mitatu basi mnakuwa katika hekaheka ya kutafuta chakula.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali inaomba matumizi ya nyongeza ya Sh.37.25 bilioni kama ruzuku kwa *TANESCO*. Kiasi hiki ni nyongeza kwa Sh.28.3 bilioni ambazo zilikuwa zimeshatumika kuishia Desemba tulipokutana na Waziri mwezi Januari na sasa zinaombwa nyingine ili ziwe nyongeza katika hizo ambazo zimekwishatumika. Tatizo la umeme, Kamati ilielezwa limesababishwa na kupungua kwa maji katika mabwawa yanayozalisha umeme baada ya ukame wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukumbushane kwamba katika miaka ya hivi karibuni, mvua zimepungua sana nchini mwetu na hata majira yake hayatabiriki sawasawa. Pia hakuna aliye na uhakika kuwa huko tuendako hali ya mvua itakuwa nzuri zaidi kuliko ilivyo sasa. Utabiri wa dunia ni kwa maji kupungua zaidi kuliko kuongezeka. Tanzania inapaswa kulielewa hilo na kujiandaa ipasavyo. Tanzania kutegemea maji kuzalisha umeme itajiweka katika mazingira magumu sana siku zijazo kadri mvua inavyopungua. Katika miaka ya ukame tutakuwa na matatizo makubwa zaidi na huenda tukulazimika kuzima umeme.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili huenda lisingekuwepo iwapo uamuzi ungefanywa siku za nyuma wa kuzalisha umeme kwa makaa ya mawe badala ya maji na huenda tukaepukana nalo siku zijazo iwapo uamuzi utafanywa sasa kuanzisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe. Tanzania inayo makaa ya mawe kwa wingi katika eneo la Mchuchuma na kwa mujibu wa taarifa za wataalam, ubora wake ni wa hali ya juu. Makaa ya mawe yanapatikana pia Kiwira Mkoani Mbeya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii wametembelea Mchuchuma mara mbili mwaka 2002 na mwaka 2004. Kamati ilielezwa kuwa tafiti za kutosha zilishafanywa na mwekezaji amepatikana lakini mradi hauwezi kuanza kwa sababu maelezo ya Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC*), ambalo limekabidhiwa kusimamia mradi huo, yanahitilafiana na maelezo ya Wizara ya Nishati na Madini. *NDC* wanasema mradi unafaa na utafiti umekamilika Wizara inasema utafiti zaidi unahitajika ili kujua ubora wa mradi.

Mheshimiwa Spika, suala la kujiuliza ni kwa nini viongozi wa ngazi za juu Serikalini wameshindwa kuziweka pamoja taasisi hizi mbili ili kujua ni ipi inasema kweli. Kwa matatizo ya umeme tuliyonayo na hali ya wasiwasi iliyopo kwa miaka ijayo, je, tunao muda wa anasa wa kusubiri mpaka taasisi hizi mbili zikubaliane kwa jambo muhimu kama hili? Tunafikiri kutofautiana kwa taasisi hizo mbili yaweza kuwa ni mbinu tu ya kijanja ya kutaka kuchelewesha mradi wa Mchuchuma. Tunaliomba Bunge hili lisikubaliane na mbinu hizi. Serikali itoe maelezo ya kuridhisha kwa nini mradi huu hauanzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Februari, 2004, Rais Benjamin Mkapa alisema hapa Bungeni tusicheleweshe maamuzi ili kuharakisha kukua kwa uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, Kamati inashauri Serikali iamue kuanzisha mradi wa kuzalisha umeme kwa makaa ya mawe ya Mchuchuma bila ya kuchelewa zaidi. Tunapenda kuona mradi wa Mchuchuma katika Bajeti ya 2004/2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa Mchuchuma unao uwezo wa kuzalisha megawatt 400 za umeme na mwezi huu wa Februari, Tanzania itatia saina Mkataba wa Umoja wa Forodha wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sasa kulikuwa na maneno kwamba, Tanzania inao umeme mwingi zaidi kiasi kwamba iwapo Mchuchuma itaanzishwa basi tutakuwa na umeme zaidi kuliko tunavyohitaji, jambo ambalo mimi siliamini sana. Lakini iwapo mahitaji ya Tanzania yatakuwa ni madogo kuliko umeme utakaozalishwa, utakuwa mwingi kuliko mahitaji ya Tanzania, tutawauzia majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini tuzuie uzalishaji wa ndani na kisha tununue umeme kutoka Zambia? Kuna huu mpango wa kununua umeme kutoka nchi jirani lakini kama *capacity* ya ndani ni nzuri na ni kubwa basi tuzalish ndani. *South Africa* sasa hivi inauza umeme kwa majirani zake Kusini mwa Afrika na sisi tukiua umeme sioni kama kuna tatizo lolote iwapo tutakuwa na umeme wa uhakika unaotokana na makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imelazimika kulipa pensheni ya waliokuwa wafanyakazi wa mashirika yaliyobinafsishwa, Kamati inaunga mkono uamuzi huo. Hata hivyo, Kamati imesikitishwa kwamba hatua hii imefikiwa kutokana na uzembe au ubadhirifu wa baadhi ya viongozi wa mashirika yaliyobinafsishwa kwa kutowasilisha makato ya wafanyakazi kwenye Mfuko wa Pensheni. Hata hivyo, Serikali haikuwachukulia hatua ya kinidhamu viongozi waliohusika na mambo hayo. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa, makato ya wafanyakazi ya mashirika yake yanawasilishwa kwenye mifuko ya pensheni ili kuepuka kuwabebesha mzigo walipa kodi ya namna hii. Inapobainika makato hayawasilishwi wahusika wachukuliwe hatua za kinidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa ndege ya Serikali, Kamati inakubaliana na uamuzi huo ili kuona viongozi wetu wanasafiri katika vyombo vizuri na salama. Isipokuwa kwenye Kamati Waziri alikuwa hajaeleza bei yake, nashukuru leo ameieleza hapa na mimi nilikuwa nimesema hata hivyo Kamati haikuelezwa bei halisi ya ndege itakayonunuliwa. Kamati ni wajibu wake kujua gharama halisi ya ndege ili Bunge hili linapoidhinisha liidhinisha kitu linachokijua. Kamati inashauri bei ya vitu maalum vinavyoombewa fedha katika Bunge kwa siku zijazo basi ijulikane mapema. Namshukuru Waziri, amefafanua hapa sasa hivi kwamba, zilishalipwa shilingi bilioni tisa bado zinahitajika 36 bilioni. Mnaweza kugundua kwamba bei ni ya juu sana lakini kutokana labda na umuhimu wake hatuna kipingamizi nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kugharamia ukaguzi wa dhahabu inayozalishwa hapa nchini kwa Sh.9.6 bilioni, Kamati iliona kama ni mzigo kwa Serikali ikilinganishwa na faida itakayopatikana. Kwa sababu mpaka sasa hivi mchango wa madini ni mdogo kwa Serikali yetu na inapogharamia tena Sh.9.6 bilioni tunafikiri inaweza kuwa inazidi kujibebesha mzigo zaidi katika eneo ambalo bado haipati mapato mazuri sana na hivyo kushauri pale inapowezekana, wawekezaji katika sekta ya madini basi washirikishwe kuchangia kulipia gharama za ukaguzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Kamati imeitaka Serikali kudhibiti watendaji wabovu wasiowajibika katika matumizi ya fedha za Serikali pale zinapoidhinishwa na kwamba zitumike kwa makusudio yanayotegemewa. Kamati imesisitiza usimamizi imara kwa miradi inayotengewa fedha katika Bajeti ya Serikali ili Taifa lifaidike na gharama hizi. Nidhamu ya matumizi ya fedha ni muhimu hata baada ya

kuidhinishwa katika Bunge. Hii haina maana kwamba, maadam Bunge limeidhinisha basi watu wawe wanatumia fedha kadri wanavyotaka wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, juzi wakati Waziri anaongea na Waandishi wa Habari, alisikitishwa na matumizi mabaya, watu wanajinunulia magari wanavyotaka wao wenyewe kana kwamba hakuna usimamizi zaidi. Nafikiri kuna haja ya kuzisimamia fedha hata baada ya kuwa zimeidhinishwa kwamba zitatumika katika Wizara fulani bado zisimamiwe kule zinakokwenda kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali na uongozi mzima wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwa kazi nzuri inayofanywa ya kukusanya mapato ya Serikali na kuvuka viwango vya malengo waliyojiwekea. Kwa taarifa ambayo Waziri alitupatia kwenye Kamati mwezi Desemba, *TRA* iliweza kukusanya Sh.133 bilioni kwa mwezi mmoja. Hayo ni mafanikio makubwa sana na sisi tuliipongeza *TRA* na tunazidi kuipongeza. Tunaamini uwezo wa kupata kodi zaidi bado upo iwapo kila mtu atalipa kodi. Huu ni mwelekeo mzuri wa kujitegemea katika kugharamia mipango yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano katika Kamati na kupata maelezo ya kina kutoka kwa Waziri pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ilikubaliana na Muswada na kuupitisha. Kwa hiyo, hapa naunga mkono Bunge hili liidhinishhe matumizi ya nyongeza kama yalivyoombwa na Serikali, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu nyongeza ya matumizi ya mwaka wa Fedha 2003/2004 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Fedha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuanza kwanza, kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake kwa kuweza kwa kiasi fulani kusimamia mapato na matumizi ya Serikali. Aidha, tunaomba kuipongeza *TRA* kwa kazi nzuri ya kukusanya mapato ya Serikali hadi kuvuka lengo, jambo ambalo limeipa uwezo Serikali wa kuja kifua mbele katika Bunge lako Tukufu, kuomba matumizi ya ziada.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *TRA*, tunawashauri wajitahidi kujenga mahusiano na maelewano mazuri na walipa kodi hasa walipa kodi wa kati na wadogo wadogo. Bado yapo malalamiko ya usumbufu katika kutoa mizigo bandarini, ukadiriaji wa kodi na kadhalika. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa uwezo wa kurekebisha kasoro hizo mnao, timizeni wajibu wenu kama mlivyofanya kwa ukusanyaji wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri ameomba Bunge lako Tukufu lipitishhe Muswada wa Sheria ya Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya Sh.87,250 milioni kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya ziada kwa mwaka wa fedha 2003/2004. Aidha, Mheshimiwa Waziri anaomba kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu pamoja na uwezo wa kisheria alionao kwamba, atatumia Sh.89,534 milioni kutokana na uwezo wa kuhamisha kutokana na *re-allocation through savings from within*, hivyo kufanya matumizi ya ziada jumla ya Sh.177,784 milioni.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Sh.89,534 zitakazofidiwa kwa njia ya uhamisho wa fedha (*re-allocation warrant*) ni kwa matumizi yafuatayo:-

Kwanza, gharama za ongezeko la Walimu wapya wa Sekondari Sh.2,424,000,000. Kambi ya Upinzani haina matatizo na matumizi haya ila inashangaa namna Serikali inavyoshindwa kutafsiri takwimu kwa usahihi, kwani Mheshimiwa Spika, kama uwezo wa Sekondari ni wa asilimia 26.9 wa wanafunzi wanaoweza kuingia *Secondary School* wakati mwaka 2003 asilimia 27 walifaulu kungehitajika kuongezwa shule za Sekondari na Walimu, kwani pia tulielewa kuwa tumepanua wigo wa Kidato cha Kwanza kutoka wanafunzi 116,296 hadi wanafunzi 496,018, hivyo ni wazi kuwa madarasa ya Sekondari na Walimu wa ziada wangehitajika.

Mheshimiwa Spika, kama Sera ya Elimu ya Msingi ingeunganishwa na Sera ya Elimu ya Sekondari kama ilivyo kwenye Sera za Upinzani, tungeweza kupanga vizuri zaidi na kuepukana na mtindo wa Zimamoto. *(Makofi)*

Kambi pia inaishauri Serikali iandae utaratibu wa kutoa vivutio maalum kwa wawekezaji wa Elimu ya Sekondari ili kuziba pengo la wanafunzi waliofaulu na kuachwa. Hii itapunguza kiwango cha ujinga, umaskini na ujambazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kasoro hizo, Kambi ya Upinzani inaunga mkono matumizi ya ziada ya Sh.2,424 milioni. *(Makofi)*

Pili, matumizi kwa Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Serikali Shilingi 18.89 bilioni. Kambi ya Upinzani inaafiki matumizi haya ila bado naona Serikali haijawa makini katika ku-focus matatizo baada ya mafanikio maana kila ukipata mafanikio huwa kuna matatizo ambayo yatatokea. Ni dhahiri ukipandisha mshahara na malipo ya pensheni yataongezeka, hivyo Serikali ingejua mapema wakati wa Bajeti kiwango halisi cha malipo ya pensheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kasoro hiyo, Kambi ya Upinzani inakubaliana na pendekezo la Waziri. *(Makofi)*

Tatu, fidia kwa Serikali za Mitaa Sh.22.99 bilioni. Kama tulivyosema wakati wa Bajeti wakati Serikali ilipofuta Kodi ya Maendeleo bila ya maandalizi ya kutosha na tulisema pamoja na udhaifu wetu kuwa “Nguo ya kuazima haisitiri matako” na kwamba Halmashauri nyingi zitayumba katika utekelezaji wa kazi zao za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inakubaliana na matumizi haya ila Serikali iwe makini wakati wa kubadilisha Sera, ifanye utafiti wa kutosha yasiwe maamuzi ya kisiasa tu. Aidha, matumizi haya yafuatiliwe ili kupata thamani halisi ya matumizi. *(Makofi)*

Nne, Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Sh.14.27 bilioni. Wakati nikiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani wakati wa kikao cha Bajeti, tulihoji juu ya kutengwa Sh.3 bilioni kwa ajili ya vitambulisho na 1.1 billion kwa ajili ya Daftari la Kudumu la wapiga kura lakini hatukupewa majibu ya kuridhisha. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani na Watanzania wote, tunaungana na Rais Mkapa katika kusimamia na kutekeleza Muafaka baina ya CCM na CUF, ambao ndani yake yapo maamuzi ya kuanzishwa Daftari la Kudumu kwa upande wa Zanzibar na kwa Bara kutekeleza Katiba ya Nchi inavyoagiza kuanzishwa kwa Daftari la Kudumu. *(Makofi)*

Pamoja na kuunga mkono kwetu, tunaomba kutumia fursa hii kuomba kwamba kazi ianze haraka na iwe na uwazi wa hali ya juu. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaunga mkono matumizi haya. *(Makofi)*

Tano, ukaguzi wa dhahabu Sh.9.6 bilioni. Kambi ya Upinzani inaona kuwa matumizi haya si ya dharura, kwani Serikali ilijua mapema kuwa inakusudia kufanya matumizi haya. Pili hakuna taarifa ya awali iliyowasilishwa kwenye Bunge hili au Kamati yake juu ya matumizi haya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kupatikana mtaalam wa ku-assay na kujua bei ya dhahabu, Kambi ya Upinzani inaona kuwa hakuna uwazi wa kutosha katika matumizi haya, aidha kwa kuwa kuna mrahaba unaotokana na dhahabu kwa nini:-

- (a) Isiwe *self-financing* hii kazi yaku-assay na kujua bei? *(Makofi)*
- (b) Tusitumie utaratibu wa TANSOLT ambao Williamson Diamond inalipa \$ 4.5 kwa Caret moja ya Almasi inayochambuliwa, ukubwa, uzuri na umbile lake? *(Makofi)*
- (c) Kwa nini iwe inafanyika kila mwaka? *(Makofi)*

(d) Kwa nini matumizi haya yaitwe ya dharura wakati hii ni kazi ya kudumu hadi dhahabu itakapomalizika nchini? (Makofi)

(e) Serikali haisemi itafaidika kwa kiasi gani na zoezi hili *in terms of income*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hakuna uwazi wa matumizi haya na taarifa yenyewe ni finyu, Kambi ya Upinzani haiungi mkono matumizi haya. (Makofi)

Sita, kuimarisha uwezo wa TRC kusafirisha chakula cha njaa Sh.2.3 bilioni. Pamoja na ufinyu mkubwa wa taarifa ya matumizi halisi ya fedha inayoombwa, Kambi ya Upinzani inaunga mkono matumizi ya kuboresha huduma za reli ili TRC iweze kusafirisha chakula cha njaa. Ni matumaini yetu kuwa baada ya kazi hii kumalizika, Bunge litaarifiwa rasmi namna fedha hii ilivyotumika (mchanganuo) ili *value for money* ijulikane. (Makofi)

Saba, Mfuko wa PPF Shilingi 5 bilioni. Katika Bajeti ya mwaka 2002/2003, Serikali ilisema kuwa mapato taslimu yanayotokana na kuuzwa kwa Mashirika ya Umma ni Sh.217.2 bilioni. Asilimia 42.2 zilihamishiwa Hazina na asilimia 42.7 zililipiwa madeni ya mashirika pamoja na mafao ya wafanyakazi na asilimia 5.3 kulipia gharama za PSRC na asilimia 0.6 kulipia gharama za Mfuko wa Ubinafshaji na asilimia 8.78 ilikuwa ni fedha taslimu.

Mheshimiwa Spika, je, kutokana na kauli ya Serikali kwamba asilimia 42.7 baadhi yake walilipwa wafanyakazi mafao yao ikiwa ni pamoja na PPF kwa nini leo Serikali ifanye *re-allocation* kwa ajili ya kulipia deni hili?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imekuwa ikipiga kelele wakati wote juu ya maslahi ya watumishi wa Serikali na Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa hivyo kuuliza kwetu ni kutaka kupata usahihi wa kauli ya Serikali na kujua fedha asilimia 47.7 zimetumikaje. Pamoja na kwamba tunaunga mkono kulipwa mafao ya wafanyakazi wa mashirika yaliyobinafsishwa lakini tunaomba kupata maelezo hayo. (Makofi)

Nane, chakula cha njaa Sh.10 bilioni. Wakati Wabunge walipokuwa wakijadili Bajeti ya 2003/2004, walieleza hali halisi ya upungufu wa chakula nchini. Kwa upande wa Kambi ya Upinzani, tulitoa hata takwimu kuonyesha ufinyu wa Bajeti katika kukabiliana na njaa. Wapo waliosema kuwa tatizo la njaa linachukuliwa kisiasa.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona hadi leo Serikali imeshindwa kutumia na kuchambua takwimu za Hali ya Hewa:-

- (a) Kuweza kutabiri hali ya mvua;
- (b) Kujua kiwango cha ukame tunaotegemea kuwa nao; na
- (c) Hata kutumia vigezo vya miaka ya nyuma tuliyopata ukame.

Matokeo ya hayo ni kuwa na matumizi ya ziada ya dharura ambayo pia hayakidhi mahitaji halisi ya balaa la njaa.

Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kuwa iwe makini katika kutathmini hali ya uzalishaji wa chakula nchini na pia ifuatilie suala la kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji kwani ni aibu kuwa na ekari 250,000 kati ya milioni 4 zinazomwagiliwa hivi sasa katika kipindi cha miaka 44 ya kujitawala na hizo ekari 250,000 hatujui zinazalisha kiasi gani kwa mwaka. Ni vema Serikali ikaeleza tunahitaji ekari ngapi za umwagiliaji ili tusikumbwe tena na balaa la njaa. Aidha, Serikali izingatie thamani ya Pesa (*value for money*) na ubora wa chakula kinachoagizwa nchini kwani pamoja na waagizaji kusamehewa kodi, wapo wanaoleta chakula kisichokuwa kizuri na kuuza bei ya soko hivyo kujilimbikizia faida mara mbili, ile itokanayo na kodi iliyosamehewa na ile anayouzia yaani bei ya soko.



Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali yafuatayo:-

- (a) Ikikague chakula chote kilichoagizwa nchini ili kujua ubora wake na bei zilizoagizishiwa ili tujue kwamba kodi iliyosamehewa ni sawa; na
- (b) Ieleze Bungeni ni kiasi gani cha kodi kilichosamehewa katika muda huu wafanyabiashara walipoleta chakula nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukubaliana na maombi ya Waziri, tunaomba ufafanuzi huo utolewe. *(Makofi)*

Tisa, ruzuku kufidia gharama za umeme kwa Shirika la *TANESCO* Sh.4.05 bilioni na mahitaji mapya ya Sh.10 bilioni. Madhumuni makubwa ya Sera ya Ubinafsishaji ni kwa Serikali kuacha kutoa ruzuku. *TANESCO* ni moja ya mashirika yaliyobinafsishwa uongozi ili kuondokana na kasoro za kiutendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikilipa madeni yake *TANESCO* bila ya Serikali kusema ni kiasi gani cha mapato ya *TANESCO* kutokana na uongozi mpya kinapunguza mzigo wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi mwisho wa Desemba, 2003 na Januari, 2004, Serikali imekwishalipa deni lake kwa *TANESCO* Sh.15 bilioni na kuwapa ruzuku ya Sh.13.3 bilioni. Pamoja na hayo, Serikali inaomba iidhinishiwe Sh.37,250 milioni na kuipa tena *TANESCO* ruzuku.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaomba kuelezwa mchanganuo wa matumizi ya *TANESCO* kwa ruzuku wanayopata kutoka Serikalini ya jumla ya Sh.50.550 bilioni:-

- (a) Litazitumia vipi fedha hizo?
- (b) Linategemea kukusanya kiasi gani cha mapato kutokana na mtaji huo wa 50.550 bilioni wa uendeshaji waliopewa na Serikali?
- (c) Serikali haisemi kuwa hadi lini itaendelea kuibeba *TANESCO* na kwa kiwango gani?
- (d) Kwa kuwa *TANESCO* ni Shirika la Biashara kwa nini lipewe ruzuku badala ya mkopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, pamoja na umuhimu wa kuwa na umeme wa uhakika, tungependa kupata majibu ya kina juu ya sera ya Serikali kwa *TANESCO* na pia kujua ufanisi wa uongozi mpya unaopewa ruzuku kuliko hata uongozi wa zamani wa Wazalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haiungi mkono *TANESCO* kupewa ruzuku. *(Makofi)*

Kumi, maombi ya Sh.87,250,000,000. Kwa mujibu wa maelezo ya Waziri kuwa matumizi haya ya ziada hayatatokana na ongezeko la kodi bali ni kutokana:-

- (a) Ziada ya ukusanyaji wa mapato ya ndani;
- (b) Ziada ya misaada ya bajeti ambayo ni mikopo iliyokuwa haijalipwa kwa kuwa wadai hawajaleta madai yao; na
- (c) Kupunguza akiba ya Serikali Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, atuhakikishie kuwa vyanzo hivi vya mapato anavyotaka kuvitumia sasa havitaathiri Bajeti yetu ya mwaka wa fedha wa 2004/2005, wakati wadai watakapoleta madai yao ya 2003/2004. Mheshimiwa Waziri amesema moja katika mafungu ambayo anachukua fedha ni *savings* ambayo imetokana na wadai kutokuleta madai yao kwa hiyo Serikali

inachukulia hiyo ni *savings* lakini wadai hawa watakapoleta madai yao je, hiyo bado itabaki ni *savings*? Kwa hiyo, yapo mashaka kwamba wadai wanaweza kuwa mwaka huu hawakuleta madai lakini mwakani wakaleta madai kwa hiyo tukawa tunadaiwa mara mbili. Kwa hiyo, ni vizuri Waziri akatufahamisha hawa wadai ambao yeye sasa hivi anachukulia ni *savings*, kwa sababu hawakuleta madai, je, katika kipindi kinachokuja madai haya yakiletwa Serikali haitakuwa imebeba mzungu mwingine tena wa madeni ya ziada? Hili nafikiri ni vizuri Waziri alifafanue.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri atuhakikishie vyanzo vya mapato anavyotaka kuvitumia sasa hivi ni namna gani havitaathiri Bajeti ya mwaka wa fedha 2004/2005 wakati wale wadai watakapoleta madai yao? Aidha, Mheshimiwa Waziri atueleze ni sababu zipi zinazofanya malipo ya ndege yafanywe kwa *Supplementary Budget* wakati Serikali katika mwaka wa 2002/2003 ilitenga Sh.9 bilioni kwa malipo ya awali hivyo Serikali ilijua kuwa mwaka huu wa fedha ni kiasi gani cha fedha kingehitajika?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilipinga ununuzi wa ndege ya Rais kwa wakati huu na hasa ukiangalia kuwa Serikali wakati wote imekuwa ikisema haina fedha, Sh.40 bilioni za kuwapelekea wananchi wa Mikoa ya Kusini umeme hakuna lakini leo Serikali inazo fedha taslimu Sh.47 bilioni za kununulia ndege ya Serikali! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Kambi ya Upinzani ingependa sana Rais wetu awe amepanda ndege mpya kabla ya kumaliza muda wake lakini pia tungependa Rais wetu atakapokwenda nyumbani jamaa zake wa Kusini wamshukuru kwa kuwajali wao kwanza kabla ya yeye mwenyewe binafsi. Hivyo, Kambi bado inabaki na msimamo wake wa kukataa Serikali kununua ndege lakini zaidi haioni uharaka wa kufanya malipo ya ndege iliyotengenezwa kwa mujibu wa mkataba kwa hiyo inajulikana *payment* ya kwanza ni lini, ya pili ni lini na ya tatu ni lini. Hakuna sababu Serikali kuja na *Supplementary Budget* wakati ilikuwa inajua programu kutokana na mkataba. Katika mkataba huo, inasemekana ndege hiyo itakuwa tayari baada ya Septemba, 2004, hivyo itakuwa wakati wa bajeti umeshafika, hakuna sababu ya kuharakisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haikubaliani na bei ya ndege hiyo kuwa ni Sh.47 bilioni kwani kutokana na *Global Security Organization Gulf-stream G550*, ambayo inasemekana inataka kuagiza ambayo haina *options* nyingi na ambayo unapata *Constructor Logistic Support* bei yake ni US\$ 18 na ikiwa ina *options* nyingi kama hii bei yake ni US\$ 26 million. Ni vipi Serikali inunue ndege karibu mara mbili ya bei yenyewe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haiwezi kukubali kuwabebeha Watanzania mzigo wa kodi kiasi hicho, hivyo, haiungi mkono matumizi haya na inaomba Bunge lako Tukufu, liunde Tume kuchunguza manunuzi ya ndege hii ili Watanzania wafahamu matatizo ya kodi wanazotaka kulipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sasa tunaanza mjadala wa jumla. tutasimamia kanuni zinazotawala mjadala hapa Bungeni ili wote waliojiandikisha waweze kupata nafasi. Tunaanza na Mheshimiwa Mgana Msindai, atafuatia Mheshimiwa Mohammed Missanga na Mheshimiwa Thomas Nyimbo jandae.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie juu ya Muswada uliopo mbele yetu wa kuomba fedha kwa ajili ya matumizi muhimu. Ningeomba niunge mkono hoja moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na ununuzi wa ndege. Ununuzi wa ndege ni uamuzi wa Serikali kwa ajili ya Marais wetu na siyo Rais huyu tu peke yake bali kipindi cha kununua ndege kimefika wakati wa Rais tuliye naye sasa. Juu ya bei ya ndege hapa Mheshimiwa Waziri alipokuwa anawasilisha alisema kabisa ni kununua ndege, kutoa mafunzo na mambo mengine. Kwa hiyo, kwa kweli si sahihi kuanza kutaja bei ambazo haziendani na matumizi ya Serikali. Ni budi sisi Waheshimiwa Wabunge kama tunataka kujua tupewe mchanganuo na Serikali, tusianze kutafuta bei za mitaani tukazileta hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi nichangie juu ya ongezeko la fedha kwa ajili ya elimu. Kwa kweli naipongeze sana Serikali kwa sababu mwaka huu vijana wetu wengi wamefaulu na wengi wamekosa nafasi za kuendelea na shule za Serikali. Kwa hiyo, kwa kweli naipongeze Serikali na mwakani wajiandae kutenga fedha nyingi zaidi kwa shughuli hiyo. Hii ikiwa ni pamoja na kuongeza walimu. Tunaomba hizi hela zitolewe haraka kama Waziri alivyosema mpaka kufikia Juni au Julai tuwe tumepata walimu wa kutosha kuwafundisha vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, juu ya Mfuko wa Pensheni, sina kinyongo na hiyo kabisa kwa sababu ni lazima watu wetu walipwe. Lakini ningemwomba Waziri wa Fedha, aangalie na madeni ya pensheni yaliyoko kwenye Halmashauri zetu za Wilaya, madeni ambayo yamekuwepo kwa miaka mingi, madeni ya nyuma ambapo Halmashauri zetu za Wilaya haziwezi kuyalipa. Kwa hiyo, ningomba kwenye hizi fedha za ziada zilipie na yale madeni ambayo Halmashauri zetu za Wilaya zilirithi kutoka madeni ya zamani.

Mheshimiwa Spika, juu ya kuongeza fedha kwenye Halmashauri baada ya kufuta kodi. Kwanza, naipongeze Serikali kwa hatua iliyochukua. Wananchi wetu walikuwa wanateseka sana, wananchi wetu walikuwa hawatulii, wanashinda milimani badala ya kufanya kazi za maendeleo kwa kukwepa kukamatwa kwa kodi. Kwa kweli Serikali imefanya vizuri na tunaomba hizi fedha za kufidia pengo hili ziwe zinakwenda mapema ili Halmashauri zetu ziweze kupanga matumizi yake kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, juu ya daftari la wapiga kura, sina tatizo nalo kabisa kwa sababu limekuwa linapigiwa kelele muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, vile vile sasa hivi wananchi wetu wana njaa na kuna matatizo karibu nchi nzima, mfano rahisi ni kule ninakotoka mimi ambapo pamoja na Serikali kusema kwamba hakuna mtu ambaye amekufa kwa njaa lakini wapo. Ie kula yale majani waliyokula ni kukosa chakula kwa hiyo wamekufa kwa njaa. Kwa hiyo, tunaomba SGR iwezeshe na fedha zilizotengwa kwa ajili ya kununulia chakula cha ziada zitolewe haraka na chakula kiende. Mimi nimetoka Jimboni kwa kweli hali si nzuri. Tunaomba Serikali ijitahidi kupeleka hizi hela haraka sana.

Mheshimiwa Spika, juu ya ruzuku kwenda kwenye Shirika la Umeme, nina imani Serikali yetu ina busara na imefikiria kabisa. Badala ya kulikopesha Shirika la Umeme kwa sababu halina uwezo wa kulipa, nashukuru sana wamewapa ruzuku na wote tunajua sasa hivi uchumi wetu unakua na tusipopata umeme hali yetu itarudi kuwa mbaya. Kwa hiyo, nakubaliana nao ila tu sasa niwaambie na hawa wanaopewa hizi fedha wazitumie kwa makini na waonyeshe zinafanya kazi gani na kwa zile hela ambazo walikuwa wamepanga kutumia kwenye miradi ya maendeleo ziendelee kufanya kazi kwa sababu tayari Serikali imeshawaongezea fedha. Fedha zilizopangwa kama vile kupeleka umeme kutoka Mtinko kwenda Nkungi. Huo umeme upelekwe mara moja ili wananchi wasiendelee kupata tabu.

Mheshimiwa Spika, juu ya umeme wa makaa ya mawe, kwa kweli nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, umefika wakati sasa ni lazima tutafute njia nyingine ya kupata nishati na njia mbadala ambayo tunayo hapa ni makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana tunaposikia kila mwaka haya mambo yanaongelewa lakini sijui utekelezaji wake utakuja kuanza lini. Ni sawasawa na utekelezaji wa kilimo cha kutegemea mvua. Tumeishauri Serikali mara nyingi, umefika wakati sasa tutumie mabonde yetu kwa kulima kilimo cha umwagiliaji na Serikali lazima ijue mzunguko wa uhaba wa mvua. Karibu miaka yote inayoishia na tatu na kwenda mwaka unaofuata wa nne huwa kuna uhaba wa mvua, tungeomba Serikali iangalie hilo na wakati wa neema ndiyo ianzishe huu utaratibu ili tuweze kulima kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, juu ya ukaguzi wa dhahabu, endapo hiki kitu kitakuwa kina manufaa kwa Taifa letu, mimi sina kipingamizi na naiamini Serikali kwamba imefanya utafiti na imegundua kwamba tutafaidika. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri atuambie tutafaidika vipi ili kutoa wasiwasi ambao baadhi yetu wanao, lakini nina imani kabisa Serikali imejua kwamba tutafaidika vipi.

Mheshimiwa Spika, nirudie kuipongeza Serikali kwa sababu sasa hivi linalofanyika ni kuhamisha fedha kutoka mafungu fulani kwenda mafungu fulani. La pili, ni idhini ya kutumia fedha ambazo tunazo, ingekuwa hizi fedha tunaomba kama mkopo au kutoka kwa wafadhili pale ingekuwa kitu kingine. Kwa kweli tuendeleo kujivunia Serikali yetu ya Awamu ya Tatu wakiwemo wenzetu wa *TRA* kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa sababu sasa hivi ni sawasawa na mtu unayetoka nyumbani kwako unakwenda kutembea lakini chakula cha akiba kipo. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri yale machache ayazingatie, lakini kwa kweli nirudie kusema kwamba, suala la njaa siyo la mchezo. Hebu hilo lifanyiwe bidii ili wananchi wetu wasianze kuisema vibaya Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia kuunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukupa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi mapema ya kuchangia katika Muswada huu uliowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu wake wote wawili, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wake wote kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia masuala ya fedha na hasa ukusanyaji wa mapato kama tunavyoambiwa siku hadi siku na Wizara yenyewe pamoja na Mheshimiwa Rais anavyotukumbusha kwamba kwa kweli tumepiga hatua kubwa katika kukusanya mapato yetu. Kazi hii inafanywa na wenzetu na sisi tuna kila sababu ya kuwapongeza, naomba niwapongeze sana na niwaombe waendeleo na kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza wakati, naomba niseme kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono nitasema machache tu. Kwanza, niipongeze Serikali ya Awamu ya Tatu kwa hatua thabiti inayochukua katika kupambana na suala la njaa hapa nchini. Kama Ilani ya Uchaguzi inavyosema kwamba, Serikali ya CCM hata siku moja haitapenda kuona mwananchi wa Tanzania anakufa kwa sababu ya njaa, hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali hii ya Awamu ya Tatu, zimethibitisha kauli hiyo. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu na Waziri wake anayehusika na suala hili la baa la njaa, kwa kazi kubwa ambayo wamefanya. Sisi kwa upande wa Singida nashukuru tumepata fursa ya kupata chakula cha njaa na kimegawanywa ingawa katika baadhi ya Vijiji tu ambavyo vilikuwa vimeonekana kwamba vinastahili kupata chakula hicho cha msaada katika awamu hiyo iliopita.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba, tatizo hili bado lipo. Bado kuna kazi kubwa ya kufanya katika kuona kwamba wananchi wetu wanasaidiwa ili wasipate madhara ya njaa. Tathmini iliyofanyika ilifanyika mwezi wa sita au wa saba mwaka 2003. Mimi sina hakika ni Wabunge wangapi walishirikishwa katika kufanya tathmini ya njaa katika sehemu zao, lakini inaonekana maeneo mengi kwa kweli sisi Waheshimiwa Wabunge hatukuhusika sana katika kuainisha au kubainisha ni Vijiji vipi ambavyo vimeathirika kwa kiasi kikubwa. Ingawa hili ni suala la utaalim, lakini nadhani na sisi tungehusishwa tungeweza kutoa mchango mzuri zaidi, kwa sababu hivi sasa tayari yameshaanza kujionyesha malalamiko mengi tu kwenye baadhi ya Vijiji ambavyo havikupata mgao wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Jimbo langu, Tarafa ya Ikungi na Ihanja, Tarafa mbili nzima hizo zimeachwa, hazikupata chakula kwa maana ya kwamba wao wameonekana kwamba walikuwa na afueni ukilinganisha na Tarafa zingine. Inawezekana kuna ukweli kiasi fulani, lakini pia upo ukweli pia kwa kiasi fulani kwamba kulikuwa na makosa ambayo yamefanyika katika tathmini hiyo. Kwa hiyo, chakula ambacho kimepelekwa sasa kimezingatia yale maeneo ambayo tathmini ilifanyika mwezi Juni au Julai, 2003.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati nikiunga mkono hoja hii ambayo itasaidia kupata fedha kwa ajili ya chakula, niombe sana kwamba kwa kweli hasa katika maeneo yote kwa sasa hali ya chakula ni mbaya katika Vijiji vyote. Kwa hiyo, chakula hiki kitakachonunuliwa na kugawanywa kisiende peke yake katika Vijiji vile ambavyo mwanzoni vilionekana kwamba vina matatizo na badala yake kipelekwe katika Vijiji vyote ambavyo kwa sasa kwa kweli havina chakula, hata vile Vijiji ambavyo vilionekana mwanzoni vina chakula hivi sasa havina chakula kwa sababu kwanza wametumia. Lakini vile vile wale ambao walikuwa

hawana wamekwenda kuhemea katika sehemu hizo na kufanya Vijiji hivyo visiwe na chakula. Kwa hiyo, kuna kila sababu kuona kwamba Vijiji hivi ambavyo havikupata mgao wa kwanza wa chakula naomba sasa vipewe umuhimu na visaidiwe kupewa chakula kama ambavyo Serikali imeahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la njaa katika Jimbo langu ingawa ni kweli kwamba uhaba wa mvua ilikuwa ni moja ya sababu hii ya tatizo la njaa, lakini kama nilivyosema awali, nataka nirudie tena kwa sababu ni jambo ambalo linaniuma na ni la kweli. Kwa upande wetu ukiacha suala la mvua, lakini ndege waharibifu wamechangia sana kwa sehemu kubwa sana kuharibu chakula ambacho kilipatikana ingawa kilikuwa kichache. Katika kikao cha Bajeti nilieleza hili na nataka nirudie tena kulieleza hili kwa sababu kila ninapotembea katika Vijiji vile ambavyo nimepita bado wananchi wanalalamika kwamba hawaoni jitihada ambayo Serikali inafanya katika kuangamiza ndege hao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli ndege ilikuja lakini ilichelewa. Sasa ombi langu ni kwamba, katika kuliangalia hili naomba Wizara inayohusika na hapa ni Wizara ya Kilimo na vile vile Wizara ya Maliasili, walishughulikia hili jambo la kuangamiza wale ndege *quelea quelea* na kasuku ili wananchi wetu angalau wapate hamasa ya kuendelea na kilimo. Hivi sasa wameanza kuvunjika moyo kwa sababu wanasema chakula tunalima lakini ndege wanatuharibia mazao yetu na jitihada ambayo Serikali inafanya inakuwa siyo ya kutosha. Kwa hiyo, naomba wasingoje mpaka mwezi Juni au Julai, hivi sasa ndege wale wapo, ukipita kule kwenye Tarafa ya Ihanja na Sipuka wale ndege wapo. Kwa hiyo, ni kazi ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa kutumia kitengo chake kile kinachohusika kiweze kupeleka ndege ili wananchi waondokane na tatizo hili, vinginevyo tutaendelea kuwakatisha tamaa wananchi wetu ambao wanajihusisha na suala hili la kilimo.

Mheshimiwa Spika, pia kwa upande wa Wizara ya Maliasili kumekuwapo na tatizo la ndege kasuku kwa maelezo kwamba kasuku wamepigwa marufuku hawawezi kuuawa au kuvunwa na tulihidiwa kwamba, Serikali ingeomba kibali kutoka kwenye Umoja wa Mataifa au kwenye *Institutions* zinazohusika ili kibali cha kuwavuna hawa ndege kipatikane. Naomba nikumbushe suala hilo na nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili au Serikali kwa ujumla, kuona kwamba kibali hicho kinapatikana kwa sababu kwanza huyu kasuku hata kumwangamiza kwa ndege ya kawaida inakuwa vigumu. Kasuku hapatikani kwa sababu anaondoka asubuhi mapema na kurudi usiku. Kwa hiyo, ndege ya kawaida haiwezi kupata nafasi ya kumwangamiza kwa sababu haiwezi kufanya kazi usiku kwa sababu itagonga miti na kuweza kuumiza wataalam wetu. Kwa hiyo, hapa naomba nikumbushe na nisisitize kwamba, Wizara ya Maliasili nayo iharakishe katika kuona kwamba kile kibali ambacho kinaombwa kinapatikana haraka iwezekanavyo.

Kwa upande wa maombi ya fedha kwa ajili ya umeme, mimi nayaunga mkono kama nilivyosema kwa asilimia mia moja. Naunga mkono kwa sababu pengine bado maeneo mengi hatujapata umeme ingawa pale Wilayani kuna umeme na baadhi ya Vijiji, lakini baadhi ya maeneo mengi bado hayana umeme. Siku zote nimewasilisha kilio changu hapa cha Tarafa moja ya Ihanja ambayo wamewekewa nguzo zimelala pale toka mwaka 1997. Zile nguzo zimewekwa lakini hazichimbiwi, wananchi wamepewa matumaini lakini hayatekelezwi. Kwa hiyo, wamekuwa wakijiuliza hivi tuna matatizo gani mpaka Serikali ituletee nguzo halafu haizichimbii? Kwa hiyo, matarajio yangu ni kwamba, fedha hizi ambazo wenzetu wa *TANESCO* wanapewa basi angalau wazingatie na kutekeleza baadhi ya miradi ambayo ilibuniwa.

Mheshimiwa Spika, kinachonisikitisha ni kwamba, inaonekana kwamba, *Net Group* baada ya kuingia wametekeleza na kudharau mipango ambayo ilikuwa imepangwa kabla wao hawajaja na hilo ni jambo la kusikitisha sana. Nilidhani kwamba, kazi ya kwanza ya *Net Group* ni kuheshimu Mikataba na miradi ambayo Serikali ilikuwa imejitengeneza ili itekeleze na mingine mipya inaweza kutekelezwa lakini kwa hali ilivyo sasa, kwa sababu Serikali iliahidi kupeleka umeme Ihanja toka mwaka 2002 na mpaka sasa mwaka 2004 haijapeleka, basi niwaombe sana Serikali na *TANESCO* na *Net Group* wenyewe waone kwamba wale wananchi wa Ihanja ambao wamekuwa na matatizo wapatiwe umeme.

Mheshimiwa Spika, dhana ya kwamba *management* za kutoka nje zinaweza kutusaidia sana inaanza kuwa *defeated* na *Net Group*. Kwa sababu toka wamefika, kwa kweli sijafika mahali nikafurahi, nikaona kwamba wamefanya kazi nzuri. Dar es Salaam kule na nchi nzima bado umeme unakatika ovyo ovyo kila siku, miradi ambayo ilikuwa imepangwa bado haijatekelezwa. Sasa hivi tunaambiwa Serikali

itoe ruzuku kwa ajili ya *TANESCO* kwa sababu hali ya fedha siyo nzuri. Sasa wamefanya nini hawa *Net Group* toka wamekuja? Kwa hiyo, ile dhana au *concept* ya kwamba eti ukipata *foreign management* kuja ku-*manage* hapa Tanzania tutafaidika, mimi nasema inakuwa *defeated*. Nashawishika kusema kwamba, kama hawa walikuwa na Mkataba wa miaka miwili basi ukiisha huu Mkataba tutafute mtu mwingine tuendele, hakuna haja ya kuongeza tena Mkataba mwingine baada ya miaka miwili kwa sababu hakuna ambacho mimi nakiona kwamba wamekifanya ambacho ni kitu kipya kinachoweza kutusaidia. Kwa kweli napenda nishawishi wenzangu kama suala hilo tungeletewa sisi hapa tuongeze Mkataba wa *Net Group*, nasema hakuna haja ya kuongeza kwa sababu hatujafaidika chochote na utaratibu huu wa *Net Group*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hii Wizara ya Elimu naunga mkono kwamba waongezewe fedha kwa sababu kwa kweli Wizara hii imefanya kazi nzuri chini ya Mheshimiwa Mungai na nina hakika wakipewa uwezo au wakiwezesha watafanya kazi nzuri zaidi. Ombi langu ni moja tu kwamba, yapo malalamiko au maombi kutoka kwa wananchi kwamba ile ada ya shilingi 20,000/= ya mitihani kwa kweli inakwamisha baadhi ya wazazi. Wengi wanashindwa kulipa shilingi 40,000/= kwa ajili ya ada ya shule, sasa mtoto anapofika *form four* unamwambia mzazi aongeze tena shilingi 20,000/=, kwa kweli wengi wanapata shida. Mimi nadhani kazi nzuri imefanywa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu wa Serikali yetu ya Awamu ya Tatu katika kuboresha elimu, hili nalo ilianguka. Pengine katika mpango ambao Mheshimiwa Waziri wa Elimu anakusudia kuuleta katika bajeti ya mwaka 2004/2005, hebu waanguka hii shilingi 20,000/= ni hela nyingi, lakini kwa kweli tunadhani kuwa Serikali kama ipo *serious* katika kuwatatulia wananchi wake kero kama ambavyo Serikali ya CCM ya Awamu ya Tatu imefanya, hili nalo nadhani linaweza kuondoka. Kwa hiyo, niombe sana hizi Sh. 20,000/= za ada ya mitihani, Serikali itafute njia ambazo inaweza ikafanya ili iweze kuziondoa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niseme na mimi tu kwamba, ingawa wenzangu wawili wamesema kwamba inasikitisha kuona kwamba baadhi ya waajiri wanakata fedha za wafanyakazi wao lakini hawapeleki na jambo hili linazungumzwa na Serikali wanakubali hapa kwamba moja ya upungufu ni kwamba waajiri wanakata fedha lakini hawapeleki. Sasa Serikali kama inalalamika sisi wengine tufanye namna gani? Serikali inashindwa nini kuchukua hatua thabiti kwa waajiri wale ambao wanakata fedha za wananchi au wafanyakazi wao halafu hawapeleki kiasi kwamba mfanyakazi anapostaafu wakati angetegemea kupata mafao yake ya kustaafu mapema iwezekanavyo ili akayakabili maisha mapya anaanza kukaa miezi sita au miaka mitatu kuongelea Serikali tena itafute njia nyingine za kupeleka fedha.

Mheshimiwa Spika, mfano wa *NASACO* juzi unasikitisha. Tulipozungumza habari ya *NASACO* hapa tulieleza mwanzo mpaka mwisho. Sasa mfano umesikitisha, njoo kesho, nenda kwa Waziri wa Fedha, sijui nenda kwa Waziri gani, nenda *PPF* na kadhalika. Kwa hiyo, ningomba kwa kweli Serikali iwe *serious*. Iwe *serious* kwa maana ya kwamba, kama kweli waajiri wakorofi wanaonekana wanakata fedha za watu na hawaziwasilishi kiasi kwamba wafanyakazi husika wanapata tabu wanapostaafu, nadhani Serikali ina uwezo kabisa wa kuwachukulia hatua thabiti waajiri hao na siyo kuwalea lea kama inavyoonekana ili kupunguza taathira kwa upande wa wafanyakazi wale ambao wanastaafu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**MHE. THOMAS S. NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili nichangie kidogo hoja ya Waziri wa Fedha. Kwanza, nampongeza Waziri wa Fedha na wataalam walio chini yake. Pili niwapongeze *TRA* na kiongozi wao kwa kazi nzuri wanayofanya, hata leo tumeweza kufanya *power load shading* kwa njia ya fedha badala ya *physical* ambayo ingetuletea upotevu wa mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa maeneo yote na pekee kama eneo la ndege. Wapo ambao wanatazama kununua ndege ya Serikali kama vile inanunuliwa ndege ya Rais Mkapa. Rais Mkapa angekuwa anatamani ndege mpya ya kupanda asingenunua wakati anapoondoka, angenunua mapema ili aipande sawasawa. Kwa hiyo, ananunua ndege ya Serikali, Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba tulitazame hivyo na busara ndivyo inavyoongoza. (Makofi)

Wala siyo jambo la kiuchumi kwa nchi hii kununua ndege au kulipia njaa. Ni vitu ambavyo vimetokea, vinafanywa na vinakwisha. Tatizo hapa ni umeme. Umeme ni tatizo kubwa. Tatizo kubwa linalotakiwa litazamwe kwa sura ambayo hivi tunafanya nini. Nchi yetu tangu miaka ya 90 tumekuwa hatuna umeme wa kutosha kwa sababu tunategemea umeme wa maji. Nchi yetu ina uwezo kwa mitambo iliyofungwa kuzalisha megawatt 850. Lakini kinachozalishwa tangu miaka ya 90 mpaka leo ni chini ya asilimia hamsini. Wote tunaona, Serikali hiyo hiyo imeagiza zitafutwe njia tofauti za uhakika za kuzalisha umeme nchini. Rais Mkapa alipotoa salaam za mwaka mpya alieleza ni vizuri wataalam wapate njia tofauti ya kupata umeme ili tuweze kuendelea. Tanzania na ninyi Waheshimiwa Wabunge, Julai, 2001 tuliitwa kushuhudia kuwekwa saina Mkataba wa Makubaliano wa Makusudio ili mwishoni mwa 2003 ujenzi wa umeme wa makaa ya Mchuchuma uanze. Haya yote yanafanywa lakini kwenye vitendo ni maneno matupu. Hivi Wizara hii inamdanganya nani? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi naishangaa sana Serikali. Wizara hii ya Nishati na Madini wao wenyewe na Serikali waliagiza *NDC* iongoze, namna ya kumpata mwekezaji na isimamie namna gani Tanzania itapata faida katika mradi wa Mchuchuma. Nini kinatokea? Wizara ya Nishati ikaajiri wataalam wanaitwa *EKARS*, *EKARS* nina uhakika Serikali inajua ni watu wa rushwa hawa. Mimi nasema kwa mifano, nenda Lesotho, kuna kesi hivi sasa ambayo wamehukumiwa na kutozwa faini kwa sababu ya rushwa. *EKARS wame-appeal* mpaka *Court of Appeal*, Lesotho bado wameshindwa na wameadhibiwa. Hii ndiyo rekodi ya chombo kinachotumika na Serikali. Hazina tulizonazo Tanzania za Mkaa wa mawe ni kutupatia umeme mwingi wa kutosha hata kuenea nchi za jirani zote kwa gharama ndogo. Lingine la kushangaza, umeme wa Mchuchuma ni mradi ambao mwekezaji anagharamia. Umeme wa *Songo Songo Gas* ambao Wizara ya Nishati inaukumbatia, ni mradi ambao Serikali, Watanzania tunakopa. Endapo haukwenda vizuri hasara ni kwetu ya mkopo huo. Umeme wa Mchuchuma kama mambo yakiharibika hasara ni kwa mwekezaji. (Makofi)

La pili, umeme wa *IPTL*, *capacity charge* tunayolipa tayari shilingi bilioni 3 na zaidi. Umeme wa Songo Gesi ukianza ni shilingi bilioni 6 pengine na zaidi. Umeme wa Mchuchuma ni kati ya shilingi bilioni 3 na bilioni 4.5 kwa kipindi hicho hicho cha mwezi na kila nililosema ni mwezi mmoja mmoja. Lakini umeme tunaolipia shilingi bilioni 3 hivi sasa ni megawati 100. Umeme wa Songo Gesi ni megawati 150, umeme wa Mchuchuma ni megawati 400.

Kwa hali ya sasa wakati wanaotumia umeme Tanzania hawafiki *percent 10*, tunahitaji kama megawati 500 hivi. Ni dhahiri Mchuchuma ingeanza kufanya kazi, mitambo yote ya mafuta nchini ingefungwa na mitambo ya maji iliyo mingi ingekuwa *standby*. Maji mengi tungeanza kuyaona yanaelekezwa kwenye kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini Waheshimiwa wa Nishati na Madini, hayo yote hawayasikii, wanachotaka ni umeme wa maji, umeme wa maji sijui wapi? Huku dunia inatangaza maji yanatoweka duniani. Mimi nilidhani Serikali ina uwezo mkubwa wa kujua mambo kuliko mimi. Sasa hapa kitendawili kinachotokea mimi sikielewi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala la umeme mimi nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu yeye ameleta busara ya kufanya *load shedding* kwa kuchukua fedha ambazo angetumia labda kwa maji au nini au nini ili kuhani mapato yake ya mwakani yaendeleo kuwepo na kukua. Angekuwa hana busara akakubali wafanye *physical load shedding*, hasara ingetufikia ya kutisha. Lakini hivi Serikali inafanya nini? Hivi kwa nini hatutaki kuhakikisha tunapata umeme wa makaa, nini linatokea?

Hivi sasa hii Bajeti tunayopitisha Bunge hili linawambia *the fuel giant* kwamba tuko tayari kuwapa bilioni hizo hawataachia mnajua tabia, hawa watafanya nini? Hawataachia! Watahakikisha umeme wa Mchuchuma hauji na dhahiri bora mradi wa umeme wa Mchuchuma hauji, tutaendelea kugharamika kama tunavyogharamika sasa na itazidi. Umeme wa Songo Gesi, Serikali kila ikisimama hapa inaongelea Songo Gesi, Songo Gesi watoe mfano wa nchi duniani iliyoendelea kwa kutumia nishati ya uhakika kutokana na gesi, haya ni mambo ya kusadikika, nyimbo ya Shabaan Robert ya wapi? Ni nini kinatokea mpaka Serikali inakwepa mambo yaliyo wazi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi jana jioni nilishangazwa sana ninaporudi nyumbani kwangu nilimkuta rafiki yangu mmoja nje, sina uhakika alikuwa na maudhui gani, amelewa au mzima au nini, amelala mlangoni kwa geti lake! Nikamwambia: "Why are you sleeping here?" akasema: "My dog is so fears I can't go in," nikamwuliza kwa mshangao: "Mbwa wako?" Ndiyo. Nilimwacha hapo hapo. Siwezi kumsaidia mtu wa namna hiyo. Leo Serikali, Katibu Mkuu, kila ukiongea na Mheshimiwa Daniel Yona, utaambiwa mtaalamu huyu, mtaalamu huyu, *how comes, my own dogs stops me from entering in the house?* (Makofi/Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuko kwenye mchezo wa kuchezea shilingi chooni, ndiyo tunachofanya hapa na kwa kweli suala la umeme limefanyiwa mzaha sasa karibu miaka 20. Jana hapa tumepata semina kama kumbukumbu yangu haikosei namna ya kuunda vyombo au chombo cha kupeleka umeme vijijini.

Mimi wakati wote nilikuwa nawashangaa, hivi hawa watu wana akili timamu hawa walioleta hii semina! Hivi mnaleta semina ya namna ya kupeleka umeme vijijini ambao haupo. Hivi mkiunda hicho chombo kitapeleka nini huko vijijini kitapeleka hewa? (Makofi/Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Tulikuwa tunapokea posho bwana!

**MHE. THOMAS S. NYIMBO:** Posho ni suala lingine si juu yangu mimi. Lakini niliwashangaa sana hekima gani imewatuma tarehe ya jana wakati Serikali inaomba kulipia ziada umeme kutokana na kuwa umeme hautoshi. Lakini tunaanza kuhangaika namna gani tutapata chombo cha kusimamia *Rural Electricity* kwa umeme upi? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, mimi kwa upande wangu naliomba sana Bunge hili, bahati mbaya nataka kumwomba Mheshimiwa Spika, Bunge hili liweke *Select Committee* ikaisaidie Serikali kufanya kazi, lakini pia Kanuni zetu nazo zina matatizo. Kanuni zetu nazo zina matatizo siyo Spika, kanuni.

Huku Kanuni ya 104 inataka tufanye hivyo, ukirudi kwenye Kanuni 77 inasema fanyeni hivyo kama hamtaongeza gharama kwa Serikali. Sasa hiyo maana yake nini?

Kwa hiyo, mimi ninalosema Waheshimiwa Wabunge, wengi hapa wamechangia kwamba wanafikiri tukiwapa fedha tutapata umeme vijijini siyo kweli. Hizi fedha tunapeleka bado umeme utakuwa ni ule kidogo, na jibu la kupata umeme vijijini ni kupata umeme ambao ni wa bei nafuu kutokana na mkaa na iko mifano ya nchi nyingi duniani zilifanikiwa hivyo. Serikali kila siku inatwambia nia wanayo na malengo wanayo. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, namuunga mkono Mheshimiwa Waziri wa Fedha, aendelee na hoja yake. Ahsante sana. (Makofi)

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Bajeti ya Nyongeza ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa mipango wataalamu wanasema unapokuwa na mpango wako ni lazima hufuatilie kwa makini na wewe mwenyewe uweze kuwa *dynamic* na *responsive* pale unapooni kuna haja ya kufanya hivyo. Kwa hiyo, napenda sana niipongeze Serikali na Wizara ya Fedha kwa kuwa *dynamic* na *responsive* na Bajeti yake ambayo tuliipitisha mwaka jana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, moja ya sababu za kuomba fedha za ziada ambazo hazikuwa kwenye Bajeti ni ili kukubaliana na tatizo la njaa na kwa kweli tatizo la njaa katika nchi yetu ni kubwa sana na wananchi wetu wamefikia hatua ya kuhangaika.

Kwa hiyo, napenda niungane mkono kwa kweli hoja hii asilimia mia kwa mia. Lakini fedha hizo tutakapokuwa tumezipitisha basi zipatikane haraka, chakula kinunuliwe na kisambazwe nchini ili kupunguza bei kubwa ya chakula hasa nafaka zilizopo katika Wilaya zetu.



Mheshimiwa Spika, watu wengi huwa wanadhani kwamba tungeweza kuepukana na njaa kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji. Lakini hoja hii inapotajwa wakati mwingine watu wanasahau kwamba maji yanatoka kwenye mvua na kama mvua haikunyeshwa basi hakuna maji ya kunyweshea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama tukitaka umwagiliaji huo unaosemwa kwa hoja hiyo inatubidi tutumie maji ya mito mikubwa na mito hiyo ndiyo hiyo tunatumia kuzalisha umeme.

Napenda hapa niwaunge mkono wasemaji waliopita ambao wameshauri kwamba wakati umefika sasa tufikirie upya kipaumbele cha kutumia maji, kati ya uzalishaji umeme, kunywa na kuzalishia chakula kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, ukizalisha umeme wa maji unaelewa wazi tangu mwanzo kwamba kunapokuwa na ukame, maji yanapungua na umeme huo utapungua, na unaelewa kabisa kwamba mvua inapoonyesha basi utapata umeme wa kutosha. Sasa umeme huu huwezi kuusimamia.

Kwa hiyo, ni vizuri tuanze kuzalisha umeme kutokana na njia nyingine na hizo zimetajwa kwa uzuri kabisa mpaka katika maeneo ambako utazalishwa. Lakini tunatakiwa tuongeze uzalishaji wa umeme kutoka kwenye makaa ya mawe na kutoka kwenye gesi ili tupunguze kutegemea maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine takwimu zinapotolewa tunashindwa kuzitafsiri sawasawa. Sisi Watanzania tunazalisha umeme megawati 500, wakati *South Africa* inazalisha megawati 38,000. Sasa umeme wetu wote wa nchi nzima ni kama *plant* moja ya kule *South Africa* na ukweli ni kwamba tayari mahitaji yetu ya umeme ni megawati 600.

Kwa hiyo, hata kama tunataka wawekezaji kwa kweli hatuna umeme wa kuwapa na kwa hiyo, ni muhimu sana tufikirie kuzalisha umeme kutoka kwenye miradi hii hasa mradi wa Mchuchuma na tufanye hivyo haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na Bajeti hii ya nyongeza kwamba haina kodi mpya. Tungekuwa na kodi mpya tungekuwa tunayumba hapa, maana tulifuta hata kodi ya kichwa. Kwa hiyo, mimi nimefurahi sana kwa *consistency* hii ya kuwa na Bajeti ya Nyongeza, lakini inatumia mapato ambayo yapo. Napenda niwapongeze Wizara ya Fedha kwa ufundi huu wa kutengeneza Bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini sitasahau suala ambalo nililitaja kidogo hapa Jumamosi iliyopita wakati wa semina kwamba tuliwaahidi wakulima wa Kahawa kwamba hatuwezi kuwalipa fedha ya *STABEX* moja kwa moja, lakini tutawatengenezea barabara zao vijijini.

Sasa mwanzoni tuliambiwa utaratibu kwamba fedha hizi zitakuwa Wizara ya Kilimo na Chakula na kwamba Wilaya ambazo zinahitaji fedha hizi zitaomba, basi tukaenda tukaomba, sasa tukifuatilia maombi yetu tunaambiwa fedha ziko Wizara ya Ujenzi na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi jizi ametueleza hapa kwamba hakuna fedha hizo kwenye Wizara ya Ujenzi.

Nikamwuliza rafiki yangu Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa sababu ni mtani wangu, nikasema hebu nimwulize mtani wangu, zile fedha ziko wapi eeh? Akasema fedha zile ziko Wizara ya Kilimo na Chakula. Sasa tunataka tueleze waziwazi kabisa hapa kwamba fedha hiyo iko wapi? Na tunataka tukiondoka hapa tukawaeleze wakulima itakuja lini ili barabara zitengenezwe na masika yakija tuanze kupanda Kahawa mpya. Hili lazima mtueleze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ningependa kuipongeza sana Bajeti hii ya nyongeza kwa kuwa *responsive* kufuatia idadi kubwa ya watoto ambao wamefaulu mtihani wa darasa la saba. Kama ambavyo nimezoa hapa kila Kikao nimekuwa napiga debe sana kuhusu kusomesha watoto na kwamba nchi ambayo haisomeshi watoto wake haina *future* na sisi tunasomesha watoto wachache sana katika kiwango cha elimu ya sekondari ukilinganisha na nchi zingine za dunia. Ukitulinganisha na nchi za dunia unapata aibu kwa sababu tunakuwa wa mwisho kusomesha watoto katika kiwango cha elimu ya sekondari.

Kwa hiyo, kwa kweli safari hii tumefurahishwa na hatua ya kwanza watoto wamefaulu wengi, hii inaonyesha kwamba kiwango cha elimu kinapanda. Lakini bado watoto ambao tunapeleka katika elimu ya sekondari ni wachache. Kwa hiyo, kama tungeweza kuwapeleka wote hawa karibu 144,000 mimi ningekuwa mtu mwenye furaha kubwa sana. Krismasi yangu ningeleleta mapema.

Kwa hiyo, nimefurahishwa sana kwamba tumeweka shilingi bilioni 2 ili kuweza kuongeza idadi ya watoto ambao wataingia katika elimu ya sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupongeza ninadhani kiwango kilichopangwa hakitoshi. Kwa hiyo, ninapenda nitoe rai kwamba mwezi Juni tutakapokuwa tunajadili Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na tutapokuwa tunapitisha Mpango mpya wa Kupanua na Kuendeleza Elimu ya Sekondari basi kutakuwa na nyongeza ambayo inaridhisha katika kuongeza kiwango cha watoto wetu wanaosoma katika elimu ya sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeza Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kupunguza masharti ya kuandikisha shule mpya za sekondari. Hii ni hatua kubwa ninajua kwamba ukipunguza masharti unahatarisha kiwango au thamani ya elimu. Lakini katika hali tuliyonayo sasa ni vizuri tukarahisisha masharti ya kuziandikisha hizi shule kama Wizara ilivyofanya ili kuwapa motisha wakulima waweze kuanzisha shule mpya na wazikanzanie kwa kiwango chao walichonacho.

Naiomba Serikali ifikirie kutoa ruzuku zaidi kwa wakulima hasa wale wa vijijini wanaojenga shule mpya za sekondari. Wawasaidie kununua mabati, wawasaidie kununua saruji na wawape vifaa vile ambavyo haviwezi kuzalishwa kule vijijini. Ujenzi wa shule za sekondari una matatizo makubwa kwa sababu ya gharama kubwa ya vifaa vya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunategemea kwamba baadaye mwaka huu tutaweza kupitisha bajeti ambayo itaweza kuwapa wananchi wanaojenga shule mpya za sekondari afueni hii ili shule ziongezeke na watoto wetu wengi waweze kupata elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na napenda niseme wazi kwamba ninaunga mkono nyongeza hii ya Bajeti asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake kwa Bajeti walivyotuletea na taarifa ambazo pia wametuletea. Kama alivyosema Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuna maeneo tunayaunga mkono kutokana na umuhimu wake pamoja na kwamba tunakataa baadhi ya sababu na maeneo mengine tumeyakataa.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa niongelee kwa kirefu kidogo suala la chakula. Katika suala la chakula mimi nadhania hatujawa bado na makini. Nina taarifa kutoka Serikalini zinaonyesha hali ilivyo mbaya. Lakini vilevile tuna taarifa za *FAO* ambazo zinaonyesha kwamba hali bado ni mbaya sana, iko Mikoa 17 ambayo hali yake ni mbaya na Arusha inatajwa kuwa mojawapo, na tathmini yetu bado nadhani haijawa makini. Tungekuwa na tathmini makini shilingi bilioni 10 siyo fedha za kutengewa kwa tatizo ambalo dunia nzima linazungumziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianzie na hilo la tathmini ni juzi tu tarehe 20 Januari, 2004 kama alivyosema Mheshimiwa Waziri William Lukuvi, walipita hao watu wanaofanya tathmini kule Wilayani kwangu, walipita watu wawili, wamekaa siku moja wamefika katika vijiji vitatu na hao ndiyo wanatoa tathmini ya Wilaya nzima. Mimi ningependa huu mtindo wa kutoa tathmini za namna hii ufike mwisho na tathmini sahihi zifanywe na kwa wakati unaofaa, vinginevyo watu wetu wataendelea kuathirika. Waliofika watu wawili mmoja ni mzungu na mwingine ni Mwafrika. Sasa mimi sijui kwanza hata *attitudes* za watu wetu kama wanazifahamu na ndiyo tatizo linaanzia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe labda takwimu chache tu ambazo zimepata kutoka Serikalini katika taarifa ya mwezi Julai wametoa mahesabu ya watu ambao wameathirika katika nchi nzima. Natoa mfano,

Karatu walitoa watu 24,000 tu ambapo wakati ule walisema ni asilimia 12, lakini wakati huo kwamba njaa itakuwepo kwa miezi mitatu tu.

Mimi simjui huyu mtu ni mtu wa aina gani anayesema njaa ya Karatu inanzia mwezi Oktoba hadi Desemba, mimi sijui ni wapi wanapata kwamba hata mvua za vuli zingenyeshwa mwezi Desemba tungevuna sijawahi kuona hata moja tangu nimezaliwa leo nina miaka 50 kwamba Karatu tumevuna katika miezi mitatu. Kwa sababu tunaanza kupanda kwa kawaida mwishoni mwa mwezi wa Novemba na tunavuna mwanzoni mwa mwezi Machi au katikati ya Machi.

Sasa hawa tathmini wanayofanya wanaipata wapi hii tathmini na hii si Karatu tu. Waheshimiwa Wabunge sijui kama wanazipata hizi takwimu, lakini ni vizuri wazitafute. Huko Manyara wanasema ni miezi minne mwezi Oktoba hadi mwezi Januari ninapafahamu na kwenyewe sijaona hata siku moja kama wamevuna mwezi Januari. Labda niende Mkoa mmoja wa ajabu tu, tuchukue Mtwara, Mtwara wamesema wanavuna mwezi Oktoba mpaka mwezi Desemba, mimi sijawahi kuona labda Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara asimame hapa na aseme kwamba huwa wanavuna mwezi Desemba. Nimefika huko nimeuliza wakaniambia hawavuni mwezi Desemba. Sasa hivi taarifa zinatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri tuna tatizo kubwa kabisa kuhusu aina na namna tathmini zinavyofanyika. Nimekwishatoa ombi hapa katika Bunge hili kwamba takwimu hizi ni vyema zipitishwe katika Baraza la Mawaziri ambapo Waheshimiwa Wabunge wanashiriki na taarifa hizi zipigiwe kura ikiwa ni lazima kule ndani, lakini zinatoka tu hatujui zinatoka wapi? Ukiuliza DED hazijui, kuna Kamati zinaitwa ni Kamati za Maafa zenyewe haziko Kisheria, lakini wananchi wanaendelea kuumia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kabisa tatizo hili ni lazima liangaliwe na tufike mwisho wa kuwa na tathmini na takwimu ambazo hazisaidii watu wetu. Isitoshe katika tathmini ile ya mwezi Julai, kuna taarifa ambazo kidogo zinatia chungu. Taarifa ya kwanza tuliyoletewa ni kwamba mahitaji ya chakula katika Wilaya nyingi, Karatu walisema ni tani 724, tukapewa tani 146 tukifikiri tuna zaidi ya tani 500 zilizobaki, zote zimeyeyuka, hatujui zimekwenda wapi na wala hakuna taarifa. Arumeru walikuwa na tani 1,023 walipata tani 206 zilizobaki zote zimeyeyuka, Masasi mahitaji yalikuwa tani 1,914, wakapata tani 600 kama walichukua kuna Wilaya kumi na kitu hawakuchukua, lakini nafikiri hawa walichukua.

Mheshimiwa Spika, sasa tunajiuliza kwamba kama kuna utaratibu na suala hili tulilijua. Labda niseme toka mwanzo kwamba ndiyo maana sisi tunasema tatizo la msingi ni mipango. Kwa yote ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha leo anayaombea fedha, tungeomba itazamwe Hansard ya mwaka jana wakati wa Kikao cha Bajeti haya yote tuliyasema sisi, tukaonwa kwamba sijui ni watu wa aina gani, tulionekana ni wa ajabu.

Lakini leo tuko hapa hapa na wale wenzangu wanaopenda kutukashifu tu hapa ningependa wasome. Kwa sababu tatizo la msingi ni mipango. Watoto wanapoingia *form one* huanzi kuwajua leo, ulipaswa kuwajua wanapoingia darasa la saba mwanzo wa mwaka. Utakuwa mtu wa ajabu sana kama hujui kwamba watoto wako wanamaliza darasa la saba na wanahitaji kwenda *form one*, ni mtu wa ajabu.

Hata Waheshimiwa Wabunge, ambao wanasema kwamba sisi tunakuwa wa ajabu wao ni wa ajabu zaidi. Ni wa ajabu kabisa kwa sababu mwezi Julai, unafanya tathmini, mwezi Januari hujui watu wako wana njaa kiasi gani na mvua hizo unazona! (Makofi)

Karatu mpaka leo haijanyesha mvua tumepanda mbegu mara tatu na kila wakati zinakauka, tumepata mbegu hata kwa njia zetu tunawashukuru sana ndugu zetu wa CRS wametusaikia vijiji 18 kuliko vile hata vya Serikali, lakini yote yamekauka.

Sasa hii ni hali ambayo inatakiwa iwe monitored kila wakati kwa kutumia vyombo vilivyoko pale pale Wilayani na vyombo hivi havitumiki kwa sababu hakuna sheria inayosimamia hii. Tunasema tumkabidhi DC sawa, mimi sina tatizo na kumkabidhi DC, lakini basi vipite mahali ambapo wananchi wote watashirikishwa, Waheshimiwa Wabunge watashirikishwa, Madiwani watashirikishwa na hali halisi iweze kuonekana.

Mimi naomba suala la shilingi bilioni 10 kwa ajili ya chakula kwa kweli itakuwa ni kichekesho kwa sababu hali bado ni mbaya katika eneo kubwa na ningependa Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili kama Tanzania tutabaki kuwa na uzito wa kuangalia hali ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba mapendekezo yangu katika hili niyarudie yale niliyokwisha kuyasema tungependa Kamati za njaa ziwe za Kisheria na ile sera tuliyoambiwa kila wakati iletwe Bungeni na kama imeshapitishwa tuone ili sheria iweze kurekebisha inavyotakiwa ili kuvipa vijiji vilevile mamlaka ya kuweza kufanya tathmini kwa kutumia wataalamu walioko vijijini. Tathmini ianze kule kule vijijini, hii habari ya mtu mmoja kuja ametumia mamilioni ya fedha, halafu anafika mahali anaweka tathmini ya kichwani kwake mimi nafikiri haitufikishi mahali.

Tungefikiri vilevile kwamba tunahitaji sasa tufike mahali, kama tumeshindwa kuwapata wawekezaji kwenye kilimo cha kisasa basi Serikali ingetenga fedha za kutosha tutangaze hata *tender* tuwape watu hizi fedha bilioni 10 tutapata chakula cha kutosha kuliko kuomba omba kila siku ambayo ni aibu kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ningesema tu kwamba Mheshimiwa Waziri katika tathmini uliyonayo nimepewa vijiji 12 tu na hivi vijiji 12 havifiki hata nusu ya vijiji ambavyo vina njaa. Ukienda katika vijiji kama Qaru, Qurus, Bashay, Changarawe, sitaki kuvitaja *list* ni ndefu vyote vina njaa, lakini vimeachwa vingine kutokana na mtu ambaye amefanya tathmini isiyo sahihi. Tuna vijiji zaidi 22 lakini Serikali katika *list* yake ina vijiji 12, tutawafanya nini hao watu ambao hawapo katika list hiyo.

Katika Ofisi ya Waziri Mkuu kuna tathmini iliyofanywa mwaka 1998, Ofisi ya Waziri Mkuu imetuma watu wamefanya tathmini katika eneo linaloitwa Mbulumbu na imesema kwamba eneo hilo linazalisha na kwa macho kweli linaonekana linazalisha sana, hata mwaka jana lilizalisha. Lakini asilimia 70 ya watu wa eneo hilo wote ni matajiri na asilimia 30 hawana kitu hata kidogo, sasa tuwafanye nini hao? Mheshimiwa Waziri ningependa yaangaliwe kwa undani kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kidogo juu ya ndege ya Serikali, tutumie jina la ndege ya Serikali au ndege ya Rais ni kitu kile kile kwa sababu ile ndege ya Rais inatumia Serikali. Lakini ningependa kutoa tahadhari kwa wenzangu wanaopenda kuzungumza bila kufanya utafiti. Waheshimiwa Wabunge kazi yao ya kwanza ni kuidhibiti na kuisimamia Serikali si kupewa taarifa tu na Serikali. Tungependa kuwaambia kwamba taarifa hizi zinapatikana siku hizi si lazima upate kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wakifika Bungeni kazi yao ya kwanza ni kuhakikisha kama alichosema Mheshimiwa Waziri ni sahihi au si sahihi. Tuna taarifa hapa ambayo inatoka *Global Security* na mimi sitaki mnilipe nawapa bure. Ndege ya Serikali ambayo Mheshimiwa Waziri ametoa taarifa hapa inasemekana *the contract includes a firm, fixed price, ten year contract logistic* ambayo bei yake ni *18 million dollars*. Hii taarifa ni ya jana kutoka *Internet* ya tarehe 15 Februari, 2004.

Kwa hiyo, hakuna cha kutwambia kwamba hatujui. Kama unataka zile *additional* ikiwepo *training*, ikiwepo hiyo aliyosema ni ya hospitali sijui nini? Ni *up to 26, milioni US Dollars. 26 millions US dollars* ambazo ni bilioni 26. Sasa sisi tunazungumzia bilioni 46 tunataka Mheshimiwa Waziri atupe taarifa sahihi na hii kazi ndiyo ya Bunge hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini si hilo tu cha ajabu Waheshimiwa Wabunge wanatakiwa kujua kwamba hii ndege ndiyo kwanza inatengenezwa. Ni ndege saba tu ndiyo zinatengenezwa, zitakuwa tayari Septemba. Katika ndege saba hizo *test* ya kwanza imefanyika mwezi Desemba, 2002. *Test* ya kwanza ime-*fly* kwa masaa matano tu na dakika moja.

Kwa hiyo, tunanunua ndege mpya ambayo hatuna hata uhakika nayo. Ndege hiyo imetengenezwa kwa ajili ya wakubwa ambayo inatoka New York inakwenda Tokyo kwa saa 14 1/2. Ndege hiyo inawekwa hata kwa Ulaya, imetengenezwa wa watu wachache na moja ni Jeshi la Israel. Na hii moja inawekwa Stockholm kwa ajili ya kukodisha kwa watu wakubwa kwa sababu watu wadogo wa kawaida si rahisi kui-*afford* kwa sababu ndege inatoka *non stop*.

Sisi Tanzania hatutaki ndege inayotoka *non stop* New York kwenda Japan, tunataka ndege inayotoka Dar es Salaam kwenda Kigoma, Rukwa, Lindi, Nanyumbu, Karatu na sijui wapi. Hizi ndizo ndege tunazotaka tutumie fedha za Tanzania. Lakini tunatumia ndege kwa bilioni 40. Rais wetu au Serikali yetu inakwenda Ulaya mara ngapi. Tokyo tunakwenda mara ngapi. Bilioni 40 badala ya kupeleka kwenye chakula tunapeleka kwenye ndege.

Mheshimiwa Spika, tungefikiri tuwe makini zaidi na Waheshimiwa Wabunge wafanye utafiti ndio waweze kuidhibiti Serikali vizuri iwezekanavyo. Ndege hii tunavyoambiwa sisi inaruka kwa zaidi ya kilomita 12,500 *non stop* na inabeba watu 18 tu. Tena hao 18 ni kama utaipanua lakini kuna *design* yake imewekwa hapa ukitumia *design* hii unaweza kubeba watu 14 tu. Tunanunua shilingi bilioni 40 ndege ya watu 14 tu ambapo tuliyokuwa nayo ilikuwa inabeba mpaka watu 40 na ilikuwa inafanya kazi kusaidia hata usafirishaji.

Waheshimiwa Wabunge, tuwe makini, tutetee maslahi ya nchi. Ie ndege ya zamani tuliyosema kwamba ni mbovu inakodishwa sasa hivi kwa *Eagle Air*. Kama ni mbovu je, ni nzuri ibebe wananchi wa Tanzania roho zao ni ndogo zaidi kuliko ya watu wa Serikali. Ni vyema basi tukafanya utafiti tukajua haya. Kama ni mbovu basi ilitakiwa iwekwe chini na kama ni mbovu iuzwe na kama ni mbovu basi isibebe watu lakini ndege inakodishwa inafanya biashara tunasema hii ndege imezeeka.

Tuna bei ya ndege duniani kote hapa na mtu anayetaka anaweza kuja kuiona. Kwenye Kampuni zote za dunia nzima bei zinatolewa hapa unaweza kununua ndege nzuri *executive jet* sio zaidi ya shilingi bilioni 14 pamoja na mpango wake wote wa miaka zaidi ya 10 wa matunzo na huduma zote zinazotakiwa, kwa nini tunachukua hiyo kubwa?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Kwanza kabisa napenda nimshukuru sana Waziri wa Fedha kwa uamuzi wake wa kutetea Taifa lisitetereke. Nilikuwa nafikiri kama Mawaziri wote wangesimama kidete kutetea Wizara zao kwa manufaa ya umma kama huyu alivyofanya tungekwenda mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninao wasiwasi kwamba shilingi bilioni 36 zitapunguzwa katika matumizi ya Wizara ili zisaidie shughuli hii. Sasa kama Wizara hizi zilileta maombi kwa ajili ya miradi sasa fedha hizi hazikutumika zikatwe ni kwamba tunasimama katika maendeleo yetu kungoja baadaye. Sasa hili mimi linanipa woga sana.

Mimi nadhani wale Mawaziri ambao fedha zao zitakatwa kwa kuwa zimekuwa idle mahali hazikutumika itabidi wafike Bungeni wajieleze kwa nini hawakuzitumia. Walitupotezea muda wetu kufikiria na kuona zingefaa fedha hizo zitumike, leo hazijatumika. Wawe na wajibu wa kujibu hoja hizi Bungeni ili tueleze.

Mheshimiwa Spika, la pili katika hilo inaonekana kwamba bado dunia hii tunaogopana. Imesemekana *PPF* tunaitolea fedha kwa sababu Mashirika yale hayakupeleka malipo ya wafanyakazi wake. Lakini Mashirika yaliyobinafsishwa hawa viongozi wanalipwa marupurupu yao na faida yote. Hivi Serikali haikuona hili. Leo tunawalipia watu binafsi wametuibia tunawalipa na ziada tena tualipie.

Hivi tunafanya nini na lengo letu ni nini. Hivi hata nikipewa na mimi Shirika kwa nini nilitunze vizuri kama ningeweza kulitafuna bado wakalipa watu wengine. Ndiyo hatari tunayoifanya nchi hii kwa sababu tumetoa mwanya watu wanadhulumu tu Serikali. Wanadhulumu umma bado hatuchukui hatua zozote za kuwafanya wajali na waogope ili watende kwa mujibu wa taratibu walizopewa. Lazima mtu akipewa kazi kwa kweli awajibike mafanikio yake. Kosa kubwa tunalolifanya ni kwamba hatutaki kuona matokeo ya fedha zinazotolewa kila mwaka. Hatutaki kuona hilo.

Hili nadhani iko haja ya kulifuatilia na kuona kwamba wale wote wanaokabidhiwa hizi fedha zinafanya kazi inayotakiwa. Hili ndilo tatizo linalotupa shida la *STABEX*. Sasa *STABEX* tumetetea Serikali kwa wananchi kwamba hizi fedha zinakuja, lakini sasa majibu tunayoyapata ni ya kuzunguka tu. Watu wanatupiana maswali hapa hivi hizi fedha ziko wapi, tuna njaa. Kama Serikali au Wizara hii ingeamua hata kuwalipa wakulima kidogo kidogo hizi fedha zingewasaidia kununua chakula kwenye njaa. Lakini sasa hizi fedha mpaka leo hazieleweki. Hadithi za Alfu Lela Ulela zinazidi kuendelea. Hatuwezi kwenda mbali na tutakwama, tena wazi wazi na kudhalilishwa na Mataifa mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala haya ya umeme, mimi nimebahatika kwenda Mchuchuma. Kwa kweli suala hili na tumezungumza na Waziri wa Nishati na Madini lakini tumekwenda pale hata Wizara yenyewe haijafika pale mahali wako kwenye makaratasi mezani. Hivi nchi hii itakwendaje, kutunga mambo mezani yatafanikisha wapi? Ndiyo tumeyaona kule.

Kuna mlima wa chuma Liganga kule na wataalamu wameshauri kama hizi shughuli mgodi wa mkaa ukifanikiwa basi ufanye na kazi ya kuyeyusha chuma. Lakini hata viongozi wa Wizara hawajafika kule na wao wanafuata hadith afadhali mimi nimefika nimewatangulia. Ni hadithi. Hivi tutakwenda wapi, tufanikiwa vipi. Tunazungumza masuala ya kununua mafuta wakati mkaa yako na pale hata huna haja ya kutafuta vifaa ni sepeto na kung'oa mkaa unakwenda unafanyia kazi. *(Makofi)*

Yaani mkaa umekuwa ndio vifusi vya barabara vijijini kule. Leo tunabaki tunazungushana hadithi hadithi tunakwenda wapi. Kwa kweli hatutafanya lolote wala hatutafanikiwa kitu. Lazima kwa kweli Waziri wa Nishati na Madini hili suala maadamu wako watu waliojitolea ni kuanza mradi, kwa kweli atupe jibu kwa nini anachelewesha au ana maslahi yoyote ya kutuhujumu sisi pale tuelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni daftari. Daftari hili mara nyingi tumesema kuwe na vitambulisho. Daftari bila vitambulisho halitasaidia kitu. Maana majitu yatakuja yatajiandikisha tu. Hujui limetokea wapi na nini linajiandikisha. Vitambulisho vitiliwe mkazo mapema. Watu tupate vitambulisho ndipo tuingie kwenye daftari hilo la kupiga kura.

Bila hilo hatutakwenda tutarudi tena hapa kupigiana kelele na Vyama vya Upinzani kulialia ambavyo kwa kweli itakuwa ni matatizo. Tupate vitambulisho pamoja na fedha zimetengwa vitambulisho vitangulie haraka na daftari lifuate ili kusiwe na udanganyifu wa kujiandikisha watu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho tumesema hapa kwamba jamani hii reli hii ndio ukombozi wetu. Reli hii ndiyo inayosafirisha ng'ombe kutoka Shinyanga au Mara huko kwenye ng'ombe wengi. Lakini na usafiri wa watu vile vile. Lakini watu wameona kama huo ni mradi wa kubabaisha tu. Sasa leo njaa hivi kweli kama tungekuwa tumeimarisha hii njia tungezungumza kwamba hapa kweli, tufikirie hata fedha za ziada za kupeleka chakula cha njaa.

Mimi nadhani liko tatizo mahali. Hili ndilo tulitafute tatizo limetoka wapi na ni la nani au ni upungufu wa mawazo. Tuliangalie hili suala kwa kweli ni jambo la kushangaza kabisa. Hii *TRC* ndiyo njia pekee huwezi ukasafirisha mizigo yote hii mpaka kule Shinyanga, Mara kwa malori mabasi hatuwezi. *TRC* ndiyo mahali pake.

Sasa hili mliloliweka mimi nakushukuru sana Waziri wa Fedha, nakushuru sijui kama uliwaomba na hawa wanaosaidia wengine walikusaidia, lakini nashukuru sana. Hili litupe funzo kwamba njia hii tupe kabisa kipaumbele kuhakikisha kwamba ni njia itakayotusaidia katika matatizo yetu yote. Lisiwe ni kwa ajili ya chakula cha njaa tu. Hata usafiri maendeleo ya jamii tuweke nguvu na ndio uwezo wetu na ndio heshima yetu.

Kwa kweli ni aibu kuwa na Shirika ambalo behewa linakwama Saranda halafu tunasema tuna matatizo, matatizo gani? Fedha ngapi zinapotea hapa hata za kwenda kusaidia hata hizi bilioni 2 naona ni kidogo sana.

Namwomba Waziri wa Fedha aangelie ziwe angalau tatu au nne zitusaidie angalau kukwamua tatizo hilo. Ni aibu sana watu wanashindwa kusafiri na chakula kishindwe kwenda na hapa mmesikia watu

wanakufa, wafe watu kwa sababu eti *TRC* haina uwezo wa kusafirisha kwa kweli tutakuwa ni wachawi badala ya kuwa watu wa kusaidia maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naunga mkono Muswada huu na ninaomba Waziri wa Fedha awe na nguvu ya kufuatilia fedha zote zinazopelekwa katika Wizara zote afuatilie na atutolee taarifa ni Wizara gani inayosuasua kutumia fedha vizuri au inatumia vibaya. Hii itatusaidia sana hata kwa Bajeti inayokuja na miradi hii itakayotumia fedha zake kwa njia ya Bajeti hii ya dharura basi iwekewe utaratibu katika Bajeti ijayo ili miradi ile isikwame ipate kuendelea.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru na naunga mkono. (*Makofi*)

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Kwanza napenda niseme kwamba naunga hoja mkono mia kwa mia. Ningependa tu nielezee kwamba sina matatizo na mambo mengi hasa ununuzi wa ndege, lakini nataka niongelee kuhusu mambo ya *TANESCO*, baadaye na njaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la *TANESCO* ni vyema wakapewa fedha lakini si vizuri wakapewa fedha tu halafu wakapewa kama ruzuku wangepewa fedha hizi halafu wakatakiwa wazirudishe baadaye kwa kutumia *sinking fund*. Walitakiwa hizi fedha wapewe hata tukisema tuwakopeshe kwa muda hata wa miaka 10 halafu wawe wanazilipa kidogo kidogo kwa kutumia *sinking fund*. Si vizuri kwa uchumi unaoendelea kama wetu sasa hivi watu wawe wanapata fedha za bure. Hii si sawa na nilifikiri kwamba Serikali ingewapa hizi fedha kama mkopo wa miaka 10.

Naelewa kabisa kwamba tunapoanza mzunguko wa mvua tuseme mwaka unaoishia 5, 6, 7, 8 na 9 huwa miaka mizuri sana na ina mvua nzuri. Kwa hiyo, wakati ule wangeweza wakalipa hili deni, kwa nini wapewe fedha za bure?

Mheshimiwa Spika, naomba hili lijariibu kufikiwa na Hazina na wapewe hizi fedha kama mkopo na wala sio fedha za bure. Kuhusu ununuzi wa ndege mimi naiunga mkono moja kwa moja na mambo mengine nayaunga mkono. Lakini nilitaka niongelee suala la njaa. Mtakumbuka hata wakati nachangia hapa kwenye Bajeti niliwatahadharisha kabisa kwamba njaa sio kitu cha kuchezea. Njaa ni hatari, ni kifo. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya njaa kwa kweli mimi naziona ni kidogo sana kulingana na ukubwa wa tatizo lilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninapakana na Jimbo la Kishapu. Jimbo la Kishapu ninapakana nao na Kata 4 ambazo ni Kizumbi, Ibadakuli, Kolandoto na Mwamalili. Katika uthamini wa chakula cha njaa ambao ulifanywa ovyo ovyo na Serikali wenzetu ambao ninapakana nao walipewa chakula na sasa hivi wanapata chakula kutoka *WFP* na wale wananchi wa Jimbo langu wanapoona wananchi wa Kishapu wanapewa chakula inaonekana kama mimi ni Mbunge *fake*.

Hivi kama Kishapu walikosa mvua ambao tunapakana nao mimi Jimbo la Shinyanga Mjini lilipata wapi mvua ya Mungu? Kwa hiyo, mimi naomba kabisa Serikali suala hili lazima walione namna gani wanaweza kulitatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Serikali ifanye upya tathmini kwa haraka zaidi tathmini ya njaa sasa hivi katika Jimbo langu wananchi wanahangaika kweli na nina hakika wengine wanakufa. Wanakula majani "kubitaa", kuna majani fulani wanatoa kama mboga, chakula hakitoshi.

Namwomba Mheshimiwa Benjamin Mkapa, suala la njaa. Najua ni mtu mahiri sana inawezekana watu wanamficha. Naomba kabisa kama inabidi aunde Kamati hata watu anaowaamini watathmini upya suala la njaa ni kubwa sana na ninaamini kabisa kwamba sisi hapa wananchi wametutuma. Tuko hapa tumekaa kwa niaba yao na kama kwa kweli hatuwezi kuwatetea, kwa kweli mimi naona kwamba tuko hapa kama *fake people*. Kwa kweli hali ya njaa ni kubwa sana hasa katika Jimbo langu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu linapakana na Kata zile za *pre-Urban* kwa kuwa mvua haijanyesha kwa muda mrefu kwetu karibu miaka mitatu mapato ya wananchi yamepotea hata unaposema kwamba niwapelekee lazima kije chakula cha bure. Mimi hapa niliomba tangu zamani nipewe chakula aina tatu cha kununua wenye fedha, halafu cha nguvu kazi wenye nguvu lakini fedha hawana halafu na chakula cha bure kabisa.

Mheshimiwa Spika, usisahau kama leo una bahati ya fedha wengine hawana kabisa ule uwezo. Katika jamii yetu tuna watu vilema, wengine vilema kwa ugonjwa. Tuna watu vilema kwa mambo mbalimbali halafu wengine ni wazee ambao hawana uwezo wa kuwa na fedha. Huu mtindo wa kusema kwamba tunapata chakula cha kwenda kununua hata shilingi 50/= wengine wanashindwa kukinunua na wanabaki pale wanahangaika.

Nilikuwa naomba kabisa kwamba suala la njaa tusiliwekee upuuzi au masihara. Kwa kweli suala la njaa ni kubwa sana na ninaamini kabisa kwamba mimi mwaka jana nilisema kuwa mwaka wowote unaoishia na 4 kuna njaa na wakati huo nasema ilikuwa inanyesha mvua kubwa, nilisema kwenye *RCC*, Mkuu wa Mkoa, Bwana Abdurahman Babu wakati yuko Shinyanga akasema kwamba ninawatisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, Farao alitenda kazi kwa ndoto iliyotafsiriwa na Yusufu. Sisi hapa Tanzania tuna data za hali ya mvua katika nchi yetu kwa nini hatufanyi hiyo kazi. Kama Farao aliweza kufanya kazi miaka saba akaweka chakula kwa ndoto sisi tunazo taarifa hapa na Serikali inazo kwa nini haichukui hatua. Nilikuwa naomba kabisa kwamba suala la njaa kwa kweli tusilifanyie mzaha sababu tutapoteza wapiga kura wetu.

Tuna uchaguzi sasa hivi mwaka 2005 sijui nani atatupigia kura kama watu hawatakuwepo. Najua Serikali inatoa chakula lakini chakula chenyewe hakitoshi. Kinaletwa chakula ambacho kinasababisha ugomvi kwa wananchi. Kwa mfano, kule kwangu niliwahi kwenda nikapewa tani 43 wakasema mimi nimepewa tani 75, tani 43 zingine zilipelekwa kwenye Jimbo la Solwa. Lakini sasa wale Maafisa Watendaji wa Kata wanakuta kwamba kile chakula ni kidogo hakikidhi mahitaji badala yake kuna ugomvi wa hali ya juu kule kijijini sasa hivi na chakula kinachotolewa.

Juzi Mheshimiwa Waziri hapa alinipa taarifa kwamba amepeleka chakula kingine kule tani 150. Lakini tani 150 hazitoshi. Tatizo la njaa ni kubwa kuliko Serikali inavyolifahamu. Sijui hizi *data* wamezipata wapi. Hizi *data* zimetoka wapi. Kwa kweli tunaiomba Serikali ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa. Mheshimiwa Benjamin Mkapa ni mtu mahiri sana suala la njaa atafute watu kabisa wafanye tathmini kama watu walioko kule Mikoani wameshindwa hii kazi atafute watu wa kusaidia. Tunaomba vile vile Serikali ituamini sisi Wabunge kila wakati tunapopeleka taarifa kule kwa Waziri Mkuu ama watu wanaohusika na njaa inaonekana kwamba sisi ni watu ambao tunazua mambo tu, kwa nini hatuaminiki? Sisi kwanza wananchi wanapokuwa wanalalamika hawaendi kwa *DC* wala kwa Mkuu wa Mkoa wanakuja kwa Mbunge. Kwa nini hatuaminiwi? Unamwambia Waziri Mkuu kwamba kwangu kuna njaa anakwambia leta taarifa.

Mimi nimehangaika na taarifa za njaa. Nimekwenda kwa Mkuu wa Wilaya anasema hana taarifa. Nimekwenda kwa Mkuu wa Mkoa anasema hana taarifa. Nimekwenda Manispaa wanasema wamemwagiza Afisa Kilimo atengeneze hizi taarifa. Amezitengeneza hizi taarifa amepeleka kwa *DC* amesema watu walioathirika ni 6,500, *DC* anakata anafanya 2,000 sijui anaogopa nini? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kama tunaficha, tutaficha ukweli. Baba wa Taifa alisema hivi kwa lugha yake alisema: "*Ukificha ficha burwae kiriro kilakubura.*" (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja lakini naomba suala la njaa tusilifanyie mzaha. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hoja hii ya Waziri wa Fedha. Kwanza kabisa ningependa nitamke wazi kwamba naunga mkono hoja hii sina matatizo nayo. (*Makofi*)



Mheshimiwa Spika, mambo ambayo ningependa nichangie hasa hasa yanahusu suala la kilimo cha mazao ya chakula ili kukabili baa la njaa. Kwanza natoa pongezi kwa Serikali kwa jinsi inavyoshughulikia tatizo kubwa hili la njaa. Lakini ni vyema Serikali ihakikishe kama wenzangu wanavyoeleza kuhakikisha kwamba wanapata takwimu zilizo sahihi kutoka sehemu zote za nchi na wasiachwe watu mahali popote walio na tatizo hili la njaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie juu ya mpango wa kudumu wa kukabili njaa yaani kujenga uwezo wa nchi ili kuwa na hifadhi ya chakula kinachotosha muda wote kama ule mpango mzuri uliokuwa umetolewa na Waziri wa Fedha na Serikali kwa jumla juu ya kuwezesha Mikoa minne ya Iringa, Ruvuma, Mbeya na Rukwa ili iweze kuwa na uwezo wa kuzalisha chakula cha kutosha. Kwa hiyo, kukaweza hata kutolewa ruzuku kwa ajili ya mbolea.

Baada ya kujifunza mambo yaliyokuwa yametokea baada ya hapo ni vyema taasisi za Serikali kwa mfano kama Hazina, Kilimo, *Tanzania Fertilizer Company*, Mfuko wa Pembejeo wa Taifa wa-coordinate vizuri suala la uagizaji wa mbolea iwe inafika mapema vijijini kulingana na msimu wa mvua. Vinginevyo unakuta kwamba *delivery* ya mbolea inafika msimu wa mvua ulishaanza muda mrefu. Kwa sababu pengine kunaweza kuwa na urasimu mwingi unaokuwemo hapo katikati.

Kwa hiyo, utakuta mbolea hii iliyoletwa sehemu kubwa kwa mfano kama ya Iringa nina *experience* ya Jimbo langu ni kwamba mbolea ya kupandia hawakupata ila iliwezekana kupata mbolea ya kukuzia. Kwa sababu haikufika mapema kwa walengwa kule vijijini.

Jambo lingine ni tatizo la bei kwa huko vijijini pamoja na kwamba kulikuwa na ruzuku katika mbolea hii lakini bado unakuta mkulima huyu alikuwa anakuta bado bei ni juu sana kwa sababu alikuwa mkulima huyu ana tatizo la kukabiliana la ukame na njaa. Halafu hapo hapo anunue mfuko wa kilo 50 wa mbolea kwa shilingi 12,000 na kuendelea. Fedha taslimu hana.

Kwa hiyo, unakuwa umeweka ruzuku kwenye mbolea ambao kiutekelezaji inashindikana kumsaidia mkulima. Mkulima huyu kumkopesha hakuna mfumo wowote ambao ulio *practical* wa kumkopesha mkulima. Lazima atoe dhamana na wakati huo huo anakabiliwa na ukame na njaa.

Kwa hiyo basi, anakuwa hakupewa fursa ya kumwezesha kupata hii mbolea ili aweze kuongeza mazao ya chakula. Kwa hiyo, inaonekana kwamba menejimenti ya kilimo haijawa yenye uhakika wa mafanikio yaani ule mfumo tulionao wa *delivery of inputs and extension services* kwa wakulima haukusukwa vizuri kwamba una uhakika kitu hiki kikitoka hapa kinaingia hapa kinakwenda hapa. Kwa hiyo, kila wakati kuna vikao na kadhalika.

Kwa hiyo, mara nyingi menejimenti inayumba. Unakuta usambazaji wa mbolea ulipangwa kwamba, *TFC* kwa mfano kama kwa Mkoa wangu wa Iringa ilipangwa ipeleke mbolea kwenye magodown ya Iringa Mjini na Makambako. Sasa baada ya hapo hakuna mpango mwingine tena. Kwa hiyo, mbolea kutoka pale Mjini Iringa au Makambako mpaka kufika kwenye Vijiji kama vya kwangu sijui Wasa, Ihomasa mpaka mpakani mwa Usangu Mbeya zaidi ya kilomita 80 mpaka 100 hakuna mpango wowote ambao unakuwa umewekwa. Ule mpango wa kusambaza mbolea kwamba ifike kwa walengwa haupo.

Kwa hiyo, unakuta hata wale wafanyabiashara ambao tuliwaomba watutawanyie mbolea hiyo ilikuwa wapate mikopo kutoka kwenye mabenki ambayo ilitokana na Mfuko wa Pembejeo wa Taifa, lakini wamekumbana na masharti magumu. Kwa hiyo, wengi wameshindwa, wakaacha. Wengine ambao walichukua kwa vile *system* haipo hakuna wala Mawakala wa Mbolea Vijijini, mtu anatoka na mbolea amejaza kwenye lori anazunguka nayo vijijini, jamani mbolea nauza. Sasa, unakuta mkulima hakujuu kwamba kuna mbolea inakuja, kwa hiyo hakujiandaa. Yule anazunguka anarudi na mbolea imeuzwa kidogo. Kwa hiyo, zile gharama za usambazaji zinakuwa kubwa na *prohibitive*.

Kwa hiyo, napendekeza kwamba *TFC* ipewe jukumu la kufikisha mbolea vijijini, walau kwenye Kata na kule *TFC* iwe na Mawakala wa Mbolea kule Vijijini. Aidha, wanaweza kuwa wafanyabiashara wadogo wadogo, wakulima wakubwa pamoja na Vyama vya Ushirika. Vile vile, hao wakulima wapate

mikopo, kwa maana kwamba ni vema tujue kuwa wakulima wetu sasa hivi wanatambua sana wajibu wao wa kurejesha mikopo na *test* ambayo imekuwepo ni huu mpango wa MEM na *TASAF* kwamba wametumia fedha vizuri sana na tumefanikisha maendeleo makubwa, lakini suala la mikopo kwa wakulima bado hatuwaamini. (*Makofi*)

Kwa sasa hivi kwa sababu tumepata mabadiliko ya Sheria ya Ardhi, kwamba tunaweza kupata hati za kule vijijini na hizi zikatumiwa kama dhamana, naomba Wizara ya TAMISEMI iwahamasishe Halmashauri za Wilaya ili ziwafundishe au zizifundishe Serikali za Vijiji ziweze kujua namna ya kupima ardhi ya wakulima wao na kuandika zile hati. Wizara ya Ardhi nafahamu imetoa *format* ya namna ya kuandika zile hati, lakini unaweza kukuta jambo hili utekelezaji wake unaweza kuchukua miaka mitano kabla haujaanza kuwanufaisha wakulima.

Vile vile, kwa Mfuko wa Pembejeo wa Taifa fedha hizi zipewe mabanki ambayo yako tayari kutambua hati za ardhi zinazotolewa na Vijiji maana fedha hizi ni za Serikali ambazo tumepitisha hapa Bungeni. Pia, mikopo kwa Vyama vya Ushirika, Mfuko wa Pembejeo ufanye hivyo hivyo, lakini hapa wanaweza wakapitisha kwenye hiki Chama kinaitwa *The Savings and Credit Cooperatives Union League of Tanzania Limited (SCCULT)*, wamekuwa wanafanya kazi nzuri sana hawa. Nao watambue hati za ardhi pamoja na mbinu nyingine ambazo wanaweza wakazitumia.

Sasa, hawa *SCCULT* wanaweza wakatoa mafunzo kwa Vyama vya Ushirika na kuvi-transform kuwa *SACCOS*, kuwa Vyama vya Ushirika vya Mazao, halafu vile vile kuweka na kukopa. Ikitokea hivyo, watakuwa na uwezo wa kuwa baadaye na mali ambazo wanaweza wakaziweka kama collateral. Kwa hiyo, wanaweza wakakopa. Lakini tukifanya utaratibu huu ni kwamba tuta...

(*Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika*)

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Muda umekwisha?

**MBUNGE FULANI:** Endelea hiyo ni ya kwanza.

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Ahaa, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, kama tukiweka hizi management linkages zinazohakikisha kwamba huduma hizi zinafika kwa walengwa ni kwamba tutapata mafanikio yafuatayo: Kwanza, tutapata chakula cha kutosha kwa sababu wakulima wanakuwa na uhakika wa mahitaji ya kilimo kwamba wanapata. Pili, wakulima watakuwa wamewezeshwa au kupata fursa ya kupambana na umaskini. Kwa hiyo, kupata maisha yaliyo bora, maana wakiuza mazao mengi kwa bei nzuri ni kwamba hali yao itakuwa nzuri, lakini tutakuwa tumepata chakula vile vile.

Jambo lingine ni kwamba, hivi Vyama vya Ushirika vitaimarika, vikiwa *SACCOS* chini ya usimamizi ya *SCCULT* vitakuwa na uwezo kama nilivyosema, kuwa na mali ya kuweza kuweka kama dhamana. Lakini vile vile ni kwamba, ukitazama jinsi ambavyo nchi mbalimbali za Afrika zinavyofanya ku-create hizi *SACCOS* ni kwamba, hivi Vyama vitakuwa baadaye na *reserves* za kutosha, yaani kujikopesha wenyewe fedha bila msaada wa Serikali. Kwa hiyo sasa, huko vijijini wakulima watakuwa wamekuwa *organized* kama *production units* ambapo tunaweza kuwa na na uhakika juu ya uzalishaji wa chakula na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza kwa haraka kidogo kwa sababu nilitaka niyamalize haya, lakini naamini kwamba Waziri wa Fedha amenielewa maana yeye mwenyewe ni muumini sana wa mambo haya ya *SACCOS*, ndipo tuwe na uhakika wa kupata chakula na siyo kila wakati tuwe tunaombaomba chakula huku uwezo tunao katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia na ninaunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia katika hii Bajeti ya Nyongeza.

Kwanza kabisa namshukuru Waziri wa Fedha na wasaidizi wake kwa kazi ambayo wanaifanya kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali, kwa sababu tunapowasifu TRA hatuwezi kuwatenganisha na Waziri ambaye anawasimamia. Kwa hiyo, tunashukuru kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Tunajua hawafanyi kazi wao peke yao, wanafanya kazi katika mfumo. Katika mfumo kunakuwa na tu-mifumo tudogo tudogo, kwa hiyo, kamfumo kengine kadogo kakiharibika sasa hata lile limfumo likubwa wakati mwingine lina-jam.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia hili la pesa zilizotengwa kwa ajili ya chakula na kwa maana hiyo kilimo. Nitangaze maslahi yangu mimi ni mkulima na sikuwahi kufanya kazi Serikalini. Kwa hiyo, hata kama watu wananipuza hawataki kuniuliza, lakini mambo yanayoendana na kilimo nayajua. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa misingi hiyo, kama alivyotaja mtu mmoja hapa, hata hizo hela zilizotengwa ni kidogo na kama alivyokuwa akizungumza Mheshimiwa Derefa. Sasa, unatenga bilioni 10 na matatizo haya yameanza Zambia, Malawi, Zimbabwe tunayafahamu wamekaa nayo sasa hivi karibu miaka mitatu. Sisi hapa tumejaribu kutenga Shilingi bilioni 10 sijui tunatanzua tatizo la miezi mitatu ijayo au miwili sielewi! Nadhani hatulioni hivyo kuwa, tunako kwenda lazima tungejiandaa kwamba tunapoleta Bajeti hii na tunavyojiandaa tunajiandalia kitu cha miaka minne au mitano na siyo mitano, kwanza isirudie. Nadhani Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, alisema anaona aibu kuwa wanaomba chakula. Kwa kweli ni aibu na nadhani ninaposema ni aibu kwa upande wa Serikali wangekuwa wanainama chini kwa kushika macho. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisema juzi hapa mtu umeambiwa mtoto anaumwa wewe una ng'ombe, una mbuzi. Unaambiwa: "Uza tupeleke mtoto shule" wewe unang'angana. Halafu mtoto anakufa, unamchinja yule ng'ombe wako wa maziwa mnakula nyama kwenye kilio halafu mnacheka. Hii maana yake ni nini? *(Kicheko)*

Tunapozungumza kutoa ruzuku kwa wakulima kwa ajili ya kilimo watu wanasema: "Hayo ni maneno yenu, utatoaje ruzuku sisi nchi maskini?" Lakini kusamehe wanaochimba dhahabu kodi hiyo ruksa. Matokeo yake tulivyozungumza hivi sasa Serikali haiwezi kusema haijapata hasara, hata hiyo ya ruzuku iliyokuwa inaikatalia kwa sababu hawatapata kodi ambayo wangeipata kama wangeuza mchele nje au maharage, au mahindi. Serikali itatumia hela zile ambazo imekusanya kutoka kwenye sehemu nyingine mfano viwanda, kwenda kununua hicho chakula kwa hiyo ingetoa ruzuku. Serikali imetumia hela za kigeni zilizokuwepo, badala ya kuagiza vitu vingine itazitumia kuagiza hicho chakula. Sasa, yapo mambo ambayo lazima uyaangalie, unapokataa hiki ujue kwamba unajizalishia kitu kingine.

Mheshimiwa Spika, katika nchi ambayo zaidi ya asilimia 80 ya wakazi wake ajira yao na kazi yao na mapato yao ni kilimo inasikitisha. Lakini kwa kuwa viongozi wao hasa baada ya kupata mapato kutokana na utalii, viwanda na mageuzi hawategemei tena kupata hela kutokana na kilimo, wao kwamba wanaweza kujilipa mishahara, wakajinunua magari, wakajilimbikizia utajiri kutokana na maeneo hayo, sasa kilimo wanakisahau. Ni bahati mbaya kwamba mambo hayo mawili sasa yaendi vizuri katika nchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kuna wakati tulikuwa tunapishanapishana humu na mpaka wengine ukiwaambia wanakasirika wanasema: "Mutungerehi ana mdomo mbaya anasema maneno mabaya." Lakini watu tumewaeleza hapa. *(Makofi)*

Kuna methali moja Wafaransa wanasema: "*Celui-qui aime les vaches pouvoit s'endormir comme ces elles.*" Wale Wamasai wanajua. Yule anayewapenda ng'ombe lazima alale kama wao, ndiyo maana Mmasai anahama na ng'ombe wake analala huko ananyeshewa na mvua analiwa na mbug'o, anawatafutia maji na anahama kufuata nyasi. Kama huwezi kufanya hivyo, huwezi kupata wale ng'ombe angalau kwa kiwango hicho cha hali yao ya ufugaji. Ndiyo maana yake, kwamba awapendaye ng'ombe

analala kama wao. Najua hapa hata watu wa Kilimanjaro mnaelewa, wewe kama umefuga hata wale ng'ombe wa kawaida hutaki kwenda kutoa yale matope mle ndani, ng'ombe atafanana kama nguruwe na hutapata maziwa.

Sasa kama umezungumzia kilimo, halafu mnaowapanga washughulikie kilimo wanakaa pale kama alivyosema Mheshimiwa Halinga wanaanza kutunga hadithi pale mezani: “Mimi nilisoma Ulaya, kilimo unaendesha hivi...” Unaendesha hivi wapi? Hapa ...

*(Hapa Microphone ilizimika)*

Mheshimiwa Spika, tukubaliane hapa, siyo suala la semina ya siku moja wala la kucheka. Watu wako kwenye ajira, inawaajiri asilimia 80 ya nchi siyo maneno ya kucheka hapa, tutenge wiki moja tuje tukubaliane hapa mkakati wa kilimo ni nini. *Experience* yetu sisi Wabunge, tunaotoka kule ni nini, kwa sababu naamini walio wengi wanatoka huko huko. Hakuna eneo la Tanzania ambako wakulima wapo hatoki Mbunge. Tukubaliane hapa ni nini. Nilileta maelezo hapa nikamwambia Mheshimiwa kuhusu kahawa: “Wewe hela zetu unazitafuna kahawa itaporomoka bei.” Akasema: “Wewe ni mlaghai na mwongo.” Lakini nina ushahidi ambao hawezi kupinga.

Mheshimiwa Spika, nadhani Mbunge anapozungumza ana ushahidi unautaka aulete, niulete? Sasa nauleta, kutoka kwenye authority ambayo ulitumbia juzi. Mheshimiwa Rais anasema: “Uzalishaji wa mazao ya korosho ulishuka kutoka tani 122,00 hadi tani 90,000, kahawa kutoka tani 58,000 hadi 52,000. Kushuka kwa uzalishaji wa korosho na kahawa kulitokana na wakulima kukosa fedha za kununulia pembejeo baada ya bei ya mazao hayo kushuka.”

Mheshimiwa Spika, sasa sijui kama ushauri huo amepewa na Waziri wa Kilimo au sijui ameutoa wapi, kwa sababu Waziri wa Kilimo na Chakula hautambui.

Mheshimiwa Spika, sasa haya ndiyo maneno tunayoyasema. Bahati nzuri mimi kwangu hamna njaa na tangu mwaka 1947 hapajawahi kuwa njaa pale Karagwe.

Kwa hiyo sina tabu. Lakini sioni gele kwamba wengine wasipewe na siyo wapewe chakula maana yake Rais ametuonya hapa siyo kuwapa ili wakushukuru, kwamba tulipokuwa na njaa Serikali ilitujali aah, uwawezesha wazalishe chakula chao. Chakula kile wengine mnasema *cash crop*, mimi sioni *cash crop* maana yake nini? Kwani kama mchele unauzwa *is cash crop*, kama mahindi yanauzwa hiyo *cash crop*.

Kwa hiyo, tuwawezeshe wazalishe, siyo njaa imewakaba sasa hivi anauza ng'ombe wake anakwenda kununua chakula badala ya kuuza ng'ombe yule aende kusomesha mtoto au kujenga mtaji mwingine. Halafu tukasema hapa: “Wapeni hela za *STABEX*.” Wakasema: “Hatutawapa, watalewa. Nyingine tutawachimbia barabara nzuri.”

Sasa tukauliza hapa: “Hela za barabara ziko wapi?” Mimi nilidhani Serikali imezitifuna hizo hela, kumbe siyo Serikali iliyozitifuna, nadhani ni watu wawili ndani ya Serikali. Waziri wa Ujenzi mwenye barabara anasema: “Mimi sizijui.” Waziri wa Fedha anasema: “Mimi nilizitenga nikazipeleka kule.”

Mheshimiwa Keenja ni wajibu wake na mimi sivunji Kanuni kwa kumtaja hapa, atuambie hizo hela ziko wapi, maana uharibifu ndiyo huu. Pale unataka kutekeleza sera uwape wakulima ruzuku umekataa, unagombana na watu wa Ulaya, Wazungu ni wajinga wanawapa watu wao ruzuku. Wamekupa wewe uwape wa kwako unakataa, wamekupa tengeneza barabara, barabara hukutengeneza, mazao ya watu wakiyaacha halafu unalalama, unajua umaskini umezidi watu wameacha kulima. Sasa unalalama nini, wewe si ndiyo ulikuwa pale?

Mheshimiwa Spika, mimi siungi mkono bajeti hii na wakati wa kupitisha vifungu nakamata hapo mpaka Mheshimiwa Keenja aseme zile hela za *STABEX* alizopewa kutupa tupeleke kwetu tukulime barabara ziko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka atueleze zilipo. Sasa kama hizo za barabara ambayo ndiyo tunaweza tuiona, hatuioni; je, zile ambazo zinakwenda kwenye Sekta ambazo hatuzioni, sijui Chuo cha Utafiti, sijui kupeleka pale, ambazo hatuwezi kuziona wala kuuliza, kwa sababu vile ni vitu ambavyo ni *physical* kwamba unaviona, hizo zenyewe ziko wapi?

Sasa, katika mazingira kama haya ndizo tunasema kwamba juhudi zetu nyingi zitakwama, njaa itaingia, watu hawatakuwa na chakula na ni wengi, Wamachinga watajaa Mjini, tunafukuzana nao pale na virungu, halafu tunasema umaskini sijui utakuwa umepungua, halafu tutajisifu kwa misaada tunayopewa.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kutaja hapa kwamba hela zilijaa pale *foreign reserve* zote ni misaada tu na mikopo, si kwa sababu tumeuza mahindi, wala karanga wala kitu chochote wakanikejeli. Lakini nadhani Mheshimiwa Rais amesema hivi viko humu. Hivi hao Wazungu watakaposema sasa misaada yetu tunaisitisha mnafanaye? Na kutatokea nini? Maana yake kitu cha msingi sisi tunapuza.

Kwa hiyo, hii bajeti kwa kipengele tunachozungumza, hizo fedha Shilingi bilioni 10 sioni kama ni nyingi na tunamwomba Waziri kwamba uliangalie kwa upeo wa kujua kwamba hiyo Sekta ya Kilimo mnei-stimulate vipi? Ikiwa ni kujiandaa, msije mkadhani kwamba hii ni ya miezi mitatu watu watavuna. Wasipovuna tunaendelea kufanya nini? Kwa sababu hii imetokea kule Malawi tumeshawaeleza na mmekuwa mnaiona.

Mheshimiwa Spika, baada ya kulisemea hilo niseme hili jingine la ndege. Ndege nadhani hatukatai kwa sababu kama kuna mtu anakuwa na staili yake hiyo stahili lazima aipate. Kama tumekubaliana Wabunge watakopeshwa magari yenye thamani kiasi fulani ni mapya watapata. Kama ni Wizara itanunuliwa gari kwa Shilingi milioni 50 wanapata sisi hatukatai. Lakini tunachopaswa kuchunguza ni: Je, kama tumesema gari ni Shilingi milioni 50, mtu akitaka kununua kwa Shilingi milioni 80 tushangilie tu kwa sababu anastahili?

Hoja ya msingi hapa haiwi kama kunastahili kununua hiyo gari ama hiyo ndege, hoja ya msingi ni kwamba; je, *can we query?* Pia, tunaweza kujidhihirisha kwamba bei ndiyo hiyo hiyo au kuna *manipulation* na mizengwe mingine? Hiyo ndiyo hoja ya msingi na nadhani ndicho kitu cha msingi. Nilikuwa nasoma gazeti wanasema Rais mwenyewe ndege hiyo hakuitaka, lakini kwa sababu wanasema ndege ni ya Serikali, huenda na wale wengine wa Vyama vya Upinzani wakapakiwa siku moja wakaletwa hapa ili waambiwe. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulichokuwa tunataka ni kwamba Mheshimiwa Waziri anapotujibu na inawezekana wakati mwingine mimi ninavyoamini, sijawahi kufanya kazi Serikalini, lakini sidhani kama Waziri ndiyo anajipeleka pale anasema lete mkataba, lete tu-*negotiate*, kila makaratasi anayo. Anaweza kuwatuma wataalam wake wakamletea pale na kwa sababu anawaamini wakafanya hivyo. Lakini huenda kukawa na makando makando ya vitu ambavyo si sahihi.

Kama inaweza kutokea ndivyo hivyo basi Mheshimiwa Waziri wakati anatujibu hapa, yeye akubali hiyo kwamba kunaweza kuwa na *doubt* mahali fulani ili turekebishe haya mambo tufike mahali tuwe tunakubaliana. Maana kama unabeba maji kwenye gunia kama uliweka limejaa yatakwenda yanavujavuja, hutayafikisha huko unakoyapeleka.

Kwa hiyo, kuvuja huko kwa mapato haya ya Serikali ndiko kunatufanya wakati mwingine tusiweze kutimiza haya ambayo tumekuwa tumekusudia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ilikuwa niseme na kwa uchungu kabisa hilo suala linalohusika na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, hii itakuja kumchafulia maana yake mwanzo kabisa walipomtangaza kuwa Waziri wa Kilimo na Chakula, iko kwenye *Hansard* nilisema: “Namwamini atafanya kama alivyofanya pale katika Jiji la Dar es Salaam.”

Sasa yaani sifa zote zitaharibika, maana ndiyo watu hawana cha kuuza, kahawa ndiyo watu wanaing’oa, mahindi hamna na miaka mitano inakwisha, sasa ni *problem*, sijui itakuwaje? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kupata majibu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndiyo tunafikia mwisho wa kipindi cha asubuhi cha kikao cha leo, tutaendelea mchana. Kwa ajili hiyo, sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.48 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kuniwezesha kupata nafasi hii niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii iliyo mbele yetu. Muswada umeleza shabaha na madhumuni ya Muswada wenyewe na shabaha ya kwanza kabisa ni ile ya kupitisha matumizi ya gharama ya kununua chakula cha njaa kiasi cha shilingi bilioni 10. Shabaha ya pili, ni gharama za kulipia umeme kiasi cha shilingi bilioni 37.3 hivi na tatu ni ile gharama ya ununuzi wa Ndege ya Serikali. Mimi sisemi Ndege ya Rais Mkapa, nasema ni Ndege ya Serikali. Kesho na keshokutwa Mkapa anaweza asiwepo, akawepo Rais yeyote, kwa hiyo, anaweza akaitumia, lakini ni ya Serikali. Kwa hiyo, hayo ndiyo mambo matatu ambayo tunatakiwa lazima tuyachanganue na tuisaidie Serikali iweze kupitisha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ningependa nichangie tu kwa mpangilio ufuatao: kwanza Muswada ni mzuri sana, unajadilika na pia nauunga mkono kwa shabaha zile zile za kuuboresha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, fedha bilioni 10 za kugharamia janga la njaa ni chache sana, hazitoshi hata kidogo. Kama ningekuwa mimi ndiyo serikali ningesema bilioni 25 ndiyo zinaweza zikakabili janga la njaa lililopo katika nchi yetu, kwa sababu ni zaidi ya asilimia 80 ya Mikoa yetu yote inakabiliwa na njaa, tena sasa hivi ndiyo kali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu labda Serikali haijajuajua vizuri nini maana ya tafsiri ya njaa, nataka niikumbushe ili iweze kujua, mimi naona katika vipengele vyote vitatu, hiki ndiyo kikubwa zaidi, ndiyo kizuri zaidi. Tafsiri ya njaa ni binadamu kukosa milo muhimu miwili. Yaani anaishi kutwa nzima asubuhi, mchana, jioni hakuna chakula, analala hivi hivi bila chakula. Ndiyo maana ya tafsiri ya njaa. *(Makofi)*

Tafsiri ya pili ni watu kukosa matumaini ya kuishi kutokana na tatizo la njaa. Hiyo ni tafsiri ya pili. Nataka Serikali ijue na mwishoni nitasema maneno. Tatu, katika tafsiri hiyo hiyo watu hupoteza maisha, yaani hufa kutokana na tatizo la njaa.

Lakini tafsiri ya nne, watu hushindwa hata kufanya kazi. Sasa hivi mvua zimenyesha mashambani huko hakuna watu wanaolima kwa sababu ya njaa, watakwendaje kulima wakati wana matatizo ya njaa? Kwa hiyo, hiyo ni tafsiri mojawapo ya njaa, tunaposema njaa. Kwa hiyo, naomba na Serikali ijue hilo. *(Makofi)*

Lakini pia tafsiri ya tano, magonjwa huwaua watu kirahisi sana. Mtu aliyedhoofika kwa matatizo ya njaa akiumwa hufa na wakati fulani watu husema kafa kwa ajili ya njaa. Ni kweli kwa sababu njaa imemkuta amedhoofika. Kwa hiyo, ni hatari sana. Kwa hiyo, naiomba serikali izingatie sana katika masuala haya. Tafsiri ya sita, wanaume hukimbia nyumba au familia zao na wanabaki akina mama na watoto ndiyo wana matatizo zaidi. Hata ukienda katika maeneo yenye njaa, familia zilizobaki nyumbani zinahangaika na watoto ni akina mama. Kwa kweli mimi nawapongeza sana na kuwasifu, wanajitahidi sana. *(Makofi)*

Tafsiri ya saba, vifo vya watoto huongezeka na hasa watoto wadogo, kwa sababu mama akila akishiba ndiyo maziwa yanapatikana, kama hakula na kushiba maziwa hakuna. Ugonjwa kidogo mtoto anafariki. *(Makofi)*

Tafsiri ya nane, binadamu hula binadamu mwenzie njaa inapodhihiri ili apone na kadhalika na tusipoangalia tunakwenda huko.

Tafsiri ya tisa, watu hula mizizi na matunda sumu wakifikiria wanajinusuru, lakini wakati huo huo kumbe wanajiua. Tafisi ya kumi, hakuna ubinadamu katika njaa. Kwa hiyo, kunakuwa na ujangili, kunakuwa na wizi na kadhalika, amani inakuwa haiipo.

Tafsiri ya kumi na moja. Masuala yote ya afya huzorota nchini, elimu vile vile huzorota, maendeleo yanazorota na uchumi unadorora mara dufu kutokana na tatizo la njaa lisiposhughulikiwa vizuri.

Tafsiri ziko nyingi lakini nimekomea tu ya kumi na mbili. Ya kumi na mbili, wananchi huichukia Serikali wakifikiri kwamba Serikali inafanya makusudi. *(Makofi)*

Jambo la kwanza, kwa hiyo basi, kama ilivyoelezwa hata na Waheshimiwa Wabunge wengine, zaidi ya asilimia 80 ya Mikoa yetu yote imekumbwa na njaa tena njaa kali. Tunatofautiana tu kwa viwango. Mfano tu katika Wilaya yangu ya Kondo, Wilaya ya Kondo ina watu/wakazi wasiopungua 429,824. Wanaume wapo 213,729, wanawake 216,095 na kaya zipo 89,895. Hivyo asilimia karibu 75 zote zinakabiliwa na tatizo la njaa. Ndiyo maana nilisema kwamba shilingi bilioni 10 hazitasaidia chochote kwa sababu hiyo ni wilaya moja tuna Wilaya nyingi zinafanana na hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali basi itunusuru sisi wa Kondo, lakini pia na majirani na Wilaya zingine zote na Mikoa mingine yote.

Jambo la pili, katika kuboresha Muswada huu kwa manufaa ya wananchi wetu mimi nasema kwamba fedha za kununua na kusafirisha chakula, narudia tena bilioni 10 hazitoshi ni chache sana. Serikali iangalie katika hazina yake iongeze ndiyo itakabili suala hili. Sisi ndiyo tunatoka huko katika maeneo halisi ya njaa. *(Makofi)*

Hata hizi bilioni 25 nilizotaja hizi ni chache kabisa. Kwa hiyo, namwomba sana Waziri wa Fedha, ndugu yangu Pesambili Mramba aongeze, atafute fedha zaidi ili tukabiliane tena kwa operation hasa vinginevyo tutafika mahali tutakwama. Kwa hiyo, hali ya njaa ni pana. Tusifanye mzaa wowote katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu sasa napendekeza mpangilio uwe kama ifuatavyo; kwamba fedha za chakula kwa ajili ya kununua chakula, kusafirisha na kupeleka katika maeneo ambako kwa walengwa mimi nasema kwamba ni shilingi bilioni 25 ndiyo zitatoshereza vizuri kukabili hali iliyopo.

Jambo la nne, umeme na kadhalika bilioni zile zile 37.3 na katika Ndege ya Serikali bilioni 40 kama ilivyo mimi nakubali kabisa ndege ya Serikali inunuliwe sina kikwazo kabisa. Lakini ili tufanikiwe Serikali ihangaikie chakula, ihangaikie hawa wananchi chakula. Jumla ya matumizi ya ziada kwangu mimi kwa mujibu wa hesabu ni shilingi bilioni 102.3, kama itajengwa hivyo mambo yanakuwa mazuri kabisa. Kwa hiyo, hii ina mantiki hata wananchi watatuelewa na wataridhika kabisa kwamba Muswada huu ni mzuri. Pia kasi ya kusambaza chakula cha njaa haitoshi lazima tujitahidi kabisa tuwe na msukumo tuanzishe kitu kama *operation*, chakula kisafirishwe kwenye Mikoa kiende kwenye Wilaya, kiende kwenye vijiji ambako wako walengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimependa kueleza Serikali haya, nimetumwa na wananchi si wa Wilaya ya Kondo tu bali wa nchi nzima kwa sababu siku hizi mtandao ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba Serikali izingatie na hasa hasa tuwe na kasi kubwa ya kusambaza chakula kwenye vijiji. Njaa ni njaa ni hatari sana. Mimi sitapenda kusikia watu wanakufa kwa sababu ya njaa, uwezo tunao kabisa wa kuwahi sasa ili watu waweze kupona njaa. Baada ya hapo nashukuru sana naunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. KABUZI FAUSTINE RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyo mbele yetu. Mimi nakubaliana na maombi ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, moja kwa moja, na ni ya msingi yote kama yalivyo na kweli kwamba fedha za njaa ni vizuri ziongezwe. Tunawomba naye akubali kuziongeza kwa sababu hata kwangu Wilayani ya Geita kuna tatizo la njaa na sehemu nyingine unazopita sasa hivi hali ni mbaya sana. Ukiangalia hii shilingi bilioni 10 itakuwa ni kidogo sana kama alivyosema wenzangu waliotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambayo kwa kweli yanatisha na hakuna kitu kibaya kama mtu kuona anahangaika kwa ajili ya kutafuta chakula. Kwa mtu ambaye haelewi tabu, tabu ni wakati ana njaa anakwenda kutafuta chakula. Kuhusu suala la Ndege ya Serikali ni vema ndege inunuliwe. Viongozi wetu wasafiri vizuri, wasisafiri na ndege za mashaka mashaka kwa kipindi hiki. Ni vizuri wapande ndege waangalie na ina hali gani naimani watakuwa wamefanya uchunguzi wa kutosha. Lakini katika yote haya yaliongezewa nilikuwa nafikiri kuna janga jingine ambalo kuna haja sasa Serikali kuliangalia mimi nilidhani katika kuondoa fedha hizo, wamejaribu kuangalia matatizo mengine yaliyopo, maana yake tunaona tunalisha pua tunasahau mdomo. Kuna watumishi ambao vile vile wanakaa mazingira haya njaa Serikali wanaidai na vyakula vinapopanda bei na wenyewe wanahangaika hivyo hivyo, hususan walimu pamoja na waganga wanaoweza kwenda kukaa vijijini na waratibu. Watu wamehamishwa mara mbili, mara tatu hawajalipwa haki zao. Sasa tunawafikiriaje hawa na wenyewe wananyong'onyea hivyo hivyo wana matatizo. Sasa mimi nilikuwa namwomba Waziri wa Fedha ni lini haya madeni atayalipa ya walimu ambao wanapiga kelele, ukizunguka kila mahali wanalalamika. Serikali haiwajali. (Makofi)

Mimi naona hata sisi Wabunge, tukiwa ndani kama labda inachelewa siku nne huwa hali ni mbaya, lakini hawa miaka miwili, mitatu, mtu anahamishwa au anapandishwa vyeo vitatu juu yake hajapata hela yake. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha hawa watu watalipwa lini? Juzi Rais ametuhutubia hapa vizuri kabisa na akatoa data ambazo zilitia matumaini, nikafikiri sasa Waziri wa Fedha, atakuja anasema na madeni ya watu tutawalipa sasa wasiwe na wasiwasi hawatuelewi wasipolipwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Serikali iwaangalie hawa watumishi madeni yao yalipwe. Mimi kwangu kuna walimu nimekaa nao kata ya Bukondo, Chigunga, Nyakagomba, Nyalugusu, wote unapokutana nao kila mmoja amenuna na hali ya maisha ilivyo na hali ya njaa iliyopo hawawezi kumudu. Sasa tumeongeza idadi ya madarasa, tumeongeza idadi ya wanafunzi sasa hawa wanafundishaje kama na wenyewe wako katika mazingira hayo? Mheshimiwa Waziri wa Fedha nilikuwa naomba hilo walimu na waganga walipwe.

Labda ili wakati mwingine Serikali, iwajibike nilikuwa nafikiri kuna haja ya kuongeza, wapewe *penalty*, Serikali 10% kama mwaka mzima mtu hajalipwa miezi inayofuata kila wakati iwe inaongezeka kwa sababu fedha kila wakati inashuka thamani. Umeni-*promote* leo kuja kupata fedha yangu labda 2010 maana yake ile fedha haina thamani tena. Basi anapopata mtu *promotion* au anapohamishwa ukimchelewesha kumlipa kuwe na *penalty*, Serikali itawajibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi hainifariji tunapozungumza tunaangalia upande mmoja, lakini na hawa tuwaangalie ni wenzetu na ndiyo wanatufanya tuishi hapa. Naomba sana Waziri wa Fedha kama anaweza kuongeza ebu aongeze na hawa. Mkoa wa Mwanza najua wanadai karibu milioni 600 na nchi nzima sidhani kama ni zaidi ya bilioni 4. Sasa walipeni hawa watu, tuwalipe. Serikali tunaiomba sana iwalipe. Siyo kungoja wakati wa mbanano kwamba sisi tuwalipe inakuwa haina shukrani hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize kwa kusema fedha ya njaa kwa kweli kulingana na hali ilivyo katika nchi hii, inatisha ni kidogo mno na kuhusu suala la watumishi naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie kama kitu ambacho ni makini hongereni. Ahsante sana. (Makofi)



**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kabla sijamwita mchangiaji anayefuata nimepata vi- *note* vingi hapa vya kuomba kuchangia, lakini naomba niwakumbushe tu kama alivyosema Mheshimiwa Spika, leo asubuhi, orodha zote zimefungwa. Mjadala huu unaendelea na ile Hotuba ya Mheshimiwa Rais, yote imefungwa kwa hiyo, haiongezi tena watu. Kwa hiyo, naomba niwakumbushe hilo. Sema tu naweza kupata vi-*note* kuuliza niko wa ngapi kwenye orodha hiyo, hiyo haina tatizo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze nikachangia katika hoja hii muhimu ya Mheshimiwa Waziri wa fedha. Labda nianze kwa kumpongeza kwa dhiti kabisa Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere kwa kuteuliwa kuwa Mbunge.

Nawapongeze sana vile vile Waheshimiwa Wabunge, wenzetu ambao watatuwakilisha katika Bunge la Afrika na vile vile katika Mikutano ya Wabunge wa *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote waliogombea walikuwa na sifa nzuri sana, lakini nafasi zilikuwa chache. Hivyo basi nawapongeze vile vile wote walioomba nafasi lakini wakashindwa kuzipata hizo nafasi. Katika hili mimi naona hakuna aliyeshinda wala aliyeshindwa, mshindi ni Bunge lako tukufu kwani limetekeleza wajibu wake kufuatana na mikataba ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa pole vile vile Waheshimiwa Wabunge, wenzangu ambao wamepoteza, ndugu, marafiki na jamaa katika kipindi tangu tulipokutana mwezi wa 11 nasema poleni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea naomba nitamke mapema kabisa kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utakuwa katika maeneo mawili, moja ni mchango mfupi tu kuhusu ruzuku kwa Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) halafu la pili, kama ambavyo mnaweza kukisia Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu ununuzi wa Ndege ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ruzuku ya shilingi bilioni 2.3 kwa *TRC* kwa kweli ni muhimu sana na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kuona umuhimu wake. Itaimarisha kwa kiwango fulani shughuli za *TRC* mpaka hapa tutakapoweza kukodisha kunako mwisho wa mwaka huu.

Lakini katika kipindi hiki shehena imeongezeka na uwezo wa shirika umepungua kwa hiyo, hata baada ya kusambaza chakula cha njaa tutahitaji *TRC* iweze ikaendelea kubeba mizigo na shehena na abiria si Tanzania tu lakini vile vile kutoka nchi za jirani. Katika msimu baada ya huu msimu wa mvua *TRC* itahitajika vile vile kubeba mazao hasa kutoka maeneo yale ambayo mvua zimekuwa nzuri. Kwa hiyo, yote haya hasa hizi fedha zitasaidia sana katika kuimarisha *TRC* katika kipindi hiki cha mpito.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mheshimiwa Edson Halinga, aliposema Reli ni mkombozi wetu. Kwetu sisi hii ni kama kauli mbiu na tutaizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nielekeze mchango wangu katika kutoa ufafanuzi kuhusu ununuzi wa Ndege ya Serikali. Nashukuru kwamba umuhimu wa ndege hii unaeleweka sana na hasa baada ya Mheshimiwa Mramba wakati fulani kueleza kwa lugha rahisi na nanukuu kwamba “hivi sasa mnataka Rais/Viongozi wetu wapande punda kwenda London”? Basi hilo alimaliza *debate* yote. *(Makofi)*

Lakini kilichonishangaza leo ni kauli ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ambaye ni Msemaji Mkuu wa Upinzani, katika masuala ya fedha, anasema kwamba Wapinzani bado wanaendelea kupinga ununuzi wa ndege. Sijui wanapinga nini? Wanasema kama tulivyopinga.

Mheshimiwa Spika, sasa nimkumbushe tu alipokuwa akichangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi Msemaji wa Upinzani tarehe 4 Julai, 2003 Msemaji wa Upinzani katika masuala ya Mawasiliano na Uchukuzi Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, aliunga mkono kwa niaba ya Wapinzani ununuzi wa Ndege mpya ya Serikali na alisema pamoja na mambo mengine na ninanukuu na

mtaweza mtaanza kuipata katika hansard kwamba “tatizo si kama ndege kununuliwa au isinunuliwe ni wazi kwamba shughuli za Rais wetu zinahitaji matumizi ya ndege nzuri”. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa zito zaidi katika kauli ya Waheshimiwa hawa yaani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi ni kuhusu bei ya ndege ya aina ya *Gulfstream G550*. Nitazingatia zaidi katika mchango wangu katika suala la bei kwa sababu yale mambo mengine waliyoeleza ya kiufundi nitawasamehe kwamba hawaelewi sawa sawa. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei kumekuwa na upotoshaji dhahiri na pengine wa makusudi kuhusu bei ya ndege aina ya *Gulfstream G550*. Wanasema na eti kwa kujiamini kabisa kwamba bei ya *Gulfstream G550* ni kati ya dola milioni 18 na dola milioni 26, ya jana, mimi nimepata ya leo.

Hata ya leo, taarifa hiyo inazungumzia mkataba, wa wananishangaza. Chanzo chao cha bei hizo eti ni taarifa hii hapa ya *Global Security*. Mauzo ya ndege nne za *Gulfstream G550* kwa ajili ya Wizara ya Ulinzi ya Israel. Nisikilizeni kwa bei ya dola milioni 473 yaani ndege moja kwa bei ya dola milioni 118.2 wanasema hawa katika mkataba huo kwamba Waisrael wanaweza wakaongeza ndege mbili zaidi katika mkataba huo wakitaka.

Hata ukichukua thamani ibakie vile vile dola milioni 473 gawanya kwa 6 utaona kwamba bei ya ndege moja katika mkataba huo ni dola 78.8 milioni. Nashangaa! (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, sasa sehemu hii hawa Waheshimiwa, wameshindwa kulieleza Bunge maana yake ndiyo *preamble*. Huu ni upotoshaji wa hali ya juu. Sasa makala hiyo hiyo, hii aliyokuwa akiipeperusha sana Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, inasema mkataba huo wa mauzo ni pamoja na mkandarasi kuwasaidia Waisrael kuangalia ndege, kutoa vipuli, kutoa ushauri kwa miaka kumi kwa dola 18 milioni yaani mkataba wa *logistical support* ni dola milioni 18 siyo bei ya ndege. Mbunge yeyote anaweza kusoma na hawa watu wanafahamu kingereza. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, halafu wanasema hawa katika mkataba huo na Waisrael kwamba iwapo wanaweza wakaongeza miaka 10 kuangalia hizo ndege, mkandarasi aendelee kuzingalia hizo ndege basi mkataba huo wa kuongeza support kwa ndege hizo ni dola milioni 28 siyo bei ya ndege. (Makofi/Kicheko)

Labda niseme kwa kingereza maana yake ni Walatini hawa wanafahamu hata Kilatini. Wanasema: “*The contract includes a ten year contractor logistics support program valued at 18 milioni dollar. Wanasema with a follow up of ten year option valued at up to 26 milioni dollars.* Sasa mimi sielewi kabisa. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hawa kinachozungumziwa hapa ni *program support* wala siyo bei ya ndege na hawa ni wasomi wenzangu. Sasa sijui kwa nini tunaweza kupotosha Bunge lako Tukufu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, bei zikoje? Ukweli ni kwamba waende wakasoma katika Jarida la *Business and Commercial Aviation* wakachukue makala tu ya mwezi Mei, 2003 wakati tulipokuwa tunazungumza na hawa wakandarasi. Nitaje bei ya ndege za aina hiyo *Bombardier Global Express BD - 700* ni dola 44,400,000 za aina hiyo za kubeba wakubwa. *Gulfstream G550* kwa bei ya mwaka jana ni 46,760,000 milioni. *Airbus A310 Corporate Jetliner* ni US\$ 47,000,000, *Boeing 737 - 700* ni US\$ 52,000,000, *Boeing 737 - 800* hizi ndiyo kama zile anazotumia Mheshimiwa Mbeki ni US\$ 65,000,000. Sasa hizi bei za mitaani wametoa wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala hili labda nikumbushe tu kwamba Kanuni za Bunge kifungu 50 (1) kinasema ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni kwa sababu hiyo Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni atawajibika kwa uhakika kwa yale anayoyazungumza, yaani kwamba maelezo anayotoa yawe sahihi na siyo mambo ya kubuni wala ya kubahatisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala hili ni zito lilikuwa limewafadhaisha wenzangu wengi hasa wana Chama cha Mapinduzi. Lakini sisi Chama cha Mapinduzi ahadi yetu ni kwamba tutasema kweli daima, uongo kwetu ni mwiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala hili kama Waheshimiwa, wamezungumza kwa bahati mbaya basi wamekaa kiti cha nyuma ya gari. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Mimi nianze na kuunga mkono hoja hii, lakini naomba kujazia sehemu tatu, nne kama ifuatazo:-

Suala la kwanza ni katika kipengele cha fedha cha kununulia chakula kwa ajili ya njaa na hapa nampongeza zaidi Mheshimiwa Waziri wa Fedha, lakini asisahau Mtwara Vijijini. Kama Serikali haijapata taarifa kwamba Mtwara Vijijini kuna njaa, ndio nawaambieni sasa kwamba Mtwara Vijijini kuna njaa kiasi kwamba watu wanakula vyakula vya kubahatisha mpaka wengine wanadhutulu kula vyakula vyenye sumu, athari yake wakapooza watu si chini ya 140 katika Kata ya Nitekela, Njengwa, Ntiniko na Kiromba. Hao nimewaona mimi mwenyewe machoni na Serikali inayo taarifa. Baada ya kupata vipimo ikaonekana sio *Polio*, bali ni aina fulani ya vyakula wanavyokula havina uhakika vina sumu ya *thyroid* ndiyo ikawafanya wawe katika hali hiyo. Ninawaombeni sana kama hama taarifa Mtwara Vijijini kuna njaa, ninawaambieni leo Mtwara Vijijini kuna njaa, hiki chakula kipelekwe kila Kijiji. Suala lingine ni kuomba fedha kwa ajili ya miradi ya umeme. Kumbe inawezekana Serikali ikatafuta hapa na pale fedha kwa ajili ya umeme bwana! Sasa ule mradi wangu wa Nanyamba ambao tayari umeshafanyiwa *survey* kutoka Tandahimba mpaka Nanyamba, survey tayari, hivi haiwezekani vile vile kuchomeka humo humo? *(Kicheko)*

Halafu katika ule mradi wa maji wa Makonde, tatizo kubwa ni *transformer* ndogo, lakini mradi ule wa maji unapeleka maji mpaka Mtwara Vijijini na kusambaza Kata ya Nitekela, Njengwa, Ntiniko, Nima, Kiromba, Nanyamba na kadhalika. Lakini tatizo *transformer* ndogo, haiwezi kusukuma *pump* nyingi mpaka ikapeleka maji Wilaya nyingine. Hivi kuna uwezekano wa kutafuta fedha kwa ajili ya fedha ya umeme? Basi kwa nini *transformer* hii isichomekwe humo humo ili maji yakafika Mtwara Vijijini yakawanufaisha wanaopata shida ya maji Mtwara Vijijini?

Upande wa elimu, ni kweli kwamba kuna vijana wetu wamefanya vizuri mwaka huu ila hawakupata nafasi, sisi Mtwara Vijijini tunao wasiopungua 250 ambao wamefaulu lakini hawakupata nafasi ya kwenda Sekondari kwa sababu Shule za Sekondari ni chache. Hatua tuliyoichukua sisi ni kujenga Shule za Sekondari kwa haraka haraka, Shule ya Sekondari ya Kitaya na Msimbati. Lakini pia tutaongeza mikondo Nanyamba na Nanguruwe, baadaye tuna mpango wa kuendelea kujenga Kisiwa Libobe na Mahurunga. Tunaomba sana walimu hao, basi sisi wa Mtwara Vijijini msitusahau. Narudia kusema nyinyi watu wa Serikali mna kawaida Mtwara Vijijini kuonesha mgongo kama Waislam. Maana Waislam wanaposwali, macho huangalia kaskazini tu, Kusini huku kuonesha mgongo. Hata akiwa ugenini anauliza jua linatokea wapi ili Mashariki aweke bega la kulia, Magharibi aweke bega la kushoto, Kusini aonyeshe mgongo, Kaskazini iwe kibra. Muislam yeyote na popote pale Kaskazini lazima aonyeshe macho, Kusini kuonyesha mgongo na Serikali mna kawaida hiyo hiyo Kaskazini kuonyesha macho na Kusini kuonyesha mgongo. Ninawashaurini sana safari hii onyesheni Kusini macho, Kaskazini muonyeshe mgongo? *(Kicheko/Makofi)*

Suala la mwisho ni kuhusu ndege ya Rais. Mimi siku moja nilifanyiwa mipango nikapanda ndege ya Rais kutoka Dodoma kwenye Bandari ya Salama. Nilikuwa na kaka yangu Mheshimiwa Lutavi. Moshi uliokuwa ukitoka kwenye ndege ile na mngurumo mbaya, nikamwuliza kaka yangu Lutavi; “Ama kaka tutafika lakini safari hii?! Akasema ah, tutafika. Nikauliza *che kaka* yuko humu humu kufanyaje? Akasema tuombe Mungu tu. Maana tulikuwa naye Rais mle mle. Yaani ndege ile hata ukinipa mimi kutembelea kwenye Jimbo langu kwamba mnampa Mbunge wa Mtwara Vijijini siitaki, mbovu! Sina haja nayo kabisa! Kwa sababu siku ile tulipofika salama, basi sipandi tena ndege hiyo. Sembuse Rais anayepanda kila siku! Suala la kununua ndege haraka ni muhimu sana, tena ikiwezekana Waziri wa Fedha ukitoka hapa kesho mipango hiyo ifanyike kama hela zipo, keshokutwa ijayo tuione ndege ya Rais pale. Ile haifai!! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Haya niliyoyasema naomba sana yazingatiwe na kurekebishwa, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja hii ya Waziri wa Fedha kuhusu Nyongeza ya Bajeti. Awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake pamoja na wataalam wote kwa kazi nzuri waliyoifanya. Pia napenda niwapongeze Wabunge waliochaguliwa kuiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika pamoja na SADC na vile vile kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naafiki kabisa sababu ambazo zimefanya iandaliwe Bajeti ya Nyongeza. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, ningependa nichangie katika maeneo yafuatayo kwa lengo la kuboresha Bajeti hii. Kwanza kabisa, naomba niungane na wale Wabunge ambao wanaona Shilingi bilioni 10,000/= kwa ajili ya kununua chakula haitoshi kabisa. Kwa sababu ukweli ni kwamba jinsi tunavyokusanya takwimu zetu kuhusiana na watu waliopatwa na njaa au walioathirika na njaa haziridhishi, njia tunayotumia kidogo ni ya ubabaishaji. Sisi ambao tumepata nafasi ya kuangalia maeneo mengi tunaona kabisa kwamba karibu maeneo yote ya Tanzania yana matatizo ya njaa hasa kwa kipindi hiki. Kwa hiyo, ni muhimu kwamba Mheshimiwa Waziri aangalie, achote mahali pengine ili suala hili la njaa lishughulikiwe kwa ukamilifu zaidi. Pili, utaratibu wa kugawa na kusambaza chakula unazo kasoro zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa kawaida watu wenye njaa hawana fedha. Sasa huku nyuma pamekuwa na maelekezo kwamba eti Serikali inasambaza chakula na kuwauzia watu wenye njaa kwa bei nafuu. Hivi kweli mtu akiwa na fedha atashindwa kununua chakula? Mimi naona hili jambo ni la ajabu kidogo. Kwa ushauri wangu ni kwamba hawa watu wapelekewe chakula. Wakishashiba, ikibidi waambiwe wafanye kazi lakini kutegemea kwamba wanaweza kununua, ni jambo ambalo kimantiki haliwezekani hata kidogo.

Pili, kwa kawaida tunapowatumia wafanyabiashara kusambaza chakula kwa watu walioathirika ni kweli kwamba chakula kile hakitawafikia, badala yake wafanyabiashara watakwenda kuuza au wavatipeleka mahali ambapo kuna fedha na maeneo haya ni Mijini na wakati mwingine upo ushahidi kwamba baadhi yao hata wanatoa chakula hiki kwenda kukiua nje ili waweze kupata fedha. Kwa hiyo, mimi ningeshauri kwamba suala la kusambaza chakula liwe ni suala au la Serikali yenyewe au kutumia baadhi ya Mashirika kama ya Dini au hata Taasisi zisizo za kiserikali. Lakini la msingi ni kwamba suala hili kwa kweli liandaliwe kwa misingi ya operesheni kuliko hali inavyoendeshwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niseme wazi kabisa kwamba pengine sasa Tanzania tufikie mahali tujifunze. Huu ni wakati muafaka wa kujifunza kwamba sisi maji tuliyokuwanayo yanatosha kwa ajili ya kumwagilia na kupata chakula, yanatosha kwa ajili ya mifugo, yanatosha kwa ajili ya shughuli za viwandani pamoja na matumizi ya binadamu. Lakini lazima tukubali kwamba maji haya hayatoshi kwa ajili ya umeme. Kwa misingi hiyo basi, nataka niungane na wenzangu wanaoona kwamba suala la umeme katika nchi hii halijapewa kipaumbele. Suala la nishati, hatujaliweka hata katika yale mambo muhimu. Mimi sijawahi kusikia nchi yoyote duniani hapa iliyoendelea bila umeme wa uhakika na umeme wa uhakika katika nchi hii hauwezi ukatokana na maji kwa sababu hatuna uhakika na mvua.

Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba Mheshimiwa Waziri atuambie hapa hapa, tuna mkaa mwingi katika nchi hii wa uhakika, nadhani katika Afrika sisi ndio tunaongoza. Kuna Mradi wa Mchuchuma, unasubiri nini? Ninaambiwa kuna watu wababaishaji hawaamini kwamba umeme wa mkaa ni safi, wao wanaamini kwamba umeme safi ni wa maji. Mimi nadhani watu wa namna hii kwa kweli pengine hawatufai. Ndiyo! Hawatufai, naomba Serikali ielewe suala hili kwamba suala la umeme liwe ni la kufa na kupona katika nchi hii. *(Makofi)*

Lakini vile vile tatizo hili la umeme limetoa faraja kwa maana kwamba nchi nzima sasa inaliona kwamba ni gumu, ni tatizo. Lakini inapofika kwa Wilaya na Mikoa ile ambayo haina umeme hawalioni. Mimi naomba na hili mlione. Watu wa Mbinga wanahitaji umeme, watu wa Namtumbo wanahitaji umeme

na watu wa Kigoma wanahitaji umeme wa uhakika. Lakini jawabu litakuwa ni moja tu, tupate umeme wa uhakika kutoka Mchuchuma na mimi nasema, ni wakati muafaka sasa tuachane na matumizi ya anasa. Semina kila siku, hazitupeleki popote! Magari ya anasa, gari analotembelea Mkurugenzi wa Idara linakuwa la anasa zaidi kuliko la Waziri, jamani tutafika wapi? Hivi kweli kila mwaka tununue magari?! Ni lazima tufikie mahali kwamba hizi fedha zitumike kwa mambo muhimu yatakayoliokoa Taifa letu. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nataka niseme wazi kabisa hapa kwamba kama Mheshimiwa Waziri hatatueleza sawasawa kuhusu suala hili la umeme wa Mchuchuma, Bunge la Bajeti mwaka huu litawaka moto. *(Makofi)*

Umeshasikia Makofi hayo, nina hakikisha kabisa tutafanya kazi kuhakikisha kwamba suala la umeme linapewa *priority number one*. Hili niko tayari kusamehe hata hela za Ukimwi kwa sababu kwa namna moja ni kitu ambacho tunaweza tukaepuka, lakini suala la nishati ni la msingi sana katika sayansi na teknolojia, elimu na katika kuhakikisha kwamba hali ya Watanzania inakuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa niseme jambo moja tu, nalo ni kuhusiana na suala la Daftari la Kudumu la Wapiga kura. Zoezi hili ni muhimu pamoja na suala la vitambulisho vya raia, lakini linapaswa kuangaliwa na kutekelezwa kwa uangalifu mkubwa sana hasa ikizingatiwa kwamba nchi yetu sasa hivi imevamiwa na wahamiaji haramu wengi sana. Kutokana na hali yetu hii ya kupenda hela ndogo ndogo, si ajabu kwamba tutajikuta ni watu wa kwanza kupata hivi vitambulisho wakawa watu ambao sio raia. Kwa hiyo, mimi ningeshauri kwamba kazi ya kufanya, tathmini ya kuwabaini wahamiaji haramu, lianze mara moja na liwe la kudumu. Mimi nashauri, sasa ni wakati muafaka kwamba sheria iandaliwe ambayo wale ambao wataonekana wamedanganya wao ni raia wa nchi hii, wachukuliwe hatua na wanapokamatwa wacharazwe bakora na kutimuliwa katika nchi hii mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kusema kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda na mimi jioni hii nitoe shukrani zangu kwako kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie katika hoja ya nyongeza ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2003/2004. Baada ya kukushukuru, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Ndugu yetu Basil Pesambili Mramba, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara ya Fedha, hususan hatua hizi wanazozichukua kukabili mapungufu yaliyoko katika nchi yetu katika Bajeti yetu. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Lakini niwapongeze zaidi viongozi wa *TRA* kwa kazi nzuri ambayo wamefanya katika kukusanya mapato mpaka tukapata na ziada ambayo leo sisi Wabunge tumepata nafasi nzuri ya kuidhinisha matumizi pasipo mapato yanayotupeleka kuingilia katika mifuko ya Wapigakura wetu. Nawapongeza sana ndugu zangu wa *TRA*. Napenda niwaombe waendeleo na juhudi hizo za kuweza kutoa mchango wao kwa kuongeza mapato na uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Pia nimpongeze Mheshimiwa Profesa Martin Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, kwa ufafanuzi mzuri alioutoa wa manunuzi ya ndege ya Serikali na tunaomba nchi nzima ijue ufafanuzi huo ndio ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nichukue nafasi hii sasa kuchangia Muswada au hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza napenda kuungana na Wabunge wenzangu wote ambao wamechangia Muswada huu na kuunga mkono na mimi naungana nao katika hoja zao mbalimbali walizozitoa na nisingependa kurudia kwa sababu nathamini sana na kuheshimu mchango yao hiyo.

Mimi mchango wangu utakuwa kwa sehemu kubwa, sehemu ya kuitahadharisha Serikali na kuishauri hasa katika upande wa njaa, nishati na Daftari la Wapigakura. Ningependa kuangalia suala la njaa na nishati kwa upande wa mazingira ya nchi yetu. Mazingira ya nchi yetu yameharibika mno kwa kukatwa ovyo kwa misitu, kuharibu vyanzo vya maji na sasa tunaingia katika gharama ya *supplementary*

*budget* kwa sababu ya mazingira kuharibika. Watu wamekuwa huru mno kuchoma mkaa katika maeneo mbalimbali. Kule katika Jimbo langu, watu wa Arusha na Moshi wanahemea mkaa kule kwangu na hii imetuletea mazingira magumu sana na hata kutusababishia mafuriko.

Serikali lazima iingilie kati hii biashara ya mkaa maana sasa haiishii katika maeneo ya nchi yetu tu. Zipo habari za kuaminika kwamba mkaa unachukuliwa Tanzania unapelekwa nchi jirani ya Kenya unasafirishwa unapelekwa Dubai. Ningeomba Serikali ilianganalie sana hilo, mazingira yetu yanaharibika kwa kasi kubwa sana na hali hiyo itatufikisha mahali pagumu. Hii hali ya njaa ni *outcome* ya uharibifu wa mazingira, upungufu wa kina cha maji kwa ajili ya kutupatia nishati ni *outcome* ya kuharibu mazingira. Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali pamoja na kutuletea hii *supplementary budget* ikaangalie *primary cause* ya matatizo yaliyotufikisha hapa. *Primary cause* yake ni kuharibu mazingira.

Sasa nije kwenye suala la njaa lenyewe. Suala la njaa kwa watu wetu ni kubwa sana. Kwa sababu kule Vijijini taarifa zinazoletwa Serikalini mimi nafikiri hazikukamilika sawasawa kwa sababu Wakuu wa Wilaya na hao wanaokwenda kufanya *survey* wanakuwa na hofu. Wanaambiwa, wewe kwa nini katika Wilaya yako kuna njaa, utawajibika. Anaogopa anaweza akaitwa na Waziri Mkuu akawajibishwa. Sasa hatuelezi hali halisi ya njaa na hii ndio sababu hata mwanzoni tumeweza tukakadiria kwamba tuna upungufu wa chakula ambao haukuwa sahihi. Mahindi yanauzwa ghali mno, gunia sasa linafikisha kati ya Sh.36,000/= mpaka Sh.40,000/= kwa hiyo chakula sio *affordable*, haiwezekani tena bei yake.

Sasa mimi ningependa Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea hii *Supplementary Budget* atuambie ni vipi atapambana na kushusha hii bei kutoka Sh.40,000/= ifike bei ya kawaida ambapo chakula kitakuwa *affordable* kwa watu wetu. Kiwe *available* na *affordable*, vinginevyo tutakuwa tunasema tunapambana na njaa lakini je, watu wetu wana uwezo wa kununua hicho chakula?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri aje atupatie ufafanuzi vizuri vinginevyo kati ya sasa mwezi wa Pili na wa Sita isije ikawepo *Supplementary Budget* nyingine tena, tutakuwa kioja. Kama watu hawana chakula wanakufa, lazima Serikali itafanya maneno, lakini kitakuwa ni kioja, *Supplementary Budget* mbili kwa mwaka mmoja wa fedha sio kitu cha kawaida. Kwa hiyo, tukaangalie kama hizi fedha hazitoshi, ni vyema zikaongezwa. Mimi ningeomba Serikali iwe na mpango wa ku-*flood the market* ili bei ishuke kwa sababu bei iko juu sana. Tusipofanya hivyo, watu wetu wataendelea kupata shida, sisi tunaongea hapa kwamba tunakwenda kupambana na njaa lakini watu wetu wataendelea kuwa na njaa. (*Makofi*)

Pili, tunasema njaa iko maeneo fulani tu, mimi siamini. Kama ni maeneo fulani tu ni kidogo, sehemu chache tu hazina njaa lakini njaa hii iko kila mahali na inam-*affect* kila Mtanzania. Kweli tunatofautiana lakini kwa wananchi tunasema wananchi walioko mabondeni, hao wana njaa, walioko katika milima hawana njaa lakini mimi katika Jimbo langu kule vilimani na huku bondeni wote wana njaa tena njaa ya vilimani ni mbaya zaidi hasa kule kwetu kwa sababu usafiri ni mgumu. Kwa hiyo, ningeomba hilo likaangaliwe lisije likawa tunasema njaa hii ni kwa maeneo fulani tu na maeneo fulani hamna njaa.

La tatu, pamoja na hali ya njaa tuliyo nayo, Wizara ya Kilimo ijizatiti kabisa katika kuwawezesha wananchi katika kilimo sasa hivi. Vinginevyo mwaka wa fedha mwingine tena tutaongea habari ya njaa. Tusingependa hii hali ya kuongelea njaa ikaendelea kuwepo. Tunayo mito mingi, tunayo raslimali kubwa ya kuvuna maji ya mvua, kuwawezesha wananchi kwa mbegu, ningeomba Wizara ya Kilimo sasa iwe karibu sana na wakulima ili kuwawezesha pamoja na msaada huu wa kukabili njaa, sasa baada ya hapo wananchi wawe wamejikomboa na baa la njaa kwa kujitegemea. Wakati huu mvua zinaponyesha, basi itakuwa vizuri Wizara ya Kilimo ikalifuatilia hili kwa karibu sana.

Lingine ni changamoto kwa Wizara yetu ya Kilimo na Chakula. Inaitwa Wizara ya Kilimo na Chakula, lakini chakula hakuna. Sasa inapoteza ule uzito wake wa kuitwa Wizara ya Kilimo na Chakula wakati chakula hakipo, uwezo wa chakula haupo. Unaitwa baba kama kweli wewe baba unafanya mambo ya ubaba! Sasa kama huna chakula bado unataka kuendelea kuitwa baba, utaitwa baba kwa sababu gani? Mimi ningeomba Wizara iweke mpango kabambe wa kuhifadhi chakula. Nchi tajiri kama Marekani, Urusi, wana hifadhi ya chakula cha kuwa-*sustain* miaka 50, sisi nchi maskini hata cha miezi sita hatuna. Hii ni hatari kwetu kabisa. Nchi tajiri zina hifadhi ya chakula kubwa na sisi tuna Wizara ya Kilimo na

Chakula, tunaomba ianze kuweka mpango kabambe wa kuweka chakula cha kututosha hata miaka kumi kwa kuanzia, kuliko baa la njaa linapotokea tunaanza kuitana hapa na kutafutana kwa sababu hatuna akiba. Silaha kubwa ya maskini ni kujihami. Matajiri hawajihami kwa sababu wana uwezo mkubwa, sasa sisi maskini lazima tujihami. Matajiri wanaweka chakula cha kuwalinda miaka 50, sisi hata miezi mitatu hatuna. Hii ni hatari kubwa sana. *(Makofi)*

Wakati mwingine wao, kwa hiyo hifadhi yao kubwa, wakati huu wa njaa sasa tunaletewa na chakula ambacho hakina hata *test*, lakini Mkemia kule amekipitisha kwa sababu mwenye njaa hana *choice*. Ule mchele ulioletwa Dar es Salaam watu hawauchukui kwa sababu hauna ladha. Wakati fulani tulipopata uhuru tulioletwa mahindi ya miaka mingi iliyopita. Yale mahindi yalikuwa hayana *test*, lakini tulikula, ile *yellow cone*. Sasa inawezekana na mchele huu unaoletwa utakuta pale juu ya kigunia umeandikwa chakula kile kilivunwa mwaka 1952 au labda mwaka wa 1940, au labda mwaka wa 1960 ndio kinaletwa kwetu. Lazima tukaliangalie hilo, ni njaa kweli lakini tuwe na mipaka.

Kwenye nishati, utunzaji wa mazingira utatusaidia sana kuhifadhi vyanzo vya maji na vina vya maji ili kuendelea na hali ya kutegemea umeme huu wa maji. Najua sio rahisi kwa Serikali kwa mara moja kuanza kubadilika na kutumia umeme wa mkaa, gesi na *uranium*, lakini sasa Serikali ianze kuchukua hatua taratibu za kuanza kutumia umeme wa *uranium*, iko kule katika Mkoa wa Ruvuma nyingi tu.

Tunao mkaa, tunayo *gas*, tuanze kutumia huo umeme taratibu, tungeomba katika mwaka wa fedha ujao tukiletwa tukaelezwwa kwamba Serikali imeanza na mradi upi taratibu ili tusingie katika matatizo hayo.

Lakini la mwisho, tumekubali mageuzi ya uchumi. Tukubali vile vile mageuzi ya kubadilika na mazoea, mazoea kwamba njaa ikitokea tunaleta *Supplementary Budget*. Hayo mazoea tuyaache. Kuna waimbaji fulani wa wimbo walikuwa wanasema mazoea ni taabu. Wasukuma wanasema: "*Nduh'u taabu.*" Mazoea ni taabu. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa tusikubali hii ikawa ni mazoea kwamba njaa sisi ni jadi yetu, hapana. Lazima tuachane nayo. Tukubali mageuzi ya kuachana na mazoea. Tuseme ya kutumia umeme wa maji tuachane nayo, tuanze kutumia umeme mwingine, labda wa *gas* au *uranium* au makaa taratibu. Mazoea ya kuharibu mazingira tuachane nayo taratibu na tukifanya hivyo nafikiri tutakuwa tumeweka nchi yetu katika hali nzuri ya kuweza kuhimili hata wakati wa matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara ya Fedha na mimi naunga hoja yake mkono asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kwa hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta hoja hii muhimu sana. Imefika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mwakilishi wa ajabu nisimame mbele yako, nipinge hoja ya msingi kabisa ya kuokoa wananchi, ya kuufanya uchumi wetu uweze kusimama usitetereke na kupinga jambo lililokwisha pitishwa kwenye Bajeti iliyopita kununua ndege ya Serikali na sasa Serikali inatekeleza, leo hii nipinge! Nitakuwa mwakilishi wa ajabu sana. Mimi naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu inafanya makubwa sana. Serikali inatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, kwa upande wa barabara, kwa upande wa elimu, kwa upande wa afya kupitia Mfuko wa *Basket Funding* kero nyingi zinatekelezwa. Mimi naipongeza Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja ningependa niongelee juu ya kuongeza fedha kwa upande wa elimu ili vijana wetu waliofaulu wengi wa darasa la saba, waweze kuingia *Form One*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya elimu nchini mwetu kidogo inatetereka, ingawa *MMEM* imefanya makubwa sana, uandikishaji umeongezeka, madarasa yanakarabatiwa, nyumba za walimu zinakarabatiwa na watoto wanafaulu sana. Hapo hapo naipongeza Serikali kwa kufuta ada ya Shule za Msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uboreshaji wa *MMEM*, watoto wengi wanafaulu mitihani na watoto wengi wanashindwa kuendelea kutokana na ukosefu wa nafasi na kazi ya ujenzi wa Sekondari, kazi yote imeachiwa wananchi. Wananchi wanajitahidi lakini wanakwama kwa mambo yaliyo nje ya uwezo wao, kama mabati, *cement*, nondo na rangi.

Kwa hiyo, wakati umefika Serikali inabidi iunge mkono wananchi kwa kuwasaidia vitu vile wanavyoshindwa kuvipata, kama tukiwaachia kazi hii ngumu ya ujenzi wa Sekondari wananchi peke yao, itachukua miaka mingi sana kukamilisha programu ya kuwapeleka watoto Sekondari asilimia 50. Kwa hiyo, ni vema Serikali ikaangalia hilo, ikasaidia nguvu za wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, shule ni majengo, walimu, vifaa na wanafunzi. Serikali imefanya makubwa kwa upande wa majengo, wanafunzi. Lakini, walimu wetu wa Shule za Msingi wanaofundisha, wana malalamiko juu ya malimbikizo yao ya pesa kwa upande wa *arrears* za mshahara, uhamisho na haki zao wakati wanapokwenda likizo ya malipo hawajalipwa kwa miaka mingi sana. Kwa hiyo, ili walimu waweze kuwa na mori ya kufanya kazi vizuri, naungana na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, aliyeishauri Serikali iangalie malimbizo ya walimu, iwalipe walimu ili walimu wawe na moyo wa kuwaelimisha vijana wetu ipasavyo.

Sasa nje kwenye hoja iliyopo mbele yetu ni juu ya njaa. Ni kweli nchi yetu imekumbwa na njaa. Ni kweli Serikali imechukua hatua nzuri za kutatua hilo tatizo na ni vema tukaelewa wazi sababu kubwa ya hali hii ni nini. Sababu kubwa ni kwamba kilimo chetu tunategemea mvua tu. Kama mvua haipo tunahangaika. Mwaka 2003 tulipata matatizo ya mvua kidogo, imetufikisha hali hiyo. Je, kama nchi nzima ingekuwa na ukame hali ingekuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vema Wizara ya Kilimo na Chakula iwe na programu kamambe ya kuangalia itajihami vipi huko mbele. Itajihami vipi, tuendelee kutegemea mvua? Ni lazima Wizara ya Kilimo na Chakula, iwe na mpango wa kuvuna maji ya mvua yote nchi nzima. Tuwe na mabwawa ili kilimo chetu kisitegemee mvua tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili maji katika nchi yetu yanapungua mwaka hadi mwaka na kilimo hakina njia nyingine, hakina nyenzo nyingine yoyote inayotegemea bali ni maji. Kwa hiyo, ni wakati umefika Serikali ihakikishe maji yote ya nchi hii yatumike kwa kilimo, kwa wanyama, kwa viwanda na matumizi ya nyumbani. Umeme una vyanzo mbadala. Ni vema umeme usitegemee sana maji. Sasa wakati umefika mipango ya kuondokana na umeme uliozalishwa kwa maji hatua kwa hatua, inafaa tubadilishe, ili tutumie vyanzo vingine kama mkaa wa mawe wa Mchuchuma, *gas*, upepo na vyanzo vingine kama jua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tusipofanya hivyo, Serikali yetu isipojihami katika hilo tutafikia mahala kama tutapata ukame kwa mfululizo miaka mitatu, hali ya nchi yetu itakuwaje? Wanaochelewesha mradi wa Mchuchuma watuambie ikiwa litatokea hilo watu tutajihami vipi, uchumi wetu utakwendaje? Tutaweza kuishi vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mengi ya kusema, bali ningependa sana Serikali yetu ianze kujihami katika tatizo la kilimo. Ianze kuweka programu ili kilimo chetu kisitegemee sana mvua, bali itegemea sana kilimo cha umwagiliaji na hilo kama litafanyika vizuri na mipango ikasimama vizuri, nchi yetu itaweza kuwa na chakula cha kutosha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. DAMAS P. NAKELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa nafasi hii jioni hii ya leo kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza



kusimama katika Ukumbi huu mwaka huu, napenda nikutakie wewe mwenyewe Naibu Spika na Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wananchi wote kwa ujumla, kheri ya mwaka mpya wa 2004. (*Makofi*)

Vile vile napenda nimpongeze Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuleta Muswada huu ulioko mbele yetu na mimi nasema ni wakati muafaka kwa Muswada huu kuwa mbele yetu ili tuweze kuinusuru nchi yetu katika hali ambayo ina-*prevail* katika nchi yetu, hali ya hatari, hali ya njaa na mimi bila kupoteza wakati, napenda niseme naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbele yetu tunao Muswada, Serikali inatuomba kuidhinisha mapendekezo yake ili iweze kukabiliana na hali ya njaa nchini, iweze kulipia gharama za umeme, iweze kununua ndege ya Serikali, iweze vile vile kugharamia matatizo yanayotokana na wanafunzi kuwa wengi waliofaulu mwaka huu ambayo ni hali tunayoipongeza kwa sababu hiyo ni kazi nzuri ya utekelezaji wa Sera ya Chama chetu cha Mapinduzi ya kuboresha hali ya elimu katika nchi yetu. (*Makofi*)

Lakini vile vile mbele yetu kuna hii *Supplementary Budget* kwa sababu ya kushughulikia suala la mafao na fidia mbalimbali zinazotokana na kodi zilizofutwa na Serikali. Lakini vile vile kuna Daftari la Wapiga Kura. Kwa hiyo, masuala haya yote ni masuala muhimu katika nchi yetu ambayo yanapaswa kushughulikiwa ili Serikali iweze kufanya kazi yake ipasavyo.

Mimi la kwangu ni moja na kwa kweli sitapenda nichukue muda mrefu kwa sababu zaidi tutakuwa tunarudia rudia. Lakini hata hili ninalotaka kulizungumzia la chakula, napenda tu nitilie mkazo katika hali nzima ya upungufu wa chakula. Lazima tuisisitize ili kuonyesha kwamba kwa kweli suala hili ni zito sana katika nchi yetu na lazima tulikabili vilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina tatizo katika eneo hili la njaa, chakula cha njaa. Tunapopitisha ongezeko hili la shilingi bilioni 10 katika hii *mini-budget* tuliyoletewa na Serikali mimi bado nafikiri Serikali haiko makini vya kutosha kwa sababu bado kiasi hicho, siamini, kama kinatosha. Najaribu kuona kwamba Serikali vile vile ina kasi ndogo katika kulishughulikia suala hili. Nitoe mfano katika Wilaya yangu na hususan Jimbo langu la Babati Magharibi.

Tangu mwaka 2003 suala la njaa lilipoanza kuzungumzwa tumepata tani 236 tu. Leo hii ninapozungumza tunatarajia kupewa tani 95 peke yake. Tani 95 tu. Lakini mahitaji halisi ni zaidi ya tani 400. Sasa hivi tunapozungumza hali ni mbaya, hali ya chakula inatisha. Lakini bado tunaenda katika kasi kama hiyo. Tani 95 itatosha kitu gani, nani apewe na nani asipewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, itakuwa ni suala la mjanja au suala la kuzidiana akili. Basi tuseme na hiyo ni *challenge* kwa Serikali katika ngazi ya Wilaya kwa sababu inashindwa kugawa pamoja na hali ambayo vile vile mimi naiona ni ya wasiwasi katika suala zima la *handling* ya ugawaji wa chakula katika Wilaya.

Labda vile vile nizungumzie suala la udhaifu katika *handling* ya ugawaji wa chakula katika Wilaya na nikizungumzia Wilaya yangu ya Babati ni kwamba nina wasi wasi kama kweli kuna uratibu ulio wa makini kama kweli kuna ufuatiliaji wa hali halisi ya chakula au hali halisi ya njaa. Inaonyesha hakuna vile vile ushirikiano wa dhata na uwazi katika ngazi zote kuanzia Kijiji, Kata hadi Wilaya.

Kwa hiyo, hakuna *co-ordination*. Unaweza kukuta mahali penye njaa zaidi pakaachwa. Lakini ukweli ni kwamba leo hii tunapozungumza kila mahali katika jimbo langu la Babati Magharibi kuna njaa. Lakini *approach* ya kutatua tatizo hili hairidhishi kabisa na mimi nafikiri inaweza kuwa ni *typical* nchi nzima. Lakini hali kwa kweli hairidhishi, ndiyo maana kilio cha njaa ni kila mahali sasa hivi katika nchi yetu.

Vile vile wahusika wanaoweza kusaidia katika suala hili hawaonekani Wilayani, hawaangalii vizuri ipasavyo. Kwa mfano tena nazungumzia Jimbo langu la Babati Magharibi kwamba kuna watu kwa kweli wenye mapenzi mema, wanaopenda kusaidia, lakini katika orodha nzima ya watu wanaoshirikishwa katika suala zima la kushughulikia chakula hawapo, wala hawafikiriwi.

Nichukue mfano wa Padri mmoja Mjerumani anaitwa Artfrid Wachtel, ni Paroko katika Kata moja inaitwa Riroda. Anafanya kazi kubwa sana ya kusaidia wananchi wa eneo hilo linalozunguka Kata hiyo. Na anagawa unga wa mahindi baada ya kuwa amenunua mahindi ameona namna ya kurahisisha hawa watu ambao ni walengwa wakafikiwa na mahitaji yao hayo ni kusagisha yale mahindi na kuuza unga ule wa mahindi kwa shilingi 150 kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika na anafanya kilo mbili kwa kila mwananchi pale kwa ajili ya chakula kwa siku anahudumia watu 2,000. Lakini mtu kama huyu hajaonekana mbele ya uongozi wa Wilaya. Leo hii ameishiwa chakula, mahindi hayo. Wananchi bado wanamfuata pale. Lakini hana cha kufanya. Yale ya mgao yanayoletwa na Serikali hayamfikii yeye na wanapogawia wafanya biashara ili nao wakagawie wengine yeye hawamfikiri.

Kwa hiyo, kwa ujumla anayelengwa katika suala hili ambaye ni mwana kijiji au mwananchi mwenye kuathirika na njaa hawezi kufikiwa kwa sababu *mechanism* inayotumika siyo sahihi. Haina ushirikishwaji katika ngazi mbalimbali, ngazi ya Kijiji, ngazi ya Kata, ngazi ya Wilaya na watu kama hawa ambao nimewataja kama huyu Padri. Padri Wachtel na nachukua nafasi hii kumpongeza, nazidi kumtia moyo kwamba aendelee na hata ikibidi mwenyewe afuatilie Wilayani kujishikiza pale ambapo anaweza akapata mgao huo naye awasaidie hawa wananchi ambao kwa kweli wamemzunguka na anafanya kazi ile kwa kujitolea zaidi kuliko kujitafutia manufaa yoyote ya kibiashara.

Kwa hiyo, mimi nafikiri Serikali katika ngazi mbalimbali, katika Wilaya ni suala hilo la utekelezaji. Lakini katika ngazi ya juu ya Taifa ifanye kazi hii au suala hili la uhaba wa chakula ilipe umuhimu wa hali ya juu kabisa na kwamba suala hili la shilingi bilioni 10 liangaliwe upya. Wenzangu wengi wamelizungumza na ni dhahiri kabisa kwa *trend* hiyo au kwa mtiririko ambao nimejaribu kubainisha hapa kwamba tangu mwaka 2003 tumezungumza habari ya chakula na upungufu wake tumepata tani 236 tu na leo tunaambiwa tunapewa tani 95 tu badala ya mahitaji halisi ya zaidi ya tani 400. Kwa hiyo, nafikiri hii ni angalizo kwa Serikali. Serikali lazima ikae chini, iangalie upya kama suala zima la uratibu, suala zima la ufuatiliaji lizingatie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona hakuna sababu ya kuzungumza hayo mengine, kwa sababu la msingi ni chakula, watu walioshiba wanaweza kuzungumza habari ya elimu, wanaweza kuzungumza habari ya afya, watu walioshiba wanaweza kuzungumza habari ya umeme. Kwa hiyo, kwa kweli hili la msingi ambalo limeleta *mini-budget* hii basi tulitatie kwa umakini unaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naomba nirudie tena kusema naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi niweze kutoa mchango wangu kidogo katika kupitisha hii fedha ya nyongeza kwa ajili ya Wizara ya Fedha. Kwanza kabisa naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii, *mini-budget* ipite kwa madhumuni yote yaliyokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono na mimi nilikuwa naomba nizungumzie yafuatayo, nikianzia suala la chakula cha njaa:-

Kwanza, nilikuwa naomba niishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa hatua ambazo imeweza kuchukua kwa ajili ya kusaidia wananchi ambao wamekuwa wakipata matatizo ya chakula katika maeneo yetu nchini Tanzania. Naipongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa nizungumzie suala la kufanya tathmini katika maeneo ambayo yanakuwa yameathirika na upungufu wa chakula. Nakumbuka siku moja Wizara ya

Kilimo na Chakula iliwahi kutoa takwimu hapa ikielezea ni vipindi gani ambavyo nchi yetu huwa inapata ukame na matokeo yake kuwa na upungufu wa chakula. Kama walivyozungumza wazungumzaji waliotangulia, mara nyingi ni katika kipindi kinachoishia miaka ya tatu na nne. Sasa hili linafahamika lakini vile vile inaeleweka katika nchi yetu ni maeneo gani ya ukame ambayo mara kwa mara huwa yanakuwa na upungufu wa chakula.

Sasa katika haya maeneo mara nyingi Mkoa wa Dodoma huwa haukosekani, Singida, Shinyanga, baadhi ya maeneo ya Tabora, Mwanza, baadhi ya maeneo ya Arusha. Sasa kama haya maeneo tunayafahamu, nilikuwa nawaomba wale wanaotoa kazi ya kufanya uchunguzi ama kufanya tathmini ya maeneo yaliyoathirika basi ni vizuri wawe wanapita katika maeneo yote badala ya kupita katika maeneo fulani tu. *(Makofi)*

Wanapofanya namna hiyo, huwa wanasababisha kuleta manung'uniko katika maeneo ya jirani ambayo huwa hawapati chakula, kama alivyozungumza Mheshimiwa Leonard Derefa. Nikichukulia mfano wa Wilaya ya Manyoni. Wilaya ya Manyoni tuna Tarafa moja, Tarafa ya Itigi. Mara nyingi huwa inajitahidi sana kuzalisha chakula. Katika tathmini iliyokuwa imefanywa, ilionekana ile Tarafa ilikuwa na chakula cha ziada. Lakini katika hali hii ya upungufu wa chakula ni wazi kwamba wale ambao wanakuwa hawana chakula lazima watakwenda katika eneo ambalo linapatikana chakula. Kwa hiyo, huwezi ukatarajia kwamba pale ulipokuwa umefanya tathmini ya kuonyesha kwamba kuna chakula cha kutosha kikaendelea kuwepo tu pale pale, lazima kitakuwa kimechukuliwa na wale ambao wamefungukiwa na chakula. Hilo moja.

Lakini la pili katika utaratibu huu wa soko huria, hiki chakula tunachosema kipo cha ziada katika labda Wilaya fulani ama katika Tarafa fulani, kile chakula ni cha watu binafsi. Kwa hiyo, wana hiari kumwuzia mtu wanayemtaka, siyo lazima wakiweke ndani ya Wilaya au katika Tarafa kwa ajili ya watu walioathirika ndani ya Tarafa hiyo hiyo, haiwezekani. Kwa sababu wengi wanakuwa na mtazamo wa biashara. Kwa hiyo, unaweza ukakuta wamekiuza kwa watu wa nje ya Tarafa ama nje ya Wilaya ama nje ya Mkoa.

Kwa hiyo, matokeo yake yale matarajio ya kudhani kwamba kile chakula kipo katika lile eneo, yanakuwa hayapo. Kwa hiyo, ni vizuri maeneo kama hayo, tusiwe na dhana ya kwamba kwa sababu kulikuwa na chakula cha ziada basi kitakuwepo wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika upande wa chakula nilikuwa nataka niikumbushe Serikali kwamba ni vizuri Serikali itusaidie kusimamia ama kutuongoza kwamba tunapolima katika maeneo yetu mbalimbali basi tulime kwa kuzingatia na hali ya hewa katika maeneo yanayohusika. Nafikiri itakuwa si sahihi kwa maeneo kama ya Mkoa wa Singida ama Mkoa wa Dodoma ambao mara nyingi unakua na ukame tukataka kung'ang'ania kulima mazao ambayo hayaendani na upungufu wa mvua ambao tunakuwa nao mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hili halikuweza kufuatiliwa kwa karibu na watu wakaachwa tu kulima kama wanavyotaka tutaendelea kupata matatizo ya chakula mwaka hadi mwaka. Lingine nakumbuka mwaka jana mwezi wa saba wakati tunajadili Bajeti Wizara ya Kilimo na Chakula, ilikuwa imekuja na mpango wa kusema kwamba ilikuwa ipo tayari kusaidia kila Wilaya zao moja la biashara na zao moja la chakula. Sisi katika Wilaya ya Manyoni tulikubaliana kabisa katika Kikao chetu cha Madiwani tukakubaliana kwamba zao la biashara ambalo tunataka lisaidiwe na Serikali ni alizeti na kwa zao la chakula tukasema iwe mtama.

Lakini bahati mbaya, sijaona utekelezaji wa huo mpango. Sasa nilikuwa naomba labda Wizara ijaribu kuangalia huo mpango wake umeishia wapi. Basi kama walichelewa mwaka huu niombe basi mwaka ujao waweze kutekeleza mapema na maandalizi yafanyike mapema kama ni mbegu, kama ni pembejeo wahuwika waweze kupelekewa mapema ili waweze kulima na kuweza kufanikisha na kuondoa tatizo la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilikuwa naomba nizingumzie suala la umeme. Katika mjadala ambao umekuwa ukiendelea kuna mzungumzaji mmoja wa Kambi ya Upinzani alikuwa amejaribu

kutoa rai kwamba *TANESCO* isipewe hii ruzuku ambayo leo tunaiombea katika hii Bajeti ya nyongeza. Inawezekana *TANESCO* kama mashirika mengine kwa sababu yanaendeshwa na binadamu, binadamu wanaweza wakawa na makosa yao. Lakini cha msingi hapa tumeona kwamba tatizo la umeme limejitokeza kutokana na uhaba wa mvua na mabwawa yetu kupungukiwa na maji ya kuweza kuendesha mitambo ili tuweze kuzalisha umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tutakubaliana na wazo la kusema kwamba wasipewe ruzuku nafikiri tutakuwa tumajikanganya. Mimi nilikuwa nashauri wenzetu wakubali *TANESCO* wapewe, kwa sababu lazima tukumbuke kwamba Serikali yetu ama nchi yetu imefanya mabadiliko ya Sera za kiuchumi. Kuna mashirika yamebinafishwa wakati huo huo tunaitisha wawekezaji waje, sasa kama tutasema tunawanyima hawa pesa za ruzuku maana yake huu umeme hautapatikana na hawa tuliowauzia mashirika wataendeshaje shughuli. Tunaowaita waje kuwekeza watafanyaje shughuli.

Kwa hiyo, haya mafanikio ambayo tumekuwa tukitoa pongezi kwa wenzetu wa *TRA* kwa kufanya kazi nzuri lakini vile vile yanatokana na haya mashirika yetu ambayo tumeyabinafishwa kufanya vizuri hasa baada ya kuchukuliwa na watu binafsi.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba *TANESCO* wapewe ruzuku kama ilivyokuwa imeombwa. Lakini nilikuwa naomba nikumbushe kwamba suala la umeme limekuwa likilalamikiwa juu ya bei zake, si watumiaji wadogo bali hata kwa watumiaji wakubwa na vile vile ukitazama kumekuwa kukitolewa wito kwamba watu waachane na nishati nyingine kama zile zinazosababisha uharibifu wa mazingira kwa mfano kuni na mkaa na badala yake watumie umeme, sasa kama bei ya umeme itaendelea kuwa juu kwa kweli tutakuwa hatuwatakii mema hawa tunaotaka watumie umeme badala ya kuni na mkaa, hilo naomba waliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sasa hivi utaona kwamba unapotumia umeme ukitumia umeme zaidi unalipa zaidi badala ya kwamba yule anayetumia zaidi pengine angekuwa na nafuu fulani ili aweze kutumia zaidi na zaidi matokeo yake ukitumia zaidi unalipa zaidi kwa hiyo unakuwa kama unapata *disincentive* usitumie umeme sana. Naomba suala hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba sasa hivi kuna malalamiko ya bei ya mafuta kama vile *petrol, diesel* kwenda juu. Nafikiri kwa sababu tulishapitisha sheria ya kuanzisha chombo kinachoitwa *Energy, Water and Utility, Regulatory Authority (EWURA)*, je, haujafika wakati wa kuunda chombo hiki? Badala ya wananchi kuwa wanalalamika mitaani au kwa Wabunge tunakuja kulalamika hapa na inavyoonekana hakuna kinachosikilizwa. Tukiwa na hiki chombo si itakuwa ni vizuri kwamba tuna chombo ambacho tunaweza kukiuliza na nafikiri kinaweza kusaidia hawa watu wenye uwezo mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka kusema kwamba sisi katika Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara tulipata nafasi ya kukutana na wawekezaji mbalimbali. Kabla sijasema hilo, kwanza naomba niungane na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa ile rai yao ya kusema kwamba ni vizuri Serikali ingeangalia uwezekano wa kuendeleza mradi wa makaa ya mawe ili kuweza kupata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu ilipokuwa ikikutana na wawekezaji mbalimbali miongoni mwa mambo ambayo wamekuwa wakilalamikia ni umeme ambao hauna uhakika kwamba kiwanda kinaweza kikawa kinaendeshwa mara ukasikia umeme umekatika na wakati mwingine haujulikani utarudi wakati gani. Sasa tukiwa na matumizi ya umeme wa makaa ya mawe nina hakika kabisa kwamba hili tatizo la upungufu wa umeme tutakuwa tumeondokana nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini uendelezaji wa huu mradi wa makaa ya mawe tumekabidhi Shirika la *NDC* lakini je, hili Shirika la *NDC* linapewa fedha ya kutosha? *NDC* imepewa kuendesha mradi wa makaa ya mawe, imepewa kuendeleza *Mtwara Corridor* na vile vile imepewa kuendeleza *EPZ* lakini je, ni kiasi gani cha fedha ambacho wanapata?

Mwaka 2002/2003 wamepewa shilingi milioni 50 na mwaka huu tulionao pia wamepewa shilingi milioni 50 je, hizi fedha zinatoshwa wao kuweza kuendeleza hii miradi? Lakini na hizo zimewekwa pale zimeelezwa kabisa kwa ajili ya EPZ sasa fedha kwa ajili ya huu mradi wa makaa ya mawe ziko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifuatilia mjadala humu Bungeni inaonyesha Waheshimiwa Wabunge wote wanaunga mkono suala la kuendeleza mradi huu wa makaa ya mawe. Ni vizuri Serikali katika mwaka wa fedha ujao iweze kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza mradi huu wa makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba niishukuru Serikali kwa uamuzi wake wa kuongeza wanafunzi katika Shule za Sekondari lakini vile vile kwa kuongeza nafasi za Walimu na kutenga fedha kwa ajili ya mishahara ya Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nina ombi moja kwamba katika baadhi ya maeneo Walimu wanaoteuliwa kwenda katika vituo vyao baadhi ya Walimu na pengine niseme tu wengi huwa hawaendi, naomba Wizara ya Elimu itusaidie. Mpaka sasa kwa mfano katika Wilaya yetu ya Manyoni tuna Sekondari za Kutwa zilozojengwa sita lakini zote zina upungufu wa Walimu. Unaweza kuona katika magazeti inatangazwa kuwa Mwalimu fulani, Mwalimu fulani amepangwa kwenda shule fulani lakini ukifuatilia ni wachache sana wanaokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itusaidie kwamba pale Mwalimu anapokuwa hajaenda basi ijaribu kufuatilia kama alipangwa kwenda Manyoni kaenda mahali pengine akijulikana basi alazimishwe kwenda huko alikopangiwa badala ya mtu kuchagua anapotakakwenda au kama Wizara inaridhika kumwacha huko alikokwenda basi Wizara ipange mtu mwingine kwenda ambako yule mwingine amekataa kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Wizara ikifanya namna hiyo itakuwa imetusaidia sana vinginevyo kazi nzuri iliyofanywa na wananchi kujitolea kujenga hizi Sekondari itakuwa haina maana kama hatutakuwa na Walimu katika shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi kutoa mchango wangu kidogo na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili kuweza kuchangia Muswada wa Waziri wa Fedha. Labda tu kuweka kumbukumbu sahihi zaidi, Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Fedha na Uchumi wakati alipokuwa anatambua viongozi wa Wizara ya Fedha alisahau kumtaja Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Mama Mwantumu Malale na yeye alikuwepo na alitoa ufafanuzi mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe pongezi za dharti kabisa kwa Serikali yetu kupitia Wizara ya Fedha kuwa *proactive* katika kushughulikia matatizo ya wananchi. Wizara ya Fedha imeweza kutumia Bajeti kama chombo katika *management* ya uchumi. Hii inadhihirisha vizuri sana katika haya masuala yaliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo au changamoto ambazo Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla inawasilisha mbele yetu ni pamoja na hili suala la njaa. Kwa kweli maombi yaliyowasilishwa mbele yetu hayana ubishi, tatizo tunalijua na limeenea karibu nchi nzima, hii ni pamoja na Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 30 Januari, 2004 ilinyesha mvua kubwa sana ya mawe kule Kahama na katika baadhi ya maeneo imeleta athari kubwa katika mazao hasa ya tumbaku, pamba, mahindi na maharagwe. Katika Kata za Ulowa, Bulungwa, Uyogo na Igwamanoni athari katika mazao haya ni kubwa sana. Nitawasilisha maombi rasmi kwa Serikali kuweza kuona ni namna gani inaweza kushughulikia matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme na lenyewe linajieleza wazi wazi, tuna ukame na kama Serikali haingechukua hatua za dharura kuweza kubuni huo mkakati wa kutoa fedha za ruzuku ili kuwezesha uzalishaji wa umeme na ili kuwezesha uchumi kuendelea bila vikwazo vyovyote haya

mafanikio tunayojisifia ya mapato kuongezeka sana mpaka kufikia wastani wa shilingi bilioni 108 kwa mwezi, hatungeyapata. Hao wanaobisha kuhusiana na suala hilo ninawashangaa sana. *You can not have the cake and eat it.* Haliwezekani hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kushughulikia wanafunzi waliofaulu sana mwaka jana, ningependa tuliangalie kwa upana mkubwa zaidi. Ni kweli kabisa kwamba kutokana na mpango wa MEM mazingira ya kufundishia yatazidi kuboreka, walimu wa Shule za Msingi watazidi kuajiriwa wengi zaidi, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia vitazidi kuwa vingi zaidi kwa hiyo mazingira ya kufundishia kwa ujumla yatakuwa mazuri zaidi kwa hiyo, watazidi kufaulu sana. Ninashukuru kwamba Serikali inaandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) kuanzia mwaka ujao wa fedha. Hili ni jawabu tosha kwa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikichukulia tu kwa mwaka jana mfano Wilaya ya Kahama na sisi tunakabiliana na tatizo hilo hilo ambalo Kitaifa limejitokeza. Wilaya ya Kahama wanafunzi waliofanya mtihani wa Darasa la Saba kwenda Elimu ya Sekondari walikuwa zaidi ya 6,900 wakafaulu wanafunzi 5,007 lakini ambao mpaka sasa wameteuliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza ni 774 tu, asilimia 15. Tatizo hili kwetu Kahama ni kubwa zaidi maana inamaanisha zaidi ya wanafunzi 4,200 watakosa Elimu ya Sekondari kama tutakaa hivi hivi. Nashukuru sana Serikali inalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa takwimu hizi sio kwa sababu ninataka kukatisha tamaa, hata kidogo. Hata katika Wilaya ya Kahama tumekuwa tukitekeleza mpango wa kuboresha elimu chini ya mpango unaoitwa Operesheni Elimu ni Ufunguo wa Maisha. Tulianza mwaka 1999 tukiwa na Shule za Sekondari tano mpaka sasa ninapozungumza zipo Shule za Sekondari 12 na tunaendelea kujenga zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kwamba ili angalau tuchukue wanafunzi 500 au 600 waliofaulu waweze kuingia katika Elimu ya Sekondari sasa hivi tunatekeleza mpango wa kupanua mikondo katika baadhi ya Shule za Sekondari zilizopo. Vivyo hivyo tunajenga Shule za Sekondari mpya tano. Tunatarajia kwamba katika kipindi cha miezi miwili, mitatu ijayo tutakuwa tumezikamilisha ili kuwahi uteuzi wa pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote ni kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000. Ninashukuru sana na natiwa moyo na Serikali jinsi inavyolishughulikia suala hili.

Naomba basi, kwa mantiki hiyo hiyo kwa sababu uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ni mdogo sana katika makisio ya takriban shilingi milioni 64 ambazo tunahitaji ili kupanua huo uwezo mpaka ifikapo mwezi Mei, tunaiomba Serikali itufikirie kutusaidia kwa sababu matatizo ya Kahama ni ya kipekee. Aidha, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni katika wale Walimu wa ziada 18,000 ambao anatarajia kuajiri kwa kutumia huo mkakati asisahau Wilaya ya Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kutoa shukrani kwa niaba ya wastaafu hasa wale waliochukua malipo yao kwa mkupuo mmoja huko nyuma ambao sasa hivi wanarudishwa katika utaratibu wa malipo kama ambavyo Serikali iliahidi mwanzoni mwa mwaka huu wa fedha. Hii kwa kweli itasaidia sana. Nadhani ndio tafsiri pamoja na mambo mengine katika maombi haya ya pensheni ni pamoja na hao wastaafu.

Kwa kweli katika mazingira ambapo mapato ya Serikali yanaongezeka na malipo ya pensheni kwa wastaafu waliopo yanaboreshwa zaidi tutakuwa tunawatendea isivyo haki hao wananchi ambao ni Watanzania bado wako hai na wenyewe wanastahili kufaidika na matunda ya Serikali ya Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya kuunga mkono mapendekezo ya Wizara ya Fedha inatokana na suala la msingi kabisa kwamba yote yale ambayo Waziri wa Fedha amewasilisha hapa ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000 katika kutoa kero miongoni mwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fikiria kama Serikali ambayo inajali wananchi wake ingekaa hivi hivi suala la njaa nani angelishughulikia, si ni kero? Kama Serikali ingekaa hivi hivi pasipo kutoa fedha za kutosha kuwezesha umeme uendelee kuzalishwa si uzalishaji katika uchumi ungepungua? Hata mapato ambayo tunajivunia si yasingekuwepo? Kama Serikali ingekaa hivi hivi pasipo kushughulikia haraka iwezekanavyo kuwatafutia wanafunzi nafasi za kuendelea na Kidato cha Kwanza kweli tungekuwa tunawatendea haki hawa vijana? Haya yote ni katika kuondosha kero miongoni mwa wananchi. Kwa hiyo, mimi ninaunga mkono mia kwa mia mapendekezo ya Waziri wa Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashangaa sana wale wanaohoji kuhusu maombi yanayohusu ununuzi wa ndege. Nadhani wangekiri hapa kwamba kwa kweli huu ni uungwana wa hali ya juu wa Serikali ya CCM kuweza kuwasilisha hapa mbele ya Bunge lako Tukufu maombi ambayo kwa kweli huko nyuma tulishayakubali na kwa kweli hata *financing* yake ingefanyika kimya kimya. Lakini kwa sababu ni Serikali inayojiamini, ni ya uwazi na ukweli basi imeyaleta hapa. Hilo halina ubishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa napenda nitoe tahadhari, matatizo yetu kwa namna moja au nyingine, ni *reflection* ya *fragility* ya uchumi wetu yaani sijui tuko namna gani? Sisi katika uchumi wetu tukiwa katika mema tunahangaika katika matatizo ndio basi tena.

Napenda kuomba kwamba katika Bajeti ijayo ya mwaka 2004/2005 Serikali ijielekeze ipasavyo kuzidi kuimarisha uwezo wa uchumi wetu kuhimili misukosuko inayotokea katika uchumi wetu yaani zile *shocks*. Hii ni pamoja na kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema kuwa na umeme wa uhakika wa Mchuchuma na kuwa na kilimo cha umwagiliaji maji cha uhakika kwamba miaka 42 baada ya Uhuru bado tunaomba chakula ni aibu sana. Tunazungumzia kwamba *The Rufiji Basin* ni *bread basket* ya *East Africa*, lakini chakula hakipo tunazidi kuomba. Lazima tuimarisha uchumi wetu usiendelee kuwa unayumbishwa na matatizo mbalimbali hayo yanayotokea katika mazingira yanayotuzunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha. (*Makofi*)

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukupongeza na kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kidogo makisio haya ya dharura.

Vile vile nampongeza Waziri kwa kuchukua hatua inayofaa ili kurekebisha mambo ambayo yamejitokeza. Mimi nimepitia hoja iliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu, nimeridhika na hoja hizo, naunga mkono moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi ya kujadili masuala mawili, matatu. Moja, linahusu elimu. Kwanza niipongeze sana Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa maana ya Serikali vile vile kwa kuchukua hatua ya dharura labda nitoe mfano mdogo kwenye Wilaya yangu. Mwaka 2002 Wilaya yangu watoto wa shule za msingi walifaulu 40% lakini mwaka 2003 walifaulu 52%. Kutokana na uamuzi wa Serikali kuchukua hatua za dharura watoto 320 wameongezeka katika Wilaya yangu zaidi ya mwaka 2003. Hiyo ni hatua nzuri na kwa kweli naipongeza Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii hatua inachukuliwa kwa ajili ya kuajiri Walimu wapya wa Sekondari na kweli hili ni tatizo kubwa kwa sababu kuna masomo mengine hayana Walimu wa kufundisha. Lakini ninafikiri kwamba pengine utaratibu wa kupata hawa Walimu ingekuwa kwa kutoa matangazo yanayoeleza wazi wazi kwamba wewe ni Mwalimu una-*apply Secondary School* gani kwa hiyo anapoajiriwa anajua kwamba mimi nakwenda *Manda Secondary School*, nakwenda *Lugalawa Secondary School* kwa hiyo ana-*apply* kwenye shule hiyo lakini haya ya kutupangia anajua anaweza kupangiwa popote. Niliona wakati mmoja tulitumia kwa walimu *Primary School* walikuwa wana-*apply* kwenda Shule zile ambazo zimeelezwa kwa hiyo anakwenda kule kwa sababu ameomba, huo ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu njaa. Bahati nzuri Wilaya yetu ya Ludewa asilimia 75 ya wakazi wake hawana njaa lakini kuna Tarafa ile ya Mwambao na Tarafa ya Masasi kule Ziwa Nyasa zimepata matatizo. Kwa hiyo, nafikiri Serikali itachukua dharura sio ku-*assume* tu kwa sababu Wilaya ya

Ludewa imekuwa na neema ya chakula hii inaweza kutuletea matatizo. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ifikirie ndani ya neema kuna matatizo vile vile, naomba hilo lifanyike kwa kupeleka chakula huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wachina wana methali inayosema kwamba: “Ukitaka kumsaidia mtu usimsaidie samaki peke yake msaidie na nyavu ya kuvulia samaki.”

Kwa hiyo, nafikiri ni lazima Serikali iimarisha mambo matatu yafuatayo:- Kwanza iimarisha na kusimamia, utaratibu wa miaka ya nyuma, Wakoloni walianza kutenga maeneo kulingana na Jiografia na hali ya hewa ilivyo yaani mazao yalimwe kulingana na hali ya hewa ilivyo. Zamani wakati sisi tunasoma Darasa la Nne tulikuwa tunajua Dodoma ni maarufu kwa uwele, mtama sasa leo mahindi haya hayatatufikisha haya. Kwa hiyo, tuhakikishe Wizara inafanya utaratibu kuhakikisha kwamba tunalima kulingana na hali ya hewa, hii itatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ule utaratibu wa ruzuku ya mbolea ulioanzishwa na Serikali kwa Mikoa ya Nyanda za Juu za Kusini ilikuwa ni moja ya mpango mzuri sana wa kusaidia uzalishaji wa chakula katika nchi hii lakini una kasoro. Kasoro kubwa kabisa ni namna mbolea ilivyoweza kufikishwa kwenye vijiji. Ruzuku ya mbolea inatolewa kutoka Dar es Salaam hadi Makambako tu wakati Wilaya ya Ludewa iko karibu kilometa 200 kutoka Makambako utaratibu huu haitasaidia.

Sisi tulikuwa tunafikiri kwamba ili kuondoa njaa pengine ingekuwa vizuri wakasogeza huduma hii ya kugawa mbolea za ruzuku. Hivi sasa tuna lawama kubwa kwa sababu tulipita kwa wananchi, ni kazi yetu kuwaambia wananchi kwamba Serikali katika vikao vyake wameamua nini na tumewaeleza kwamba Serikali imeamua kutoa ruzuku katika usafirishaji wa mbolea lakini hawaoni tofauti. Juzi Mwenyekiti mmoja wa kijiji fulani alisema kwenye redio katika kipindi cha Majira kwamba Mbunge alitambua kwamba mbolea ya nafuu inakuja ni kweli kwa sababu hatukujua utaratibu huu wa kugharamia usafiri hadi Makambako tu. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ipeleke hiyo mbolea mpaka Wilayani angalau kama haiwezekani kufika kwenye Kata pale tutajua wenyewe tutabeba kwa mkokoteni au vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kitengo kile cha *SGR* kiimarishwe na kipewe uwezo mkubwa zaidi kuliko sasa kwa sababu sasa hivi kina-*limitation* hela zake ni kidogo sana. Nakumbuka walikuja Ludewa pale Mlangali watu walikuwa na mahindi mengi sana lakini *SGR* ilishindwa kununua yote.

Kwa hiyo, nadhani tupe uwezo wa fedha zaidi na naomba kabisa wangeweza kupeleka vituo vya ununuzi na sehemu nyingine kama zile sehemu za Mlangali, Mawengi hadi kufika kule Ludewa, Lugarawa na sehemu nyingine za Mavanga hizi ni sehemu ambazo zinazalisha mahindi kwa wingi sana lakini mahindi yake yanaoza huko huko na pengine wanapata bei mbovu. Kwa hiyo, tungeomba muimarisha hayo ma-*godown* yapo toka zamani yalijengwa na *KAJIMA* wakati ule wa *Japanese Food Counterpart*, kwa hiyo tunaomba hii ifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la umeme, pole sana, hiyo nasema pole kwa sababu tukiendelea kutegemea umeme wa maji kila siku tutakuwa na matatizo. Wenzangu wamelizungumzia sana lakini napenda kumpongeza sana kwanza Waziri wa Nishati na Madini wakati tunazungumza naye kwenye Kamati alionyesha dalili kwamba mradi huu unaweza kufanikiwa. Lakini sina budi vile vile kuipongeza Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati ya Miundombinu iliyotembelea mradi ule wa Mchuchuma kwa kweli wananchi wa Wilaya ile walipata imani kubwa kuona Wabunge wamefika sehemu ile kwa ajili ya kuwaunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunategemea Serikali kwamba itatazama tazama na hasa hotuba ya Mheshimiwa Rais iliwasimua sana wananchi wa Wilaya ya Ludewa na wengine wa Tanzania kwa kuelekeza, kazi ya Mzee ni kuelekeza, Mzee wa nchi hii ni Mzee Benjamin Mkapa, ameelekeza kwamba sasa ni mkaa wa mawe. Mheshimiwa Waziri tunakuomba sasa tuelekee huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nafikiri labda pana tatizo la vigezo vinavyotumika kufidia ruzuku ya Kodi ya Maendeleo. Kodi ya Maendeleo kwenye Wilaya zetu sisi wengine Wilaya hizi ndogo ndogo uchumi wake ulikuwa unategemea Kodi ya Maendeleo peke yake.



Kwa mfano, Wilaya ya Ludewa ilikuwa inategemea karibu asilimia 75 hadi 80 ya mapato kutokana na kodi. Kutokana na wigo mdogo wa mapato huwezi kupanua wigo wa mapato kwa sababu *that is a Rural District, agricultural*, halafu *population* ya watu ni ndogo lakini *complication* zake ni kubwa. Ni Wilaya ndogo yenye *poor communication system, potentials* za uchumi zipo nyingi kwa hiyo utakuta mapato yake yote yalitegemea sana Kodi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tungeomba Serikali ifanye maamuzi ya makusudi kuisaidia hii Wilaya tukitegemea kwamba tutapata maendeleo kwa ajili ya msingi huu wa fidia ndogo ya kodi ya maendeleo utakuta sisi Ludewa kila siku hatutapata maendeleo yoyote.

Kwa hiyo, tungeomba Serikali kwa kuwa sasa hivi wanafikiria namna ya kusaidia Halmashauri zote Wilaya ya Ludewa ingepewa fursa maalum kuziba pengo lile ambalo kwa kweli wana matumizi makubwa lakini mapato yao hata kama wakijitahidi namna gani haiwezekani. *A district with a population* ya watu 130,000, lakini eneo lilivyokuwa kubwa unatembea mapori na mapori. Kwa hiyo, tungeomba Serikali itupe nafasi maalum kabisa katika hilo la kufidia pengo la uwezo wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mtu anasema ukienda kwa Chifu useme machache atakusikiliza, mengi ya nini? Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PASCAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache kuhusu hoja iliyopo mbele yetu. Lakini kabla sijasema yale ambayo nakusudia kuchangia kwenye hoja hii na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Mkutano huu wa 14 naomba basi na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kutoa pongezi za dhati kwa Wabunge mbalimbali ambao wamechaguliwa kwa nafasi mbalimbali ikiwemo nafasi ya Ubunge wa Bunge la Afrika, Uwakilishi wa *SADC* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda nichukue nafasi hii pia niweze kumpongeza sana Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Rais kuwa Mbunge katika Bunge letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nichangie machache tu kwa sababu Waheshimiwa Wabunge walio wengi waliotangulia wamekwishachangia maeneo mengi. Mimi mchango wangu zaidi utakwenda katika kutoa mifano hai ambayo itasaidia labda Serikali kuelewa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na hatua ya Serikali ya kuleta mabadiliko katika matumizi ya Bajeti ambayo ilikwishapitishwa ambacho kiwango chake ni shilingi bilioni 89.534.

Mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kwamba Serikali imetumia busara kubwa sana kuweza kubana matumizi yake ili iweze kuhudumia maeneo muhimu kama yale ambayo yameorodheshwa katika orodha ya Waziri ama ya Wizara ama ya Serikali kwa ujumla. Maeneo ambayo yanakusudiwa kuhudumiwa na kiwango hicho cha pesa ni yale ya elimu, pensheni ya wastaafu, fidia kwa Halmashauri za Wilaya, daftari ya wapiga kura, vitambulisho na kadhalika. Napenda niishukuru Serikali na kuipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa aliyekaa sasa hivi alivyosema sisi wa Kondoa kwa kweli tumeshukuru sana kwa busara hii ambayo imetumika kuweza kutenga pesa kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa ajili ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano tu wa sisi kule Kondoa, katika Bajeti za kawaida kwa kutumia vyanzo vyetu vilivyokuwepo tulikuwa tuna Bajeti ya shilingi milioni 750. Lakini kwa kuwa vyanzo vingi vilikuwa vya kero, Serikali ilifuta karibu vyanzo vyote na kwa vyanzo vilivyobaki tumebakiziwa kama shilingi milioni 52 tu ndiyo tunaweza kukusanya sasa. Maana yake ni kwamba tuna pengo la shilingi milioni 698.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa naishukuru Serikali kwamba imeona tatizo au umuhimu wa kutenga fedha za kufidia Halmashauri hizo na ninategemea kwamba Halmashauri ya Kondo itapewa fedha hizo ili iweze kuwahudumia wananchi. Naomba sana Wizara na Serikali kwa ujumla tuzingatie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ajabu yenyewe ni kwamba mpaka sasa tangu mwezi Juni tulipopitisha Bajeti hii fidia tuliyopata sasa hivi katika Wilaya ya Kondo ni shilingi milioni 195. Linganisha na pengo la shilingi milioni 698, unapewa milioni 195, utatoa huduma gani?

Naomba Serikali izingatie kama ilivyokubali kutoa vyanzo vya kero, naomba pia Serikali izingatie kufidia mapengo haya. Naomba sana. Vinginevyo niliwahi kusema katika bajeti hiyo kwamba Serikali isipochukua hatua za dhati Halmashauri zetu zitakufa na kama tusipochukua hatua za dhati kweli kabisa Halmashauri hazitaweza kufanya au kutekeleza wajibu wake.

Kwa hiyo, napenda nimshukuru sana na naishukuru Serikali na naomba hizo fedha shilingi milioni 698 zipatikane ili wananchi wa Kondo waweze kupata huduma muhimu kutoka Halmashauri yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, si Kondo peke yake bali Wilaya zote wapewe fidia ya mapengo hayo. Mimi nilikuwa natoa mfano tu wa Kondo hapa, lakini Wilaya zinazoathirika ni nyingi. Kwa hiyo, kwa kweli lazima suala hili lipewe kipaumbele kwa Bajeti ambayo imetolewa hapa ya shilingi bilioni 23 nafikiri ndiyo Bajeti halali. Ile Bajeti iliyokuwa imetolewa awali ya shilingi bilioni 4 ni hakuna kitu. Kwa hiyo, sasa ndiyo Serikali imeona umuhimu wa kutenga fedha za kutosha kuweza kufidia mapengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia hayo naomba sasa nizungumzie eneo la pili la makadirio ya matumizi ya nyongeza ya mwaka 2003/2004, ambayo kiwango chake ni shilingi bilioni 87.25. Ukiangalia vyanzo vyake havina matatizo, vyanzo kwamba ongezeko la ndani la mapato pia ongezeko la msaada wa Bajeti, kupunguza akiba ya Serikali katika Benki Kuu, hivi vyanzo havina matatizo. Kwa hiyo, mimi napenda niipongeze sana Serikali kwa kuzingatia na hapa nitoe pongezi za dhati kabisa kwa TRA, nafikiri ile bilioni 7.58 ni juhudi za TRA. Kwa hiyo, wamefanya kazi nzuri sana kwa kuvuka lengo na ndiyo maana hapa tunajivunia kwamba sasa tuongeze Bajeti ya Serikali. Kama wasingefanya hivyo tungekuwa na matatizo, kwa hiyo, napenda niwapongeze. Lakini pia niwapongeze kwa sababu Serikali imetumia mbinu ya ajabu ya kuleta Bajeti ya nyongeza bila kuongeza kodi. Kwa hiyo, nalo ni jambo la kupendeza sana. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kweli kwa hatua hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye matumizi. Matumizi yako ya aina tatu tu. Yale mawili mimi sina matatizo nayo, ndege ya Serikali na ile ya TANESCO sina matatizo nayo. Sasa tatizo lipo kwenye bilioni kumi ya kununulia chakula.

Mimi napenda kuishauri Serikali, hivi tunafanya takwimu, tunachukua takwimu kweli za tatizo la njaa ndiyo tunatenga fedha hizi au vipi? Naambiwa hapa kwamba Mikoa yenye shida kubwa ya chakula sasa yapata 17 katika nchi na naambiwa kwamba kwa wastani sasa hivi watu wenye shida sana ya njaa ni milioni kumi. Hebu gawanya bilioni kumi kwa milioni kumi upate, huyu Mtanzania unampa kitu gani? Unampa shilingi 1,000/=, hivi ndivyo tunavyotaka kuwasaidia wananchi kwa shilingi 1,000/=?

Mimi naomba kabisa kabisa, mimi nimeshtuka sana na makisio haya. Haya ni matatizo yale ambayo Wabunge wamekwishazungumza kwamba tunakwenda kutengeneza Bajeti bila takwimu, ndiyo matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama kweli waathirika ni watu milioni kumi, unawatengea bilioni kumi na kila mmoja kama ni chakula utampa chakula cha shilingi 1,000/=, hivi hicho chakula kitamsaidia kwa muda gani? Leo wewe ukipewa shilingi 1,000/=, itakusaidia milo mingapi, hata chai haitoshi? Sasa tunafanya mambo ya ajabu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba tuwe wakweli katika mambo ya msingi kama haya. Naomba kabisa hili suala ni ombi limetolewa na Wabunge wote hapa kwamba nyongeza itolewe. Mheshimiwa Khalid Suru, hapa kasema bilioni 25 inatosha, lakini haitoshi. Kwa hiyo, mimi ombi langu ni

kwamba Serikali iende kuangalia wapi inaweza kubana, ikaweza kutoa, wapi inaweza kuahirisha matumizi ikaokoa maisha ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khalid Suru, hapa ametoa mifano mizuri sana. Yeye alikuwa anasema tafsiri lakini vile vile mimi naweza kusema athari za njaa ni kubwa. Mimi katika Jimbo langu kuna maeneo ambayo yameathirika sana na athari zake ni nini? Ni kwamba kwa kuwa watu wamekosa chakula wanakula vitu vya ajabu kama mizizi, mboga, mchicha, ndiyo chakula cha wananchi sasa hivi. Matokeo yake wamevimba miguu hata wanashindwa kutembea, lakini bado hapa tunafanya kama mchezo mchezo wa kubishana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Vijiji vyangu 18 hakuna watu, watu wamekwishaondoka sijui walipo, sijui kama wapo hai na watarudi lini, sijui. Naomba jambo hili tuliangalie kwa uangalifu mkubwa. Tusifanye mchezo mchezo wa kubishana, tunazungumzia juu ya hatima ya maisha ya watu.

Sasa mimi katika maombi yangu naomba kwanza nivitaje Vijiji vile ambavyo hakuna watu sasa hivi. Kijiji kimoja mimi kabla ya kuja Bungeni hapa nimekwenda, nimekutana na mwalimu Mkuu tu. Nikauliza watu wako wapi? Akasema watu wamekwishaondoka, hakuna watu hapa. Kijiji kingine jana nilipigiwa simu kutoka Kondo, wanasema watu ishirini na mbili wapo Ofisi ya CCM, Kijiji hicho kinaitwa Handa, wapo Ofisi ya CCM hawana chakula wala nini, wamechangishana jana wamekula uji, sasa kesho sijui watakula nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Serikali iangalie Vijiji kama Pangalua, Hawelo, Humekwa, Babayu, Maziwa, Chase, Handa, Tumbakose, Rofati, Ndoroboni, Kisande, Dinae, Baaba, Wairo, Mpendo, Hamai, Lahoda na Gwandi. Hivi ni Vijiji ambavyo havina watu sasa hivi sijui watu wangu hawa wako wapi! Lakini sasa tunazungumza vitu vya ajabu.

Naomba wanaohusika waende kwenye Vijiji hivyo na wapeleke chakula ili wananchi warudi, wakipata habari kama wapo hai watarudi, kama wamekufa ndiyo hesabu zitachukuliwa ili Serikali iwe *charged* kwa ajili ya kusababisha vifo.

Kwa hiyo, naomba basi chakula kiwahishwe kwa Vijiji hivi ili wananchi warudi, watoto wasome na hii fedha iliyotengwa nao waweze kunufaika na fedha hiyo. Vinginevyo tusipofanya dharura ya kupeleka chakula watu watakufa.

Pili, nimesema kwamba fedha ziongezwe za kununua chakula, shilingi 1,000/= kwa mtu mmoja haitoshi. Tupige mahesabu siyo tunazungumza. Mimi nachangia hapa kwa masikitiko makubwa kwa sababu matatizo ni makubwa lakini hapa ukieleza wanakwambia tumekwishapeleka chakula. Tani 100 Kondo italisha nini? Hata uji hautoshi, lakini hapa tunajigamba kwamba tulipeleka chakula kila Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niunge mkono ili waongeze ile Bajeti ya chakula ili wananchi wapone. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa vile nami pia ni mara yangu ya kwanza kwenye Mkutano huu na mwaka huu kuzungumza hapa Bungeni, naomba nichukue fursa hii nikutakie wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kheri ya mwaka mpya wa 2004 na pia nawapongeza waliochaguliwa kwenye nyadhifa mbalimbali. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa hoja yake na naiunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwa kuanza kwanza na hoja ya ombi lenyewe kwenye hili kabrasha la njano lenye *Supplementary Estimates of Expenditure number one*, ukurasa wa kwanza penye maelezo. Chini ya maelezo mstari wa tatu kutoka mwisho penye maneno yanayozungumzia ongezeko la misaada ya bajeti na penye shirika lililotajwa pale *ADB* halafu kuna *SAL*, *PRBS*, hapo ndiyo nataka nipate ufafanuzi kidogo. *ADB* nadhani inaeleweka.

*SAL* nadhani sijui lakini nitapenda nieleweshwe vizuri zaidi nina imani pale ni *Structural Adjustment Loan* na kama ndivyo *SAL* kama ni *Structural Adjustment Loan* basi siyo shirika bali ni *facility*

na hao bila shaka ni watu wa Benki ya Dunia na huo ni mkopo na siyo *grant*. ADB bila shaka ni mkopo lakini tungeeleweshwa kama labda ni *grant* ya ADB. Hao PRBS kama ni Bajeti *support* labda hao ndiyo tungesaidiwa hapo.

Mimi *issue* yangu pale ni kwamba ni mikopo ambayo ilikuwa imekopwa kwa ajili ya shughuli nyingine na sasa tunachukua hela kutoka kwenye hiyo mikopo tunaingiza kwenye *Supplementary Budget* hii. Hapo nitaomba ufafanuzi na si kawaida sana kuona SAL inakwenda kugharamia *recurrent expenditure* si kawaida sana lakini huenda inawezekana, sielewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kuhusu suala ambalo limekuwa linazungumziwa na wengi, nalo ni suala la njaa hapa nchini. Suala la njaa mimi kwa maoni yangu ni suala pana na kwa upeo wangu ninavyoona ni suala ambalo huenda tukaendelea kuwa nalo kwa muda mrefu na mwaka huu inavyoonekana huenda tusiondokane nalo moja kwa moja. Huenda tukawa nalo na si ajabu sehemu kubwa ya mwaka ujao pia. Kwa sasa hivi tuna *mechanism* kama tatu hivi ambazo tunazitumia kujiandaa kukabiliana na hilo suala la njaa.

Kwanza ni *Strategic Grain Reserve* miundombinu yake ilivyo sasa hivi kwa maana ya miundombinu ya kuweka hifadhi ya nafaka kwanza haitoshi, kuna sehemu kabisa hazina miundombinu hii. Kwa mfano, jirani yangu ananiambia kule Kusini kabisa hakuna miundombinu ya aina hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, uhamasishaji wa wananchi kama *mechanism* nyingine na tatu ni wahisani pamoja na ununuzi kutoka nje ya nchi. Lakini hii hutumika baada ya njaa kuingia nchini, kwa hiyo, kwa kweli siyo mkakati wa kujiandaa kukabiliana na njaa.

Kwa hiyo, mikakati inayobakia kwa kweli ni *Strategic Grain Reserve* pamoja na kuhamasisha wananchi wetu wenyewe. Kuna mkakati muhimu unaokosekana na huo ni mkakati wa mtaji yaani mkakati wa fedha kujihami na njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti hii hizi bilioni kumi tumeona hapa waziwazi kwamba hazitoshelezi, lakini tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kutuonyesha kwamba kwanza zinapatikana. Kazi tunayomwomba ni kwamba bado hazitoshelezi na kwamba zipatikane zingine. Ambacho hatufahamu ni kwamba Bajeti hii itaathiri vipi maendeleo mengine pamoja na Bajeti nzima ya 2003/2004, hiyo hatuelewi. Naomba kushauri kama ifuatavyo kama mkakati wa mtaji wa kujihami na baa la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifikirie kuanzisha Mfuko wa Kujihami na Njaa, Mfuko huo uitwe kwa mfano *Njaa Fund* au *Disaster Fund* au Mfuko wa Maafa. Serikali kuu ichangie huo Mfuko kila mwaka kupitia taratibu zake za Bajeti. Pia ni kuwa na Halmashauri za Wilaya zichangie huo Mfuko kwa njia ya hisa. Mfuko ufanye kazi kama bima ya njaa au maafa.

Kwa njia hiyo, nchi nzima itashiriki kuchangia maafa na kufanya maandalizi, wote tushiriki bila kungojea mpaka tunapata matatizo, kwa hiyo, tunapata matatizo ya kuanza kutafuta twende wapi na tupate jinsi gani tu-*deal* na tatizo tunalokuwa nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huu wa njaa nchini tuombe wale ambao tuna madeni yao wasitishe riba na *charges* nyingine kwa kipindi tangu Julai, mpaka labda Julai, 2005 ili *sarvings* ambazo tutazifanya kutokana na riba ambazo tungezilipa kwa ajili ya ku-*service* madeni yao tutumie hizo kwa ajili ya kuwekeza kwenye Mfuko kama huu ambao tutauanzisha kama ikikubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watu ambao wanaathirika ambao labda hawafikiriwi. Kuna watu ambao sidhani wanafikiriwa kwenye msaada wa kukabiliana na madhara ya njaa, hawa ni waajiriwa wa kima cha chini. Kwa kuwa bei ya chakula kwa ujumla imepanda (*purchasing power*) ya mishahara yao imeshuka kwa kiasi kikubwa na wao wanaathirika kuweza kujikimu maisha yao na ya familia zao kwa mfano kama tunavyosikia hapa kwamba gunia la mahindi limefika mpaka shilingi 40,000 na bei ya vyakula vingine. Mimi nashauri kama ifuatavyo:-

Kwamba wale wanaowaajiri uwepo utaratibu wa kuwawezesha waweze kukabiliana na upandaji wa bei ya chakula na kushuka kwa *purchasing power* yao. Kwa mfano, wanaweza wakapewa posho ya kujikimu kwa kipindi cha njaa mpaka itakapokwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu *TANESCO*. Nakubaliana na baadhi ya Waheshimiwa ambao mimi ni mmoja wao ninaodhania kwamba *TANESCO* ni shirika la kibiashara na kwa hiyo, lisingestahili kupata ruzuku kutoka Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu pekee ambayo nakubaliana na dhana ya ruzuku ni kuunga mkono jitihada za Serikali za kuongeza thamani na ufanisi wa *TANESCO*. Hii ni kawaida ili ku-*clean balance sheet* yao ili kuliandaa hilo shirika kwa ubinafsishaji ambao pia nauunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo naunga mkono mia kwa mia hoja ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. YETE S. MWALYEGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Bajeti ndogo. Kwanza kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza toka Bunge hili limeanza kipindi hiki napenda niwatakie Wabunge wote na wewe mwenyewe kheri ya mwaka mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Rais kuwa Mbunge. Vile vile Wabunge wote waliochaguliwa katika Bunge la *SADC* na Bunge la Afrika, hongereni sana kwa ushindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kidogo tu suala la ukame. Wizara ya Kilimo na Chakula na Wizara ya Ushirika na Masoko na hasa kule Mbeya. Kwa sababu ya ukame nchi yetu ina njaa na suala hili la ukame huwa linatokea kila baada ya muda. Ninavyokumbuka mwaka 1974/1975 kulikuwa na njaa, ikaja tena 1984/1985, ikaja pia 1994/1995 na sasa 2004/2005 na huenda mwaka kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni suala ambalo ni *cyclic* linajulikana, kwa hiyo nilikuwa naomba tu Wizara ya Kilimo na Chakula ihakikishe kwamba mbali ya kuwa na *reserve* za chakula kunakuwa na mfumo ambao unatengwa kutokana na Bajeti ya Serikali ili uweze kutumika wakati wa njaa. Fedha inatengwa kutokana na Bajeti ya Serikali ili iweze kutumika wakati wa njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa upande wa Mbeya hali si mbaya sana ila kuna maeneo yana njaa lakini hali si mbaya kama sehemu zingine. Napenda kusema tu kwamba kwa upande wa Mbeya tatizo kubwa ni Pareto.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamelima Pareto, wameuza Pareto, hawajalipwa. Wananchi wanayo Pareto kwenye majumba yao bado hawajauza, kiwanda cha Mufindi ambacho kipo chini ya mwekezaji mmoja kina matatizo, hawana *capital*, fedha au mtaji wa kununua Pareto.

Kwa hiyo, wananchi wamepoteza muda mwingi sana na sasa hivi wanashindwa kununua chakula. Hicho ndiyo chanzo cha njaa. Sasa hivi wanashindwa kusomesha watoto na mahitaji yao mbalimbali kwa sababu ndiyo zao walilokuwa wanalitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana katika Bajeti hii mweke fedha za kununulia Pareto kwa sababu kuna tani zaidi ya 150 za Pareto ambazo hazijanunuliwa na kuna zingine zaidi zilizouzwa lakini hawajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamenituma wanataka hizo fedha, tafadhali sana. Kwa sababu unapozungumzia njaa, kuna njaa ya kukosekana mapato na kuna njaa ya kukosekana kwa fedha. Wananchi wangu hawana fedha za kununulia chakula lakini walilima Pareto na hawajalipwa fedha zao. Tafadhali sana hili naomba Serikali iliangukie na itenge fedha kwa ajili ya Pareto. Naomba sana hilo lieleweke na tutaelewana kama fedha hizo zitatengwa.

La pili, hii Wizara ya Nishati na Madini shilingi bilioni 37.2, napenda tu kukubaliana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba Serikali yetu iangalie uwezekano wa kuanzisha Mradi wa Mchuchuma mara moja. Wakati wanafanya haraka kuanzisha huo mradi wasije wakafanya makosa kama yale ya *IPTL*, wawe waangalifu.

Kwa hiyo, wasije wakarudi hapa wakasema, mlisema fanyeni haraka, aah! Siyo haraka kiasi hicho. Kwa hiyo, tunaomba msije mkachukulia *loop hole* hiyo kwamba Waheshimiwa Wabunge mlisema bwana tunakwenda sasa, aah! Tunaomba muwe waangalifu wakati mnafanya maamuzi hayo ya kutumia mkaa wa mawe. (*Makofi*)

Vile vile mafuta haya yanayotumika pale Ubungo, Dar es Salaam *Jet -A-1* mafuta ya ndege. Mafuta ya ndege ni sawa na mafuta ya korobo ni sawa na *kerosene* ila yamesafishwa zaidi na mafuta haya yanaagizwa kwa fedha nyingi na zinaombwa hapa fedha kwa ajili ya kununulia mafuta na vilevile kwa ajili ya kulipa *IPTL*. Niseme tu kwamba Serikali inatakiwa iongeze mapato kutokana na uingizaji wa mafuta. Uingizaji wa mafuta sasa hivi umekuwa holela. Kwa sababu *TPDC* zamani walikuwa wanasimamia uingizaji wa mafuta, na sasa hivi wameachiwa wanaingiza kiholela.

Kwa hiyo, naweza kusema kwamba kwa kweli hii biashara sasa ya mafuta haina msimamizi na haina mwenyewe, na ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge tunasema hapa kwamba *EWURA* ianze mara moja, tafadhali sana ili waweze kusimamia. Vile vile bei ya mafuta inakuwa inapanda kila wakati, tunajua kabisa kwamba kuna ongezeko kidogo, lakini bei iliyopandishwa hapa haina msimamizi watu wanaongeza tu, kwa hiyo wanachukua *advantage*. (*Makofi*)

Vile vile uingizaji wa mafuta tulishauri hapa kwamba tufunge mita pale bandarini na tenda ikatangazwa, lakini ukiuuliza sasa hakuna anayejua mita itafungwa lini? Kwa sababu fedha kwenye mafuta ni nyingi mno, kwa hiyo, kuna kusuasua kufunga ile mita, watu wanataka wale kwanza. Tunaomba maelezo kamili kulikoni? Kwa sababu mita ilitakiwa ifungwe mwezi Desemba ili Bajeti ya kuanzia mwezi Januari hadi mwezi Julai, fedha ziwe zimeingia za kutosha. Mtu anapewa *invoice* pale kwenye mita na siyo unakwenda kwenye matanki kupima, hapana. Kwanza unapokwenda kupima kwenye matanki kule ile fimbo anayokupa ile *deep stick*, hivi ndiyo yenyewe ya lile pipa, huna uhakika, kwa hiyo utapata maajabu kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba nilifanya kazi kwenye sekta hii ya mafuta kwa muda wa miaka 23 kwa hiyo, najua kuna wizi sana. Kama tutakuwa na mita yetu pale bandarini hiyo ndiyo itatuongezea mapato, kwa sababu kutakuwa hakuna udanganyifu. Naomba tu nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kufuta zile *bonded warehouses* yale matanki wanayokuwa wanaibia mafuta. Hii imepunguza kidogo na kuongeza kidogo Pato la Serikali, lakini bado inatakiwa iongezeke zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni huu ukaguzi wa dhahabu bilioni 9.6 kwa mwaka, nilikuwa napendekeza tu kwa sababu hii ni kufanya *chemical analysis* ya zile *sample* za yale madini au yale mawe yanatoka pale na kujua yakienda yana kiasi gani cha dhahabu cha *copper* na kadhalika. Sasa kwamba utamuajiri kwa mwaka mzima nenda rudi, mwaka mwingine, mwaka mwingine.

Nilikuwa nadhani hii kwenye Mkataba lazima kuwe na *capacity building* ya kusomesha watu wetu ili huyu mtaalamu anayekuja awe anafanya kwa muda tu. Halafu anawaachia watu wetu., hizo ni fedha nyingi sana. Haiwezekani ukawa na Bajeti ya bilioni 10 na zaidi kwa ajili ya kufanya analysis tu. Ni vizuri hizo fedha zikatumika kununua vifaa kwenye migodi, halafu wale wafanyakazi wa Wizara wanapofanya kazi pamoja na watu wa *TRA* wanakuwa pamoja ni timu moja na ndiyo wanaojaza fomu zile zote. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hii iwe kwa muda tu siyo miaka yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niongelee kidogo kuhusu hili la shule. Wanafunzi wamefaulu wengi sana na Mkoa wa Mbeya umefanya vizuri na umekuwa wa kwanza Kitaifa na nilikuwa naangalia matokeo *average pass mark* ni asilimia 65 karibu. Mkoa wa pili *average* 52 kwa hiyo wameachwa kwa mbali sana. Nampongeza sana *REO* ambaye ni mama amefanya kazi nzuri sana na vilevile naipongeza

Serikali kwa kuongeza Bajeti kwa ajili ya wanafunzi hao na sisi wenyewe tumejitahidi tumejenga shule nyingine nyingi zaidi na tunawashukuru sana kwamba nyingi zimekubaliwa. *(Makofi)*

La mwisho, ni hili la ndege nimpongeze Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwa kutueleza wazi na kutugawia hii nakala ya *Internet*. Mimi nimeisoma nimeona kumbe hawa watu wa Kambi ya Upinzani hawajui Kiingereza. Tatizo kweli kabisa wala siyo utani, tatizo ni mtu kutokuelewa kilichoandikwa ni nini?

Kwa hiyo, tatizo kubwa sana ni kwamba hawaelewi Kiingereza iko wazi kabisa. Sasa wamekuja hapa wanasema uongo badala ya kusema yaliyoandikwa. Nilikuwa nadhani *next time* wachukuliwe hatua. Kwa sababu mimi mwenyewe nimesikitika sana niko Kamati ya Miundombinu na suala hili la ndege tumejadili sana na wenzetu wa Kambi ya Upinzani walikuwepo. Nimeshangaa sana leo wanazungumza vitu ambavyo havipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge zimebaki dakika tano tu na hizo hazitoshi kumpa mtu mwingine nafasi kuweza kuchangia. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 01.39 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 17 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*